Kikao cha Nne - Tarehe 02 Oktoba, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani hati ya Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Ame Haji Ali (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Maagizo ya Kamati ya mwaka 2016/17 kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Suleiman Makame Ali (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Spika, Kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 87

Majibu ya Mawaziri na Manaibu Mawaziri Kuakisi Kauli ya Mhe. Rais

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Mhe. Spika, ahsante sana, kabla ya kuuliza swali langu na mimi nikupe pole kwa mujukumu mazito uliyokuwanayo na leo hatimaye tumekuona baada ya siku tatu kuku-*miss*, naomba serikali ijibu swali Nam. 87 swali la wananchi.

Katika hotuba yake ya Baraza la Eid el Fitri, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein aliwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kujibu hoja na maswali ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, licha ya ugumu wa baadhi ya maswali na hoja za wajumbe.

Je, pamoja na pongezi hizo, Mawaziri na Manaibu Mawaziri wamejipangaje mwaka huu wa fedha kutekeleza ahadi mbali mbali walizozitoa wakati wa kuijibu hoja hizo za Wajumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 serikali kupitia Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wamejipanga vizuri kutekeleza ahadi mbali mbali walizozitoa katika kufikia ufanisi na utekelezaji wa ahadi hizo kwa mujibu wa sheria, miongozo na taratibu zilizowekwa na serikali. Aidha, serikali ina utaratibu wa kutekeleza ahadi zinazotolewa kwa kutumia bajeti iliyoombwa kwa mwaka wa fedha husika na kwa kupitia fedha za ndani na fedha za wahisani kwa maendeleo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza maswali madogo sana ya nyongeza.

Kwa kuwa ofisi hii ndio inayosimamia shughuli za serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na naomba kuinukuu kifungu cha 43(5) "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya Sera ya Serikali kwa ujumla, na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar".

Kwa kuwa ofisi anayoiongoza Mhe. Naibu Waziri ndio yenye majukumu ya mawaziri na manaibu waziri na kumekuwa na kilio cha muda mrefu ndani ya Baraza hili kuahidiwa mimi suala la wananchi wa Michamvi, nilisema tukea dunia kuanza mpaka hapa tunapoendelea leo hawajapata maji kutoka kwenye mfereji au bomba na ahadi hiyo imeshaahidiwa muda mrefu. Ni lini itatekelezwa kwa vitendo ili nipate usingizi na mimi kuweza kupata kulala.

La pili, Mhe. Spika, juzi ulikuwa hupo hapa Mhe. Mwanaidi Kassim aliuliza swali Nam. 135 na jawabu likajibu kwamba, tunaona kuwa uongozi wa Shirika la Bandari utakuwa na maelezo zaidi juu ya mipango katibu wa jengo hilo na hapo baadae.

Mhe. Spika, huyu swali hakuuliza Kwamtipura wala Paje kauliza ndani ya chombo hiki na alikuwa apate jawabu ndani ya chombo na ndio wajibu wa kisheria. Kwa hivyo hili suala lini litarejeshwa tena ili Mhe. Mwanaidi Kassim apate kujiridhia ili wananchi wake wapate kumuunga mkono zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, samahani nimuombe Mhe. Jaku Hashim arudie swali lake la kwanza aili tupate kumsikia vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwa kuwa ofisi hii ndio inayosimamia shughuli za serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na naomba kuinukuu kifungu Katiba ya Zanzibar Kifungu cha 43(5) "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya Sera ya Serikali kwa ujumla, na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar" kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

Nilichomuuliza, kwa kuwa ofisi hiyo ndio inayosimamia shughuli za serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, nimeahidiwa ndani humu kwa kipindi kirefu kuwa shughuli ya huduma ya maji Michamvi itafika. Nilisema mara nyingi na mimi nilikuwa nikikosa usingizi kwa muda mrefu na kupewa ahadi nyingi na mawaziri na wakafika mpaka mawaziri kutamka chochote ninachotaka hupewa humu ndani, lakini naona bado ni mdomo tu vitendo havijafika. Ni lini ahadi hiyo itafika kwa wananchi wa Michamvi kwa vitendo ili wapate maji na mimi nipate usingizi niweze kulala.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza lazima tukubaliane sote kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi *time phrase* yetu ni miaka mitano na Ilani ya Chama cha Mapinduzi inahitaji kufanyiwa utekelezaji na serikali kwa kipindi cha miaka mitano, na hili ambalo Waheshimiwa Mawaziri wamelisema dhamira ya kuhakikisha wananchi wa Michamvi wanapata maji ndio dhamira ya serikali wala sio dhamira ya mtu mwengine. Dhamira ya Mhe. Waziri kutoa ahadi ile ni ahadi iliyokuwemo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, lazima Mhe. Mjumbe hapa tukubaliane naye kwamba bado tuko katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na tuliomba ridhaa kupitia Chama cha Mapinduzi kwamba wananchi watupe ridhaa kwa kipindi cha miaka mitano na ndani ya miaka hiyo lazima Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Paje aiulize serikali sasa kama Michamvi maji yatakuwa yamefika. Lakini kwa kuamini mipango ya serikali na mipango ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa dhamira waliyokuwanyo namhakikishia Mheshimiwa wananchi wa Michamvi watapata maji salama ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano. *(Makofi)*

(b) Swali lililoulizwa na Mhe. Mwanaidhi Kassim ingawa halikuwa ni miongoni mwa swali la msingi, lakini dhamira na kinachofanywa na Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri ni kuhakikisha wanatoa majibu yaliyokuwa bora. Lakini pia muuliza swali na yeye kwa mujibu wa kanuni anapata fursa ya kuuliza swali la nyongeza ili apate maelezo zaidi. Sasa kama litakuwa limetokea kwa njia yoyote muongozo tunaoupata au ambao mawaziri sote tulioupata kutoka serikalini kupitia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwamba sote tuna wajibu kutoa majibu yaliyokuwa bora na sahihi hasa kwa

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi maana hawa wanauliza maswali kwa niaba ya wananchi wao. Kwa hiyo, tunachokiamini kilichotoka na kilicotolewa na wizara kitakuwa kimestahiki na kimesadiki, lakini kama kutakuwa kuna jambo jengine ni vyema sasa muuliza swali akarudi tena wizarani ili tukaweza kupata uhakika wa kile ambacho kimeelezwa zaidi. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa ruhusa lakini nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, naomba kuongezea majibu ya nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar siku zote imekuwa ikichukua hatua mbali mbali ya kuleta maendeleo katika nchi hii, katika nchi yetu utaona mabadiliko makubwa ya sekta mbali mbali kwa namna tulivyofikia na hasa sekta ya maji nchini.

Mheshimiwa nchi yetu ilikuwa ni nyumba kidogo sana ndani zenye mifereji na maji yanatoka, lakini sasa kwa zaidi ya asilimia 80 wananchi wa Unguja na Pemba wanapata maji ndani ya nyumba zao. Msingi wake ni kwamba hatua mbali mbali zinachukuliwa. Ukichukulia mfano wa kijiji cha Michamvi hatua kubwa zimefikia pale kutizama hali ya maisha yao ujenzi wa barabara, ujenzi wa nyumba na kadhalika unaendelea. Nataka nimhakikishie utaona suala la umeme namna Michamvi lilivyokuwepo.

Mhe. Spika, nataka nikuhakikishie suala la maji katika eneo hilo linafanyiwa kazi na muda sio mrefu maji yatatoka na hivi sasa serikali inachukua hatua mbali mbali za kusaidia kupatikana maji katika eneo hilo. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi naye anapofanya wajibu wake wa kusaidia wananchi wake hakuna sababu ya kulalamika isipokuwa aendelee kusaidia wananchi wake na serikali iko nyuma yake inamuunga mkono tunaendelea kufanya kazi ili kutekeleza wajibu wetu na kuhakikisha suala la maji Michamvi linamalizika. Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yana mwelekeo wa kuisaidia nchi yetu. Lakini katika majibu yake amesema serikali imejipanga vizuri katika utekelezaji wa zile ahadi ambazo ziliulizwa katika suala la msingi. Swali langu liko kama ifuatavyo:

Ni asilimia ngapi ya fedha za bajeti iliyopatikana kwa wizara zote hadi sasa katika utekelezaji wa ahadi hizo. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kifupi swali la Mhe Miraji Khamis Mussa ni suala ambalo linahitaji takwimu na kwa kawaida kwa sasa Wizara ya Fedha na Mipango inajitahidi sana, kadiri ya mahitaji ya kila sekta huwa yanapatiwa karibu asilimia mia moja ya mahitaji hayo. Kwa hivyo, nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba swali lake linahitaji takwimu na tutahitaji kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha tuweze kujua hayo ambayo anayataka na tutamjibu kwa maandishi. Lakini nataka nimhakikishie kwamba kwa sasa Wizara ya

Fedha inachukua hatua za ziada katika kuhakikisha inaingiza fedha kwa wakati. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 97

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2014/2015 zimeonesha kwamba Wizara za Serikali, Mashirika, Taasisi pamoja na Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na wahisani kwa kipindi hiki imefanya vizuri hadi kufikia kupewa hati isiyo na shaka.

Je, nini hatma kwa taasisi ambayo kwenye ukaguzi wa nyuma waligundulika kufanya ubadhirifu na kusababisha hasara au upotevu wa fedha za umma.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 97 lenye kifungu (a) na **(**b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika**,** Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ina jukumu la kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba.

(b) Mhe. Spika, katika ripoti ya ukaguzi Mdhibiti hubainisha upungufu na mafanikio yaliyogundulika katika ukaguzi huo. Hatma ya taasisi ambazo zimegundulika kufanya ubadhirifu na kusababisha hasara au upotevu wa fedha za umma ni serikali kuzichukulia hatua taasisi hizo kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri ambayo ameyatoa ya kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kwishakufanya ukaguzi na kutoa taarifa huwa hana jukumu jengine. Kwa sababu kule Bara wenzetu ni juzi tu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alitoa amri ya kuwa wale watu wote ambao walibainika kuwa wamefanya ubadhirifu wa fedha za umma katika ripoti yao wachukuliwe hatua na wapelekwe mahakamani, warejeshe zile fedha na wachukuliwe hatua za kisheria. Lakini yeya kwenye jibu anasema kwamba wakimaliza hapo huwa wamemalizanaje.

(a) Je, haoni kwamba kama *CAG* hana hata kanuni ya kumdhibiti mtu baada ya kumkagua kwamba kafanya ubadhirifu wa pesa sa serikali hili ni tatizo la kisheria.

(b) Kama hilo lipo ni lini serikali itaipa mamlaka *CAG* kuweza kuwachukulia hatua za kuwashtaki na kuwapeleka mahakamani baada ya ukaguzi kugundulika kwamba kuna

watu au taasisi zilizoshiriki katika kufanya upotevu wa fedha za serikali. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa wale watu ambao wataonekana kwamba wana hatia bila shaka serikali haitoweza kuwafumbia macho na wanaweza wakachukuliwa hatua za kinidhamu pamoja na kupelekwa mahakamani.

(b) Mhe. Spika, swali la lini hawa wahalifu wataweza kupelekwa mahakamani, nimwambie tu kama wapo serikali haitomfumbia macho yeyote yule ambaye amehusika na suala la ubadhirifu. Kwa hivyo, atapelekwa mahakamani wakati wowote uchunguzi utakapokamilika.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Spika,

Mhe. Spika: Samahani Mheshimiwa kuna majibu ya ziada kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake sahihi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nitoe taarifa ndogo tu kwamba jukumu la kuwaadhibu wale wanaokutikana na ubadhirifu wa fedha *CAG* keshakwenda kaja na ripoti na huwa tunaiwasilisha hapa Barazani Mheshimiwa na *PAC* ndio baadae wanafuatilia na baadae kuleta ripoti hapa tunajadili, jukumu lile liko kwa wakuu wa taasisi zile zinazohusika kuwachukulia hatua za kufaa. Kwa hivyo, ni suala la ambalo ni la kweli.

Lakini la pili tayari sasa hivi Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu wako katika hatua za mwisho katika kukamilisha kanuni ambazo zinatasaidia kuweka mambo madago madogo kama haya kuyaweka sawa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza:

(a) Mhe. Spika, Mhe. Waziri ni taasisi ngapi zilizobainika na zilizochukuliwa hatua.
(b) Ni taasisi gani ambazo zimechukuliwa hatua.

Mhe. Naibu Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuwa hili suala la kitamwimu basi nimwambie tu Mheshimiwa tutaleta kwa maandishi.

(b) Vile vile suala la (b) litakuwa linajitosheleza baada ya kujibu hili suala la (a) kwa sababu nitazileta kwa maandishi kwa sasa hivi sitoweza kutoa jibu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, tunaamini katika taasisi zetu mbali mbali matatizo yapo na hujuma mbali mbali zinatokea katika maeneo hayo. Lakini katika jibu lake Mhe. Waziri alitwambia tu kwamba utaratibu mzima uliokuwepo maamuzi yanatokea na taasisi husika zinachukuliwa hatua. Kwa bahati mbaya hatujasikia ni hatua gani.

Je, Mhe. Waziri kwa kuliangalia hili ambalo ni kero kwa nchi yetu na pato la nchi linapotea katika sehemu mbali mbali wizara ina mkakati gani kwa makusudi kwa dharura hii baada ya kupokea taarifa kutoka katika kamati yetu ya mahesabu, inachukuwa hatua gani za dharura ili kulihami hili lisiendelee katika katika sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kumjibu Ali Suleiman Ali suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, hatua ambazo tutakazoendelea kuzichukuwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na ufatiliaji wa zile taasisi ambazo kero zile zimeibuka na kuhakikisha kwamba wanazifatilia ipasavyo.

Nam. 22
Upatikanaji wa Cheti cha Kuzaliwa

Mhe. Suleiman Sarahan Said:– Aliuliza**:**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi sana kusaidia kila sekta katika kuleta maendeleo, hata hivyo suala la usajili wa vyeti vya kuzaliwa hasa Pemba, bado kuna matatizo ya kupatikana kwa vyeti hivyo ambapo watoto wanafika kupelekwa skuli bado hawajapatiwa vyeti hivyo.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.
(b) Ni sababu gani za msingi zinazopelekea mpaka kutokea hali hiyo.
(c) Je, kuna elimu yoyote iliyotolewa kuhusu umuhimu wa vyeti vya kuzaliwa na mara ngapi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali inafahamu kuwepo kwa tatizo la upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa hapa nchini na siyo kwa upande wa Pemba pekee, bali pia kwa Wilaya nyengine za Unguja.

(b) Mhe. Spika, sababu zinazopelekea kutokea kwa hali hii mara nyingi huwa ni uchache wa magamba ya kuchapisha vyeti na madaftari ya usajili. Tatizo hili husababishwa na uhaba wa fedha za kutosha kuweza kulipia huduma za uchapaji na mara nyengine hata kama fedha zimepatikana na kulipwa, upatikanaji wa magamba na madaftari hayo kutoka kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali umekuwa ukichelewa kwa maelezo kwamba kiwanda huzidiwa na kazi zinazowasilishwa hapo na Taasisi mbalimbali za Serikali ama upungufu wa malighafi zinazohitajika.

Mhe. Spika, Matatizo mengine yanayochangia hali hii ni uchache wa wafanyakazi hasa wa Wilayani kulinganisha na hali halisi ya vizazi vinavyozaliwa pamoja na uchakavu wa vitendea kazi. Hata hivyo, hatua kadhaa zimechukuliwa kukabiliana na hali hii ikiwemo:-

i) Kulipa deni lililokuwa tukidaiwa kwa muda mrefu na Wakala wa Uchapaji.
ii) Kutuma maombi serikalini ya kuongeza watendaji wa Taasisi.
iii) Kufanya mageuzi ya mfumo wa usajili kutoka huu wa "*manual*" ambao unatumia zaidi karatasi na "*typewriters"* kwenda katika mfumo unaotumia kompyuta kwa Wilaya zote.

(c) Mhe. Spika, Suala la utoaji wa elimu kuhusu umuhimu wa vyeti vya kuzaliwa limekuwa likitiliwa mkazo sana ingawa mara kwa mara hushindwa kukamilika kutokana na sababu mbali mbali. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha uliopita Ofisi iliweza kutoa elimu hiyo kwa Masheha wa Mkoa wa Mjini Magharibi na kurejea tena mara baada ya uteuzi wa Masheha wapya. Katika mwaka huu wa fedha Ofisi imepanga kuendelea kutoa elimu kama hiyo kwa Masheha wa Mikoa mingine Unguja na Pemba pamoja na kuandaa vipindi vya redio na televisheni.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimsifu sana Mhe. Waziri kwa majibu wake mazuri ambayo yamekwenda kwa kina lakini nitoe suala la a na b.

(a) Kwa kuwa cheti cha kuzaliwa ni muhimu sana katika kila eneo ambalo mtu akitaka kupata stakabadhi yake kama *passport* na vitu vyengine ni lazima awe na cheti cha kuzaliwa. Kwa hivyo, kama cheti cha kuzaliwa hana au bado hajakipata na mtu yule anataka kusaifiri nje ya nchi kwa ajili ya kupata *passport*.
Je, kuna stakabadhi yoyote ambayo anaweza akaitumia ili akajulikana kama cheti kimo kwenye *process*.

(b) Ni lini suala hili litamalizika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwaidhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Saraha Said suala lake la nyongeza lenye a na b kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza nataka nilibaliane nae kwamba cheti cha kuzaliwa ni *document* muhimu sana ambayo kila mwananchi na kila raia anastahiki kuipata. Hata hivyo hivyo, nataka niseme kwamba suala la mwananchi anapotaka kusafiri ni lazima apate *passport* ya Tanzania na bila ya kupata *passport* huwezi kusafiri. Hivyo, hata kama utapewa *temporary document* yoyote ile haisaidia kama kutakuwa hakuna *passport* isipokuwa juhudi inafanywa na serikali kwa wale ambao wanahitaji vyeti vya kuzaliwa wavipate kwa wakati ili na zile haki zao za msingi nyengine ziweze kupatikana.

(b) Napenda Mhe. Spika, nilieleze Baraza hili tukufu kwamba hivi sasa tupo katika mchakato wa kuhakikisha kwamba mfumo mpya wa usajili wa wa matuko ya kijamii tunauandaa mpya kwa mujibu wa sheria ambayo itasomwa kwa mara ya kwanza kwenye Baraza hili na kupitishwa kwenye mkutano ujao. Baada ya huo mfumo kukamilika haya matatizo mengi ambayo yanaonekana sasa yatakuwa yamepatikana ufumbuzi wake kwa sababu tunarajia kwamba kila wilaya itakuwa itaingia katika mfumo mpya wa *electronic* baada ya kwenda na mfumo huu wa *manual*.

Mhe. Minyihaji Makame Mwadini: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali langu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba kuna wimbi kubwa hivi sasa la udanganyifu wa vyeti za kuzaliwa watu wana-forge na kupata vyeti vya kuzaliwa. Je, wizara yako imejipanga vipi kupambana na suala hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwaidhini yako naomba kumjibu Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nataka nikubaliane nae kwamba lipo wimbi la udanganyifu na ndio maana serikali tumeamua kuunda upya mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii na kama nilivyokwisha kujibu ni kwamba baada ya kuingia kwenye mfumo mpya ambao utaunganisha baadhi ya taasisi ambazo zinatoa huduma na shughuli nyengine ni imani yangu kwamba suala hili tutaweza kutoa vyeti kwanza vitakavyokuwa huwezi kuzihushi na wala huwezi kufanya udanganyifu wowote. Ahsante sana.

Mhe. Amina Idd Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kumuuliza Mhe. Waziri suala la nyongeza:-

Mhe. Waziri kwa kuwa taasisi yako ina matatizo mengie sana na moja ya matatizo kuna baadhi ya watu wamezaliwa Pemba lakini sasa hivi vyeti wamebadilisha na kuvifanya wamezaliwa Unguja. Je, Mhe. Waziri unalijua hili na kama unalijua umejipanga vipi katika kuhakiki vyeti vyote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwaidhini yako naomba kumjibu Mhe. Amina Idd Mabrouk suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Sina taarifa za kutosha kama hilo alilolisema mwanzo linalohusu Pemba na Unguja kama linatokea. Lakini kujipanga vipi ni kama jibu langu nililotoa katika majibu yangu ya msingi, majibu ya nyongeza ya Waheshimiwa Wawakilishi wawili ambao wametangulia kusema. Bado nataka niendelee kusema kwamba tunakwenda kwenye mfumo mpya huu mfumo tunaokwenda nao hizi shughuli nyengine za udanganyifu zitakuwa hazipatikani.

Lakini katika kukabiliana na hilo mfumo huu utakuwa unatoa cheti pahala pale ambapo umezaliwa. Kwa hivyo, kama sasa hivi kuna wimbi hilo tayari limejitokeza maana yake tukianzisha mfumo huu jambo hilo litakuwa halipo kwa sababu nia hasa ni kuhakikisha kwamba kila mwananchi wa Zanzibar anapata haki yake ya msingi na anaipata katika eneo ambalo amezaliwa. Ahsante sana.

Nam. 13

Kuwawezesha Vijana Kujiajiri

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma– Aliuliza**:**

Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 kuna ahadi ya kuanzisha *“Green House” k*wa kila Wilaya za Zanzibar kwa lengo la kuwasaidia vijana kujiajiri na kuondokana na utegemezi wa ajira Serikalini. Hata hivyo, mpaka leo hatujaona utekelezaji wake.

Je, Serikali imefikia wapi katika kutekeleza ahadi hiyo kwa vijana wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu**:**

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye na yeye anaendelea kutupa pumzi zake na asubuhi hii tukaweza kusimama katika Baraza lako tukufu tukiwa na afya njema.

Mhe. Spika, naomba naomba uniruhusu niweze kuchukua nafasi hii kuweza kutoa mkono wa pole kwa Mhe. Bihindi Hamad Khamis ambaye amefiliwa na baba yake mzazi. Tumuombe Mwenyezi Mungu ampe subira katika kipindi hichi kizito.

Baada ya hapo Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwamba katika kuwawekea mazingira mazuri vijana juu ya kilimo endelevu na cha kisasa, Wizara yangu ilianzisha uanzishaji wa *Green House* katika eneo la Tunguu, Chokocho na Makombeni, lakini hadi sasa hakukuwa na ufanisi wowote

kutokana na hali halisi ya mazingira ya Zanzibar. Hivyo, wizara yangu imebadilisha programu hii ya uanzishwaji wa *green house* na badala yake kuwaendeleza vijana katika kilimo endelevu cha kisasa kupitia program mbali mbali ikiwemo fursa kijani, kuimarisha miundo mbinu ya maji kwa kuwachimbia visima, wizara kwa kushirikina na Program hii, imeshajihisha vijana 396 (190 Unguja na 206 Pemba) kuendeleza kilimo endelevu na cha kisasa. Kati ya hao, vijana 60 (wanawake 30 na wanaume 30) waliunganishwa na Programu hiyo.

Baada ya mafunzo hayo vijana 18, (wanawake 6 na wanaume 12) waliajiriwa na Mradi wa Maendeleo ya Mji wa Fumba. Aidha, chini ya programu hii, Wizara imegharamia vijana 10 (wanaume 6 na wanawake 4) ili kupata mafunzo hayo. Pia, Wizara imesaidia vikundi 9 vya vijana kuchimbiwa visima, vilivyoonesha bidii katika shughuli za kilimo cha kisasa Unguja na Pemba. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake aliyotupa vijana. Naomba kumuuliza swali lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kutokana na majibu ya Mhe. Waziri nilikuwa nataka kujua je, wizara inapinga na majibu ya Mhe. Rais.

(b) Mhe. Waziri katika majibu yale ametwambia kuna visima 9 vimechimbwa kwa ajili ya kuwaendeleza vijana. Je, Mhe. Waziri ni maeneo yepi na sehemu gani ambazo zimechimbwa visima 9 za kuweza kuwasaidia vijana hao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Naomba nikuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hatuna nia ya kupingana na maagizo ya Mhe. Rais sisi tunafanya kazi kwa ajili ya kumsikiliza Mhe. Rais. Lakini kama nilivyomjibu suala langu kutokana na mazingira ya Zanzibar ndio imeshindikana kufanya *green house* kama ilivyokusudiwa mwazo.

(b) Ametaka kujua katika visima 9 tulivyosema tumewachimbia vijana ni sehemu gani na sehemu gani. Naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba katika sehemu ya Unguja na Shehia ya Pongwe, Donge na Mbuzini na Maungani Pemba Tibirinzi Wilaya ya Chake Chake, Mgogoni Wete, Mgagadu Wilaya ya Mkoani na Tondooni Wilaya ya Micheweni. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a).

Mhe. Waziri umesema kwamba unawawezesha vijana kwa kuwachimbia visima ili kujiendeleza na kilimo. Je, mpango huu utakuwa ni endelevu au ndio kwa hizo shehia hizo tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali suala lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika uanzishwaji juu wa visima baada ya kufanya tafiti zetu na tukaona suala hili tutafanikiwa, kwa hivyo, nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba mradi huu utakuwa ni endelevu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nimpongeze Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa maswali yake aliyojibu. Mhe. Spika, mimi nataka niulize kwa ufupi.

(a) Kwanza kabisa tunaamini *Green House* ilikuwa mkombonzi kwa vijana wetu katika maeneo mbali mbali. Lakini kwa bahati mbaya ilipoanzishwa *Green House* hii haukuzingatiwa ushauri wa mapema. Nataka kuuliza hapa je, wizara katika kufanya tafiti zake kwa mradi huu ambao ni mzuri ulikuwa na mafanikio ilifanya utafiti sehemu gani.

(b) Je, kabla ya kufanya walifanya utafiti wowote kuhakikisha kwamba mazingira yetu hayafai?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wangu na maswali aliyouliza Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele. Nataka kusema kwamba utafiti wa awali ulifanyika na tukiamini kabisa kwamba utaendelea vizuri. Lakini baadae baada ya kuwa tumeshaanza kutengeneza *green house*, sehemu zote ambazo tumepitia tumekuta kwamba mimea inapokuwa inaanza kuota na kutoa maua, maua yanapuputika. Tulitafuta watu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ambao tunaendelea kushauriana nao na wanaendelea kuchukua *sample* ili kuona kwamba labda *sample* za awali hazikuweza kuwa nzuri zaidi, kutokana na ardhi yetu na hali ya hewa iliopo kwamba ni ya joto na tunaendelea kufanya hivyo. Kwa hivyo, tunaamini kabisa kwamba tukifanikiwa tukaona kuna tatizo lipi, tutaendelea kuendeleza *green house*, kwa sababu ni kitu ambacho unaweza kulima kwa msimu wote ikiwa kitafanikiwa vizuri ahsante Mhe. Spika.

Nam. 21

Uchumaji wa Zao la Karafuu

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kupandisha bei ya zao la karafuu kwa asilimia 80. Lakini bado zao la karafuu lina tatizo la wachumaji wa karafuu ambapo bado uchumaji wao ni kupanda juu sana hasa kwa mikarafuu mikubwa.

(a) Je, kwanini Serikali haiwapi wachumaji karafuu mikanda maalum ya kujizuia wakati wakichuma karafuu.

(b) Kwa nini Serikali haiwakatii bima wenye mashamba ya karafuu kwa ajili ya wachumaji wao ili kupata nafuu ya matibabu pindi ikitokea ajali na kuipunguzia mzigo Serikali.

(c) Je, kuna utaratibu gani mzuri kwa Serikali uliojifunza katika nchi za wenzetu zenye mikarafuu katika uvunaji wa karafuu na pindi mchumaji akipata ajali.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuhusu juhudi zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza zao la karafuu.

(a) Ipo tofauti baina ya mikarafuu ya Zanzibar na baadhi ya nchi nyingine, Mikarafuu mingi ya nchi hizo ni mifupi na rahisi kutumia ngazi maalum. Hivyo, kutokana na jinsi mikarafuu yetu ilivyo, sio busara kutumia mikanda kwa wachumaji wa karafuu, kwani inaweza kusababisha uharibifu kwa mikarafuu yenyewe na ni vigumu kupanda mti wa mkarafuu kwa mkanda kama ilivyo kwa mnazi.

Kuhusu utaratibu wa kutumia ngazi kama vile ambavyo nchi za Asia ikiwemo Indonesia na Sri Lanka na kadhalika zinafanya, utaratibu huu pia ni mgumu kutokana na kuwa mikarafuu mingi ni mirefu sana na pia serikali haijaifanyia utafiti juu ya njia bora ya kuchuma zaidi ya hii tuliozizoea. Serikali inaendelea kuwataka wachumaji wa karafuu kuwa na tahadhari wakati wa zoezi la uchumaji karafuu ili kuepuka ajali zinazoweza kuepukika.

(b) Serikali ina utaratibu wa bima kwa ajili ya watu wanaopata ajali katika uchumaji karafuu na inawalipa ipasavyo inapotokea ajali. Serikali haina bima kwa ajili ya watu wenye mashamba ya karafuu. Kwa mwaka 2015/16, watu 89 walionguka walilipwa kiasi cha TZS. 83,450,000. ZSTC mwisho wa mwaka ililipa Shirika la Bima kiasi cha TZS 126.5 millioni kwa kipindi cha mwaka 2016/17.

(c) Serikali imeshajiwekea utaratibu mzuri wa kuchuma karafuu mwaka huu, pamoja na utaratibu wa kulipa fidia kwa wachumaji wa karafuu watakaopata ajali. Mwaka huu, kiasi cha TZS 127.0 millioni zimetengwa kwa ajili ya ajali hizo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar karafuu ni uti wa mgongo na Rais wa Zanzibar amejitahidi kupandisha bei mpaka asilimia 80 ya zao hili kwa mlaji, hilo kwanza nimpongeze. Lakini kwa kuwa serikali zao hili ni zao muhimu sana na kama alivyoseme Mhe. Waziri kuhusu watu wanavyopanda mikarafuu na kuhudumia na matatizo mengine, lakini baadae hufika *ZSTC* na kuuza karafuu zao, lakini bado kuna hofu na kuna tatizo watu wananung'unika kwamba zile mezani ni za kizamani.

Je, nimuulize Mhe. Waziri serikali haioni umuhimu wa kubadilisha mezani za kuweka zile *computerise* na lini linaweza kuondoka tatizo hili ili kuondoa hofu za wauzaji karafuu ili waridhike na kipimo kile cha karafuu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Suleiman Sarahan Said kama ifuatavyo. Ni kweli kuna malalamiko mengi wanasema wenzetu wanaouza karafuu *ZSTC* kwamba mezani inawapunja. Lakini pia mezani za kizamani, kwa upande wa Kituo cha Mkoani mezani nyingi zimebadilishwa na zimewekwa mezani za kisasa. Lakini pia suala la kwamba mezani za zamani na mezani za sasa hivi za *electronic* zipi ambazo ziko sahihi. Pia kuna matatizo vile vile ya wakulima wenyewe wanapokuwa hawaziweki karafuu zao vizuri, matokeo yake karafuu zao zinapokwenda kupimwa zinakuwa zimeshapata *damage*. Kwa hivyo, uzani ule unapokuwa nao nyumbani anapokuwa ameziweka na kule zinatofautiana.

Mhe. Spika, lakini suala hili tunalitizama tena ili kuona ni kwa kiasi gani tunaweza kuweka mitani ambazo zitaridhisha. Sisi Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tuna kitengo cha mezani ambacho kinatizama mezani zote za nchi nzima. Kwa hivyo kazi hiyo itakuwa ni endelevu. Tumeshaanza Mkoani na kwengine ambako tutaona kuna mezani ambazo ni za kizamani nazo zitabadilishwa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa kuweka utaratibu mzuri wa kuchuma na kuuza karafuu. Lakini mbali na utaratibu huo, kuna taarifa serikali kupiga marufuku kuokota karafuu za mpeta kwa wananchi hususan kinamama.

Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha kupiga marufuku uokotaji wa karafuu za mpeta?

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli tumepiga marufuku karafuu za mpeta na hatukupiga marufuku kama sisi Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Ni vikao halali vilivyokaa, kuna *Task force* ya Taifa, na kuna kuna *Task force* sasa hivi za Pemba kwa kila Wilaya.

Mhe. Spika, ndani ya *Task force* tume-*review* utaratibu mzima wa uchumaji na ukusanyaji wa karafuu. Moja lililozungumzwa kwa kila sehemu ni kwamba mpeta una madhara. Kwanza unawadhalilisha wanawake. Wanawake wanatoka mfano wa Micheweni wamejipura wamevaa kila kitu, unajua wanawake wa Kizanzibari walivyo wanavyopendeza, anakwenda zake Mkoani kukusanya mpeta, hii inaleta sintofahamu ndani ya familia na wasichana wengi wamedhalilishwa katika mikarafuu huko kwenye mpeta. Kwa hivyo, tukasema hili jambo la kwanza ambalo limeona tulizuwie.

Lakini jambo la pili katika utaratibu mzima wa magendo, masuala ya mpeta yanachangia magendo, kwa sababu yule anayeuza mpeta wanakuja wananunua katika vichochoro na maeneo mengine, lakini hatuna hakika kama karafuu zile zinakwenda kuuzwa katika vituo ambavyo tuliviweka.

Mhe. Spika, na mwaka huu naomba niseme kwamba mwaka huu hali halisi ya Pemba iko *tight* sana. Serikali imefunga bahari zote, vyombo vyote vinatizamwa na yoyote ambaye anauza karafuu akiuza karafuu kwa mujibu wa sheria ambayo tumeipitisha basi atachukuliwa hatua. Kwa hivyo, tumeona kwamba mpeta unasababisha hilo na tumelipiga marufuku, na tutaendelea kusema mpeta hauruhusiwi, atakayekamatwa na mpeta atachukuliwa hatua.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Pamoja na matatizo ya ajali za kuanguka kwenye mikarafuu, lakini hivi sasa kuna tatizo la suala la utoro kwa wanafunzi katika maeneo mengi yanayochumwa karafuu. Lakini vile vile kuna tatizo hili la mali kwa mali ambalo ameligusia kidogo.

Je, serikali inafahamu hivyo, na ni hatua gani ambazo za kuweza kudhibiti hali hizi ili wananchi wetu kuepukana na kuingia katika matatizo,. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwanza naomba nitowe tu taarifa kwa pamoja kuhusu ajali za mikarafuuni. Mimi nilikuwa Pemba nimerudi jana, lakini ajali zimeanza kuwa nyingi kidogo, lakini zaidi ni Mkoa wa Kaskazini Pemba. Mkoa wa Kaskazini Pemba katika ajali 39 zilizopatikana nyingi zao ziko Kaskazini Pemba. Mimi jana nilikwenda pale nikamkuta mtoto mmoja alianguka katika mkarafuu Mtambwe Kinyasini, ikabidi na yeye apelekwe hospitali.

Kwa hivyo, natoa wito kwa ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi, hasa mliotoka huko na wengine hapa mnayo mikarafuu huko, muwaelimishe kwa sababu hayo mambo tumeyaona kule Pemba kwa udadisi wetu sisi kuwauliza wenye makambi, hasa Kaskazini inaelekea kwamba wachimbaji wa karafuu wa Kaskazini hawana uzoefu wa kutosha sana wa kupanda kwenye mikarafuu kama walivyo watu wa Kusini, kwa sababu Kusini wanawatumia wale wale ambao waliwaajiri katika miaka ya nyuma. Lakini kama mnaelewa hali ya Kaskazini ni kwamba sasa hivi wameshajihika wengi ambao wanaingia katika mikarafuu ni watu wapya, lakini wanajua kwamba ni eneo la kupata chochote. Kwa hivyo, ndio maana tunaona ajali Kaskazini Pemba zimekuwa nyingi kushinda Kusini. Kwa hivyo, nawaomba muwashajihishe sana na muwape hadhari sana wale ambao wanapanda kwenye mikarafuu kule na hasa wengi vijana wawe na hadhari katika kupanda na kuchuma.

Kuhusu suala la utoro wa wanafunzi. Mhe. Spika, tumeona kweli na takwimu zipo. Kuna shule nyengine utakuta katika wanafunzi tuseme zaidi ya 300, basi wanabakia wanafunzi 40 au 50 kote Kaskazini na Kusini, na hili jambo limeingia kwa Pemba nzima. Kwa sababu hii taarifa tuliipata juzi tulivyokuwa tupo Pemba kwenye kikao chetu, tunategemea kwamba leo watendaji wa *Task foce* na watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali watakaa pamoja, kwa sababu hili jambo ni tishio kwa watoto wetu.

Mhe. Spika, hapo nyuma tulisema kwamba wanafunzi wasiende kuchuma karafuu, kwa sababu akianguka kwenye mkarafuu mtu ambaye yuko chini ya miaka 18 hawezi kupewa Bima. Kwa hivyo, tulisema na tukatoa tangazo, na naomba nirudie tena kipindi hiki. Tafadhalini wazazi musiwapeleke watoto wenu kwenda kupanda kwenye mikarafuu, kwa

sababu atakapoanguka akivunjika mgogo au mkono basi Shirika la Biashara za Zanzibar haliwezi kumlipia Bima, sio kwamba halitaki, lakini sheria za Bima zinataka mtoto awe kijana wa zaidi ya miaka 18. Kwa hivyo, sisi binafsi tunapiga marufuku watoto kwenda kwenye mikarafuu lakini limeshakuwa sugu, tutakaa na wizara inayohusika ili waongeze nguvu kule Pemba.

Mhe. Spika, ingawa Mkoa hasa Mkoa wa Kusini wameshaanza kulichukulia hatua jambo hili, lakini tutafanya kazi ya ziada ili kuitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wahakikishe kwamba wanafunzi wanaendelea na wanasoma, na wazazi nao msiwe na tamaa ya kwamba mtapata pesa ya kuchuma karafuu na kuchambua karafuu, lakini watoto wanaathika.

Mhe. Spika, mwisho ilikuwa kuhusu suala la mali kwa mali nilizungumzie kwamba hili hatukubaliani nalo na tumelipiga marufuku. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 17

Hatua Zinazochukuliwa na Serikali Katika Kuimarisha Ufaulu wa Wanafunzi

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa jitihada zake za kuendeleza elimu Zanzibar kwa kujenga skuli nzuri na kuwapa uwezo walimu, ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu nzuri na yenye mafanikio. Lakini katika skuli za Serikali bado matokeo ya mitihani kwa wanafunzi ni mabaya na ya kuvunja moyo.

(a) Je, Serikali inalichukuliaje suala hili la kutofaulu kwa wanafunzi.

(b) Je, Serikali imechukuwa hatua gani za dharura na za muda mrefu kulipunguza au kuliondoa kabisa tatizo hilo.

(c) Je, Serikali imefanya utafiti gani kujua kasoro ambazo zinapelekea kutofaulu kwa wanafunzi wanaosoma skuli za serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo: -

Mhe. Spika, matokeo ya mitihani kwa ngazi ya Sekondari ya kidato cha nne ni mazuri kwa skuli za Serikali kulinganisha na Skuli za Binafsi. Matokeo ya mwaka 2016 kwa mfano, yanaonesha kuwa Skuli ya Lumumba na Skuli ya Fidel – Castro ndio skuli zilizoongoza katika mitihani hiyo ya kidato cha nne kwa Zanzibar. Hata hivyo, kwa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari ya awali, Skuli za binafsi zinafanya vizuri katika mitihani yao kulinganisha na skuli za serikali. Hii inatokana na wingi wa watoto katika madarasa.

Kwa mfano Skuli ya Kinuni ina wanafunzi zaidi ya 200 kwa darasa, uhaba wa walimu na vifaa kwa baadhi ya skuli, mashirikiano duni ya wazazi kwa walimu na matumizi mabaya ya mitandao kwa wanafunzi. Ukweli ni kwamba suala la kutofaulu kwa wanafunzi ni miongoni mwa masuala yanayopewa umuhimu mkubwa na wizara yangu na serikali kwa ujumla. Hatua mbali mbali zinachukuliwa katika kuhakikisha kuwa suala la ufaulu mdogo wa wanafunzi linapatiwa ufumbuzi wa kudumu kutokana na umuhimu wake. Hatua hizo ni pamoja na kuajiri walimu hasa wa sayansi wenye sifa, kuwapunguza walimu katika sehemu za mijini na kuwapeleka sehemu zenye upungufu wa walimu hasa mashamba, kuwapatia walimu mafunzo kazini, kununua vifaa vya maabara na vitabu vya kiada na ziada kila hali inaporuhusu.

Mhe. Spika, **w**izara yangu imeandaa utaratibu wa ziara za mara kwa mara za Wakurugenzi wa Idara kuzitembelea skuli zote za Unguja na Pemba, kufuatilia utendaji kazi wa walimu pamoja na kuangalia changamoto zinazowakabili na kuzipatia ufumbuzi.

Aidha, wizara kwa kushirikiana na Shirika la Watu wa Marekani kupita programu yake ya "Tusome Pamoja" tumeanzisha umoja wa walimu na wazazi wa wanafunzi (UWAWA) katika skuli za msingi, kwa lengo la kujenga mashirikiano yatakayosaidia kupunguza changamoto katika kujifunza kwa wanafunzi katika skuli zao. Hatua hii imeanzishwa kwa kuamini kwamba ushiriki wa wazazi katika mchakato mzima wa upatikanaji na utoaji wa huduma hii ya elimu unasaidia kupunguza changamoto zinazowakabili wanafunzi, walimu na uongozi wa skuli, hali itakayopelekea kufanya vizuri katika masomo yao kuanzia ngazi ya elimu ya maandalizi na msingi na hatimae kufanya vizuri katika elimu ya sekondari na elimu ya juu au ya ufundi.

Aidha, wizara kupitia Baraza la Mitihani limeandaa tathmini ya mitihani na kuiwasilisha kwa wadau wa elimu wakiwemo walimu wakuu, wakuu wa taaluma na wenyeviti wa kamati za skuli kwa lengo la kuona matokeo ya wanafunzi na kujadili sababu zinazopelekea ufaulu wa mitihani usioridhisha kwa madarasa ya nne, sita na kidato cha pili kwa Skuli za Serikali. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake yenye ufasaha. Lakini kidogo naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa shule zetu zinafanya mitihani kwa Kiingereza na kwa kuwa shule nyingi za binafsi zinaanza *kinder garden* kwa lugha ya Kiingereza na ndio wanapopatikana wanafunzi wazuri. Lakini katika shule za serikali labda kuanzia darasa la tatu ndio wanaanza Kiingereza.

(a) Je, hawaoni mfumo huu unawalemaza watoto na kubadilisha kuanza shule kwa darasa la kwanza kwa Kiingereza.

(b) Pamoja na majibu mazuri, lakini kuna tuhuma kwamba kuna baadhi ya walimu ambao hawasomeshi na kujihusisha na siasa, na hata Dk. Shein alipokuwa katika ziara zake kule Pemba, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alisema kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ifanye uchunguzi kwa wale walimu ambao wanajishughulisha na siasa na sheria ichukuwe mkondo wake.

Je, kuna walimu wowote wenye tuhuma hizo na waliokwishapewa adhabu?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, tuliwahi kusema kwamba lugha ya kufundishia kwa mujibu wa sera ya elimu katika shule za msingi, hasa msingi wa awali ni lugha ya Kiswahili. Lakini msingi ya juu, kuanzia darasa la tano na sita hapa tunatumia Kiingereza, na hapa inatumia kwa skuli zote.

Kwa hivyo, ule utata wa kuhamisha lugha ya kufundishia kutoka Kiswahili zinafanana katika skuli za binafsi na skuli za serikali. Kwa hivyo hakuna utata wowote katika suala hili.

(b) Kuna tuhuma kwamba baadhi ya walimu wanajishughulisha na shughuli za siasa wakiwa kazini. Tuhuma hizi zipo na sisi kama wizara tumeanza kuzifanyia kazi kwa kufuatilia nyendo za walimu mbali mbali wakiwa skuli. Suala hili tumelianza mapema zaidi, zaidi ya mwaka mmoja tunawafuatilia, na tumekuwa tukishirikiana na masheha. Tuliwahi kuzungumza katika mikutano ambayo tulifanya Unguja na Pemba, kwamba masheha mtakapopata fununua kwamba kuna walimu ambao wanafanya siasa katika mazingira ya skuli basi tupeni taarifa hizo. Kwa bahati mpaka sasa bado hawajatupa taarifa, lakini sisi wenyewe pia kama ni wizara tunaendelea kufanya uchunguzi. Hadi sasa bado hatujampata mwalimu yeyote ambaye tumethibitisha kama anafanya hivyo lakini uchunguzi unaendelea. Ahsante

Mhe. Said Omar Said: Ahsante, Mhe. Spika na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa kufaulu kwa wanafunzi kunatokana na mitihani na kwa kuwa mitihani hiyo wasimamizi ni walimu. Je, ni walimu wangapi waliofanya udanganyifu katika usimamizi wa mitihani ya mwaka jana na ni hatua gani zilichukuliwa dhidi yao.

b) Wizara imejipangaje kuhusu kuvuja kwa mitihani ambayo inapelekea watahiniwa kupata *credit* wakati mitihani imefanywa vichakani.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mpaka sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali bado haijapata takwimu za idadi ya walimu ambao walifanya udanganyifu katika mtihani wa mwaka wa jana hakuna taarifa hiyo..

b) Kuhusu uvujaji wa mitihani ni kwamba katika mitihani rasmi hakuna ripoti yoyote inayohusisha uvujaji wa mitihani yetu ya kidatu cha nne, cha sita na darasa la nne na sita. Na kuhusu usimamizi wa wanafunzi ni kwamba hili walimu

wanalifanya kwa umakini sana na kwa maana hiyo hakuna ripoti ya aina yoyote iliyoripotiwa Wizarani kuhusu suala hilo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi nimuulize tu suali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kwa kuwa katika mtazamo wa kawaida au takwimu zinaonyesha kwamba suala la elimu kwa upande wa Zanzibar limeshuka ukiangalia katika miaka 70, 80 na nyuma hasa wakati wa chama kimoja na kuelekea vyama vingi. Nini kauli ya serikali kwamba je, turudi katika mfumo wa chama kimoja au tubakie hapa ukiangalia suala la elimu sasa linazidi kuporomoko na hata katika jinsi wanafunzi wanavyofanya katika maskuli yetu.

b) Kwa kuwa katika jimbo langu la Tunguu Wadi ya Ubago katika maeneo yangu ya Dunga kumekuwa kuna muamko mkubwa kwa wazee pamoja na akina baba na akina mama katika kuhakikisha vijana hasa wenye vipaji maalum wanajiendeleza kimaisha na kimasomo ili waweze kwenda mbele. Ni utarabu gani unaotumia Wizara yako kuwatambua vijana wenye uwezo au vipaji maalum ili kuhakikisha ule uwezo wao unaendelezwa kwa ajili ya maslahi ya nchi pamoja na wao wenyewe. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa swali laki lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amani inaamini kwamba kwa mujibu wa takwimu tunazotumia kwamba viwango vya ufaulu katika sekondari kidatu cha nne na cha sita bado ni mazuri Zanzibar ni tofauti na maoni yake. Hii tumejaribu kutafuta takwimu katika kipindi ambacho tumeona ufaulu upo katika asilimia 94. Sasa asilimia 94 sidhani kama ufaulu mdogo.

b) Kuhusu suala la kutambua vipaji ni kwamba Wizara ya Elimu kwa kweli iko makini sana katika suala hili. Tumeanza kutafuta vipaji vya taaluma lakini pia na fani nyengine za michezo kuanzia darasa la sita mitihani yetu tunayoifanya kwa kweli madhumuni yake Namba 1 ni kuibua vipaji, sasa vile vipaji vinavyoibuliwa vya taaluma ndivyo wanavyopangiwa katika skuli maalum vinaendelezwa na wanafikia hatua ya juu kabisa. Mifano hii tunayo, tunao wataalamu wengi sana amepitia katika mfumo huu kuibua vipaji.

Lakini pia katika hatua hii ya kuibua vipaji tunaibua mkondo mwengine tunaibua vipaji vya michezo, kupitia mpango wetu maalum ya kuendeleza michezo na kwa sasa tumeibua vipaji vingi hasa katika jimbo la Mhe. Said Omar tumeibua vipaji vya sanaa vipo vingi katika jimbo lake kule. Ili kuona vipaji tunaviibua mapema zaidi ndiyo Wizara ya Elimu ikaja na mtihani wa darasa la nne, nao pia madhumuni yake ni kuibua vipaji. Ahsante sana.

Uhifadhi wa Mashamba ya Karafuu Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Mhe. Spika, kwa kuwa shamba la Wizara ya Kilimo liliopo Makuwe lina *"Block 10*" na jumla ya hekta 79.9 ambapo *"block No. 4"* ya shamba hilo lina pori kubwa sana liliopo karibu na bahari ambapo inakuwa rahisi kwa watu wabaya kuziiba karafuu zilizomo ndani ya shamba hilo.

(a) Je, ni sababu gani inafanya shamba hilo likaendelea kuwa porini hadi leo.

(b) Je, kwenye *block 5* na 6 ya shamba hilo, Mikarafuu mingi sana imekufa ni sababu gani hadi leo ikashindikana kuipanda mikarafuu mengine kujaza nafasi ya mikarafuu iliokufa.

(c) Ni lini Wizara itaongeza wafanyakazi katika shamba hilo ambao wataweza kulitunza shamba hilo ikizingatiwa kwamba wafanyakazi (6) waliopo kwa sasa hawatoshi hata kwa ulinzi tu wa shamba hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, inakubaliana na hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba shamba la Mikarafuu la Makuwe lina *plot 10* ambazo *plot No. 4* ya shamba hilo lina pori inakuwa rahisi kwa watu wabaya kuziiba karafuu zilizomo ndani ya shamba hilo. Wizara ya Kilimo inafahamu kuwa hii ni changamoto kubwa ambayo wizara yangu inatakiwa kuifanyia kazi ili kupunguza uwezekano wa kutokea wizi ndani ya shamba hilo.

(a) Mhe. Spika, Shamba la Makuwe kutokana na rutba nzuri iliyopo eneo lile haichelewi kuota majani kwa haraka na kupelekea kuwa na pori. Kutokana na uhaba wa wafanyakazi wa kulihudumia shamba hilo, Shamba hili huwa linasafishwa pale ambapo Wizara yangu inapopata pesa za kufanyia kazi hiyo.

Mhe. Spika, napenda kumjuilisha Mheshimiwa Mwakilishi kwamba katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita kuanzia Juni hadi Agosti 2017 *plot* 5 katika shamba hilo zilisafishwa ambazo ni *plot* namba 4, 6, 7, 8 na 10. Usafishaji huo umesaidia kuepusha wizi wa karafuu kwa plot ambazo zilikuwa na pori kubwa ikiwemo *plot* namba 4.

Mhe. Spika, *plot* namba 5 na 6 ambazo zina mikarafuu iliyokufa napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mwakilishi kwamba juhudi zimeanza kuchukuliwa za kupanda mikarafuu mipya katika *plot* hizo. Hivi sasa imo mikarafuu mipya iliyopandwa yenye umri kuanzia miaka 2 mpaka miaka 7. Aidha, katika juhudi za kuliendeleza zaidi shamba hili, Wizara inaandaa Mpango wa Usimamizi wa

Shamba la Makuwe wa miaka mitatu – 2017/2020 *(Management plan)* ambao utabainisha hali halisi ya mahitaji ya fedha, vifaa na idadi ya wafanyakazi wanaohitajika katika kuliendeleza shamba hili.

Mhe. Spika, Miongoni mwa kazi muhimu zilizoanishwa ndani ya mpango huo ni pamoja na suala la kupanda mikarafuu katika maeneo ya wazi kwa kutumia ajira za vipindi maalumu.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu inafahamu kwamba wafanyakazi waliokuwepo hapo kituoni ni kidogo sana, hawakidhi hata mahitaji ya ulinzi wa shamba hilo. Hata hivyo Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na uvuvi inafanya jitihada za kuomba ajira kwa ajili ya kuliendeleza shamba la Makuwe kila mwaka. Kwa mwaka huu wa fedha, Wizara imeomba kupatiwa wafanyakazi wapya 12 ili kutimiza idadi ya wafanyakazi 18 ukijumuisha na wale wafanyakazi 6 waliopo hivi sasa.

(c) Mhe. Spika, ili kukabiliana na hali hiyo Wizara yangu inaendelea kuwatumia kwa umakini wafanyakazi wachache waliopo na vile vile hivi karibuni tutakamilisha mpango wa usimamizi wa shamba hilo ambao utatoa muongozo juu ya uendelezaji wa shamba hilo. Mpango huu utabainisha mahitaji ya wafanyakazi pamoja na kutoa ajira kwa vipindi maalumu pale wanapohitajika kwa kazi maalumu kwa ajili ya kuliendeleza shamba hilo. Mpango huu unatarajiwa kuwasilishwa serikalini hivi karibuni.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ashante Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza tokea niingie kwenye Baraza hili leo ndio naanza kusema kwamba jibu langu silo nililolitegemea kutokana na uzoefu wa kazi hii. (*Makofi*)

Napenda kuthibitisha kwamba majibu haya sipendi nisimame na kanuni lakini siyo kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza mimi nalifahamu vizuri shamba hili na nalifahamu sana lilivyo na shamba hili Mhe. Spika, limefekewa *plot* moja sivyo kama alivyoeleza. *Plot No. 4* ambayo haikusafishwa na Wizara imesafishwa na mtu waliyomkodisha ambapo usafishaji wa kukodisha Mheshimiwa sisi tunaujua ni wa kwenda kukata watu wakapata kuchuma.(*Makofi*)

a) Sasa mimi namuuliza Mhe. Naibu Waziri tu swali langu dogo kwamba upo tayari tufuatane mimi na wewe twende kwenye hizo *plot* tukathibitishe kama kweli zimesafishwa. (*Makofi*)

b) Twende tukaithibitishe hiyo mikarafuu ambayo imepandwa kwenye hiyo *plot No. 5* na 6 kama ulivyojibu ni hayo tu. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa suala lake (a) nimesikia yale maneno ya mwanzo tu aliyoniuliza kwamba niko tayari mengine sikuyasikia kutokana na makofi ya Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali ni kwamba je, upo tayari kufuatana naye. Yale maelezo ya mwanzo yapo yaache jibu hilo swali tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, nipo tayari kufuatana na naye. (*Makofi*)

Kwa hilo la (a) tu lakini kwa maelezo zaidi katika tarehe 18 nimekwenda mimi mwenyewe binafsi ziara yangu ya Pemba na nimeiona *plot No. 4* ipo safi lakini sijui maelezo yako unayosema kwamba aliyokodishwa kwamba ndiye aliyesafisha kwa maelezo yetu sisi kama Wizara tumemtafuta mtu tumemlipa na amesafisha *plot* hiyo.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali na nyongeza.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri mashamba ya mikarafuu kuachwa kuwa pori kama ivyoelezwa na mtangulizi wa swali ni kuwapa mori wizi kwenda kuiba karafuu lakini sio kuiba tu hata kutia moto inakuwa rahisi sana kama inavyoendelea sasa hivi kisiwani Pemba.

a) Swali langu ni kwamba ikiwa Wizara imeshindwa kuyashughulikia haya mashamba kuna tatizo gani la Wizara kushindwa kuwapa wananchi wadogo wadogo wakawakatia wakashughukia mashamba na wakapanda mikarafuu mengine wakajiendelea katika kupata kipato.

b) Je, kama serikali haiwezi kufanya kazi hiyo mimi ninavyojua uajiri wa serikali sasa hivi ni mzito utafika miaka mikumi mikarafuu ile itapotea. Lengo la Serikali ni kuhakikisha mikarafuu ambayo ndiyo zao la taifa linashughulikiwa ipasavyo. Ni kwa nini basi serikali isitowe uhuru kwa wananchi wakayashughulikia mashamba yake wakati wananchi wakidharau mashamba yao wananyang'anywa na serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumpenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

a) Kabisa serikali bado haijashindwa kulishughulikia shamba hili la Makuwe. Katika jibu langu mama nimesema tunahitaji wafanyakazi 12 ili kukamilisha wafanyakazi 18 kuliendeleza shamba hili na kulishughulikia.

b) Kama nilivyosema kwamba serikali bado haijashindwa kwa hivyo haipo tayari kuligawa na kuwapa wananchi shamba hili litaendelezwa na serikali kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika: Majibu ya nyongeza kutoka serikalini, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, ambayo ameyatoa baada ya kuyafanyia utafiti.

Vile vile naomba uniruhusu niongezee majibu ya swali la Mhe. Hamad Abdalla Rashid kama hivi iafuatavyo:

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba mashamba haya kama Makuwe, serikali inaendelea kuyabakisha kwa ajili ya kutengeneza vitalu kwa ajili ya miche mbali mbali ya mazao ya biashara na mazao ya matunda. Kama azma ya serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilivyokusudia.

Jibu jengine ambalo ameliuliza Mhe.Hamad Abdalla Rashid kwanza nataka nimpongeze sana kwa lile swali alilouliza je, haya mashamba ina mpango gani serikali ya kuwagaiya wananchi.

Nataka nimuhakikishie kwamba kama ilivyo Sera iliyoanza tangu wakati wa Afro Shirazi Pati, ambayo ilitekelezwa na Mhe. Abeid Amani Karume kwa kuwagaia wananchi heka tatu tatu bado sera ile ipo na hivi sasa serikali imefanya utaratibu kwanza wa kuyajua mashamba yake yote ambayo yalikuwa yanaelekea kupotea. Baada ya kwisha kuyajua kwa kiasi fulani karibu asilimia 80 ya mashamba hayo tumeyatambua na kazi inaendelea. Baada ya kukamilika kwa kazi hiyo basi serikali inao mpango kabambe kabisa kwa yale mashamba ambayo hayana wananchi ya kuwagaia wananchi heka tatu tatu ili kuweza kutimiza Sera ile yetu ya kuwapa wananchi ardhi kwa heka tatu tatu. Ahsante sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze sana Waheshimiwa wote wawili waliojibu masuali haya lakini ningependa nimuulize suali dogo Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

a) Mhe. Waziri umetwambia kwamba shamba hili pale ambapo Wizara inapopata fedha ndipo mnatafuta watu wanakwenda kulipalilia shamba hili. Je, ni watu wangapi ambao wanakwenda kulipalilia shamba hili na ni vifaa gani vinavyotumika kulipalilia shamba hili lote na kwa muda gani.

b) Na je, ni fedha kiasi gani ambazo mnatumia kuwalipa hao watu wa kawaida ili kulipalilia shamba hili na kwa nini msiwaajiri kabisa. Kwa sababu itakuwa ni kitu endelevu kila siku kumtafuta mtu mmoja mmoja kumpa fedha kwenda kulipalilia shamba hili kuliko ile kumuajiri akawepo pale mfanyakazi akaendelea kufanya kazi ile ya ulinzi pamoja na wale wenziwe waliokuwepo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, kama nilivyosema katika swali langu mama tunahitaji kuwaajiri watu hawa ili waweze kufanya kazi hizi kwa ufanisi na kwa muda wowote pale ambapo wanahitajika.

b) Katika swali lake alilosema kwamba ni kiasi gani tunatarajia kulipa labda niseme kwamba swali hili naomba nimjibu kwa maandishi ili tuweze kupata idadi kamili kabisa. Uliposema tunatumia vifaa gani tunatumia mashoka, kwa sababu kuna miti mikubwa mikubwa yale ambayo ni misitu na yale ya kufyekea. Vifaa hivyo ndivyo tunavyotumika kwa ajili ya kusafisha mashamba hayo.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali langu naomba nitoe maelezo kidogo kwamba majibu niliyopokea yapo tofauti na swali langu ambalo nililouliza. Kwa hivyo ningeomba sana Wizara kwa sababu hii tabia imekuwa, kwa sababu wiki iliyopita pia tulipokea majibu tofauti na masuala ambayo tunakuwa tunauliza. Kwa hivyo tungewaomba sana ...

Mhe. Spika: Samahani Mheshimia unaondosha swali au vipi.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Siondoshi swali nimetoa maelezo kwamba majibu niliyopata yapo tofauti na swali langu nililouliza. Kwa sababu hii paper iko tofauti majibu na swali lake. Hata hiyo yako wewe Mhe. Waziri kama utaiangalia nahisi iko hivyo. Sasa sijui kunakuwa kuna utaratibu gani kwa Mhe. Waziri wa Afya, wakati hichi kitu kinajirejea leo kwa mara ya pili. Baada ya maelezo hayo naomba swali langu Nam. 126 lipatiwe majibu.

Nam. 126

Upatikanaji wa Leseni kwa Wanafunzi Waliomaliza Fani ya Uuguzi

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafanya juhudi mbali mbali za kuhakikisha kuwa inawaletea maendeleo endelevu wananchi wa kuendelea kuwasomesha wanafunzi wa fani mbali mbali wakiwemo wa fani ya uuguzi (*nursing*) ili hospitali zetu ziweze kutoa huduma zilizo bora zaidi.

a) Je, kuna utaratibu gani wa kuwapatia leseni wanafunzi wote waliomaliza fani ya uuguzi (*nursing*) kwa ajili ya ajira.

b) Je, wanafunzi hawa endapo watakoseshwa leseni hizo ambazo wanazitegemea kwa ajili ya ajira zao, serikali haioni kuwa inaingia hasara zaidi kwa vile wanafunzi ambao wanategemea leseni hizo ili waajiriwe itawawezesha kulipa madeni yao wanayodaiwa na Bodi ya Mikopo.

c) Ni utaratibu gani utaaandaliwa kwa wanafunzi ambao tayari walikuwa vyuoni na walimaliza Kidatu cha Nne (F.IV) na kwa kuwa hawakufika Kidato cha Sita (F.VI) na wanahitaji hizo leseni na bado wanasumbuliwa mpaka sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kwanza niombe radhi kwa tatizo dogo lililojitokeza ambalo linaweza likaleta sintafahamu katika Baraza.

Mheshimiwa jawabu swali ninalotarajia kulijibu ni swali namba 126 lakini jawabu ambalo limekwekwa kwenye karatasi hizi ambazo wamepewa wajumbe ni jawabu la swali namba 127 kwa hivyo naomba radhi kwa niaba ya watendaji wa Baraza kwa sababu hili ni kosa lao na sio la kwangu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba ruhusa yako ili niweze kujibu swali namba 126 lililoulizwa na Mhe. Hidaya Ali Makame Mwakilishi wa Viti Maalum lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kutoa ufafanuzi kuhusiana na utoaji wa leseni kwa Wauguzi na Wakunga Zanzibar. Kwa mujibu wa Sheria namba 5 ya mwaka 2014 ya Baraza la Wauguzi na Wakunga Zanzibar sura ya 4 kifungu nambari 15(1)(2) A, B na C na kifungu 3(a) na (b) imetoa ufafanuzi juu ya sifa ya uuguzi miongoni mwa sifa hizo ni kwamba:

a) Muuguzi anatakiwa ni mwenye sifa na tabia nzuri.

b) Awe amefaulu mafunzo ya Uuguzi na Ukunga kwa kiwango cha Stashahada yaani *Diploma* kwa muda usiopungua miaka mitatu au Shahada yaani *Bachelor* ya zaidi au zaidi katika Chuo kinachotambulika na Baraza la Waauguzi na Wakunga.

(a) na (b) Mhe. Spika, Baraza la Waauguzi wa Wakunga Zanzibar linaendelea kutoa leseni kwa Wauguzi na Wakunga wote wenye sifa za kupata leseni kwa mujibu wa sheria, utaratibu uliokuwepo ni kufika Afisi ya Baraza la Wauguzi na Wakunga Vuga na Afisi ya Wizara ya Afya iliyopo Wete na kupatiwa fomu maalum ya maombi na kutakiwa kuijaza.

Vile vile atawasilisha vivuli vya vyeti mbali mbali cheti cha kuzaliwa, cheti cha kumaliza fani ya uuguzi, cha matokeo uuguzi, kitambulisho cha Mzanzibari au cha Mtanzania, pasi ya kusafiria, picha mbili za *passport size*, cheti cha elimu ya sekondari, risiti ya malipo ya *bank* akikamilisha hayo sasa utaratibu wa kutengenezewa leseni ya usajili utaendelea bila ya pingamizi yoyote.

Mhe. Spika, si aghalabu kwa Muuguzi au Mkunga kuzuiliwa kupewa leseni au kupewa leseni na usajili ambaye anasifa zilizotimia, tunasisitza kwamba Wauguzi na Wakunga wafuate sheria na taratibu ziliopo ili kuilinda fani ya Uguzi na Ukunga kutoka kwa watu wasio waaminifu.

c) Mhe. Spika, vyuo vyote ambazo vinafundisha Uuguzi na Ukunga Zanzibar vimepewa maelekezo na Baraza la Wuuguzi na Wakunga juu ya sifa za kudahili wanafunzi hao kila mwaka wa masomo unapofika orodha ya wanafunzi husika

waliodahiliwa vyuoni huwasilishwa Barazani kwa Wauguzi na kuwaondoa wale ambao hawana sifa za kujiunga sifa zinazotakiwa ni awe amefaulu masomo ya sayansi angalau mawili, somo la *biology* ni lazima jengine ni kemia na fizikia au hesabati.

Mhe. Spika, Baraza la Wawauguzi na Wakunga hadi sasa halijapata malalamiko haya na hakuna Muuguzi au Mkunga anayesumbuliwa kwa kuwa hakufika kidato cha 6 jambo la msingi ni kwamba amefaulu masomo na pasi kama nilivyoeleza katika kifungu (a). Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika kwa kuniona tena kuuliza swali dogo la nyongeza kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanawapa moyo wale vijana ambao wapo na bado hawajapatiwa hizi ajira.

Mhe. Spika, kwanza nimuulize swali dogo Mhe. Waziri ni miaka mingapi kuanzia mwaka 2012 mpaka hivi sasa ni wanafunzi wangapi ambao walisoma nafasi hii ya uuguzi na mpaka sasa hivi tayari wameshapatiwa ajira.

Lakini jee ili uwe nasi ni lazima uwe umeshapatiwa ile leseni je ni utaratibu gani mnauchukua kuwaajiri hawa *nurse* ambao wamesoma nje ya nchi yetu. Kwa sababu kuna malalamiko mengi ambapo *nurse* hawa wanaporudi kwenye masomo yao kuna vikwazo ambavyo wamewekewa lazima wasome mpaka form VI na Chuo ndipo wapatiwe ajira wakati *nurse* hawa kabla ya hapo nafasi zilitoka mpaka yule wa form VI ambaye alipasi yale masomo ambayo yanahusika aende akasome hiyo nafasi ya *nurse.* Je, kuna utaratibu gani ambao utachukuliwa kwa hawa ambao tayari ilikuwa hili tangazo halijatoka wao tayari washarudi katika kwenye masomo au wanaendelea na haya masomo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mheshimiwa jibu swali (b) kwasababu swali A linahitaji takwimu na sidhani kama utakuwa na majibu hapo moja kwa moja jibu swali (b).

Mhe Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakushukuru naomba kumjibu Mhe. Hidaya swali lake (b) kama ulivyoniamuru.

Mhe. Spika, utaratibu uliopo mpaka sasa hivi uliopo ni ule ule ambao unafuatwa wa kumaliza kidato cha nne na awe na Diploma au kidato cha sita awe na Digrii, mpaka sasa hivi hakuna utaratibu ambao umeandaliwa lakini wazo lako tutalichukua tutalikalia kitako, tutalijadili na baadae tutapata jambo la maana kwa kweli ulilolishauri hapa mimi ninalichukua kama ni ushauri ni jambo zuri kwa sababu kule wakisoma huwa wameshapoteza pesa lakini pia huwa wameshapoteza muda mrefu na kwa kweli tunawahitaji katika Serikali yetu wanyakazi kazi ya kuwahudumia wananchi. Mheshimiwa hili tunalichukuwa na tutalifanyia utaratibu ili na wao waweze kupata haki yao kama kawaida.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo sana la nyongeza.

Kwasababu tuu Wizara ya Afya ina utaratibu wa kuwaajiri *nursing* watu wa *pharmacy* pamoja na Ma *Health Officers* wanapomaliza chuo, lakini kwa muda mrefu sasa Ma-*Health Officer* wengi wamezagaa mitaani na hawana la kufanya je ina utaratibu gani wa kuaajiri vijana wale kwa sasa.

Mhe. Sira Ubwa Mamboya: (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ya mwanzo ambayo ni kamilifu na kweli tatizo limejitokeza kwa hili liloandikwa humu kwa hiyo nashukuru kwamba wametuelewa na kwamba tumeweza kusahihisha haya ni matatizo yamejitokeza huko yalikochapwa.

Lakini swali alilojibu nataka kuongeza katika swali alilolijibu kuhusu wanafunzi ambao wanaosoma nje ya hapa ya vyuo vya nje halafu wanarudia hapa lakini hawaajiriwi. Ili uweze kuajiriwa lazima uwe na sifa. Chuo chetu hapa imeweka sifa ambazo mwanafunzi lazima awe nazo. Bara kuna vyuo nyingi na nje ya nchi kuna vyo vingi ambapo wanaweza wakachukua wanafunzi kulingana na sifa ambazo wanazifahamu wao hata kama wakisoma, hata kama watarudi na cheti lakini kama cheti cha msingi hakikuwa na sifa zile ambazo hapa tumeziweka wanafunzi wale wanakuwa hawawezi kuajirika hapa kwa sababu hawana sifa zinazostahiki.

Kwa hivyo Bara kuna vyuo na ambavyo sasa hivi vingi tu vimepigwa marufuku ambapo wanafunzi wetu wamekwenda kusoma labda baada ya kukosa nafasi hapa, lakini sasa ukija tizama vyeti vyao vya Form IV hukuti kwamba alipasi *Biology*, unakuta labda ana kiswahili, labda ana D baada ya kuwa na B na C labla anakuwa na F katika yale masomo ya msingi kwa hivyo huyo hawezi akaajirika anakuwa kama wamepoteza pesa zao bure. Kwa sababu hata hao wanaotoka Bara wakija na vyeti vina zile *qualification* ndizo zinazotakiwa hawa wanaajiriwa kunakuwa hakuna tatizo kwa hiyo hilo ndilo ningependa kuongezea kwa hili.

Lakini na hili la pili kwamba kuna wanafunzi wengi waliomaliza vyuo mengi ambao hawajaajiriwa ni kweli hilo wengi wapo kama miaka mitatu baadhi yao wapo wajaariwa. Lakini sasa hilo sio kosa la wizara kwa sababu wizara inajua mahitaji yake, lakini sasa wanaajiri watu kulingana na Tume ya Uajiri inavyowapa watu wao watapeleka mahitaji yao lakini sasa Tume inatowa kwa idadi ya ile itakachoweza kuajiri na kuwalipa sio kwamba hakuna nafasi zile lakini sasa inategemea na nafasi watakazopata, lakini kama Tume itawaajiri tutachukukuru kwa sababu nafasi zipo, shida ipo isipokuwa ajira tu inakuwa tatizo na hilo si la Wizara ya Afya ni la Tume ya Uajiri.

Mhe. Spika: Ahsante Wizara inayofuata waheshimiwa wakati wa maswali umekwisha lakini kuna Wizara moja imebaki na kwa kuwa waliomba kuchangia hii hoja ainayofuata ni wachache sana naomba tumalize haya maswali mawili halafu tutaendelea.

Nam. 4

Uegeshaji wa Meli Katika Eneo la Maruhubi

Mhe. Abdalla Maulid Diwani – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi, kwa kutoa fursa za uwekezaji kwa wageni na wenyeji kuwekeza katika sekta ya usafiri wa bahari.

(a) Je, Serikali haioni inakosa mapato yake ya kodi za uegeshaji wa meli kwa kumruhusu *Azam Marine* kuweka meli zake katika eneo la maruhubi.

(b) Je, ni lini Serikali italishughulikia suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Jang'ombe swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika kwanza napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mwakilishi kuwa vyombo vyote vya Kampuni ya *Azam Marine* vinavyofanya kazi ya kusafirisha abiria na mizigo vinaegesha katika Bandari ya Malindi kama vyombo vyengine na vinalipa kodi zote za Bandari kwa mujibu wa sheria ya Bandari.

Vyombo viwili vya kazi vya AZAM (*Dredger* pamoja na Tishali) ambayo vinafanya kazi ya uchimbaji na ubebaji wa mchanga ndivyo vinavyoegeshwa Maruhubi katika eneo la kazi kama tulivyokubalina.

Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari linasimamia suala hili na kuhakikisha kuwa hakuna chombo kinachoegeshwa nje ya eneo la Bandari kwa mujibu wa sheria yetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu ya kusikitisha ya Mhe. Waziri ambaye nilitegemea kwamba angenijibu ni kweli huko nyuma vyombo vilikuwa vinakaa lakini sasa hivi havikai je naomba anieleze humu kuanzia mwezi wa nne mpaka wa tatu vyombo vinavyorudi Dar es Salaam vya AZAM vilikuwa vinalala wapi.

a) Chombo hakiwezi kuondoka Bandarini bila ya kuwasiliana na *signal station* na pale mara pana buku linajazwa jee Waziri atakuwa tayari kujiuzulu pindi tukitoka mimi na yeye tukienda *signal station* kuangalia maelezo ndani ya buku kwamba kweli vyombo vile vilikuwa vinalala kule mtoni.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliana na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Abdalla Maulidi Diwani kwa utaratibu ufuatao.

Kiutaratibu swali likija katika Baraza la Wawakilishi tunavyolijibu maana yake tayari lishafanyiwa kazi swali hili liliulizwa ndani ya Baraza la Wawakilishi na nikakiri kwamba kweli kulikuwa hicho chomba kipo na tulachukulia hatua, sasa mimi namshangaa sana akisema kwamba bado sijajibu swali hilo nilikiri hapoa ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa hivyo namuomba sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani yake majibu nilojibu arejee atakuta kwamba nimejibu hivyo na hilo jengine namuomba sana lisifike kama ulivyosema wewe Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuwa Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 sehemu ya kwanza inasema kwamba Zanzibar ni nchi ambayo ni eneo la mipaka yake na ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vilivyo izunguka na bahari yake ambayo kabla ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kumekuwa kuna meli nyingi zimekuwa ambazo zinaegesha hasa kwa upande wa Mashariki na upande wa Magharibi kama utaelekea kutoka Bumbwini pamoja na Mangapwani utazikuta meli kubwa sana zimeegesha. Swali langu liko hivi je, hizi meli tayari ziko ndani ya bahari Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini utambulisho wake je Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata fedha kiasi gani na katika kodi je Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga katika kukusanya kiasi gani katika miaka ya mbele jinsi ya hizi meli zinapongezeka kuegesha ndani ya bahari ambayo ipo kwa upande wa Zanzibar. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika kwa ruhusa yako napenda kujibu Mhe. Simai Mohammed Said kwamba utaratibu meli ambazo zinaegesha nje ya maeneo ya bahari yetu zile zinakuwa ziko katika mipaka ya kimataifa.

Meli zote ambazo zinataka kuingia ndani zinakuwa zinaingizwa ndani kwa *pilot* mwenyewe wanasema chombo maalum cha kuingiza meli na zinapoingia ndani sasa pale ndio tunakuwa tunapata kodi maalumu na hii inakusanywa kupitia Shirika la Meli, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante swali linalofuata linaulizwa na Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Konde.

Nam. 107

Ukamataji wa Vespa na Pikipiki Zilizotoboa "*Exos*"

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Je, Wizara au Idara inayosimamia upasishaji na utoaji leseni za vyombo vya moto kwa 2016 imezikamata vespa na pikikipi ngapi ambazo zimetoboa "*exos*" kwa makusudi ambazo hutumiwa na waendesha vespa wanaojulikana kwa jina la *"T1"* ambao si tu huleta usumbufu bali pia huwa ni chanzo cha kusababisha ajali kwa watu wengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Konde swali lake nambari 107 kama ifuatavyo:-

Idara inayosimamia upasishaji na utoaji leseni za vyombo vya moto kwa mwaka 2016 haikukamata vespa na pikipiki hata moja kwa vile katika vyombo ilivyovikagua hakikuonekana chombo hata kimoja kilichotobolewa bomba la kutolea moshi kwa maana hiyo kasoro hizo hufanywa baada ya chombo kupasi na kupewa leseni ya njia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mheshimiwa nashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri.

Mheshimiwa kwa sababu kwenye jibu lako hili inaonekana hawa wanafanya udanganyifu wanapokwenda pale wanaviziba hivi vyomba ma-*exos* yao ikisha wakirudi wanaendelea kuyatoboa, lakini kwanza nataka kujua ina maana hawa *T ONE* wanazozitoboa hizi pikipiki na vespa zao hapa mjini hawapo tena, kama wapo hii wizara inayoshughulika na idara inayoshughulika ina mpango gani wa kuzikamata wakaziitaifisha hasa ili kuondoa hii kadhia iliyokuwa inatugubudhi kwa watu hawa Mhe. Waziri lini mutaanza utaratibu huu, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Omar Seif bin Abeid swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kama nilivyosema hawa vijana ni kweli wanafanya hiyo kazi wa kutoba lile *exos* lakini wanafanya kazi kwa kushirikiana na watu wenye *garage* na baadhi ya wakati hao *T ONE* wenyewe ni wale vijana ambao wanafanya hizi mbio na mambo mengine.

   Sasa kwa mujibu wa sheria yetu namba 7 ya 2003 kifungu 21mpaka 24 vinaelezea utaratibu kwmba si ruhusa kifungu 21 mwenye mmiliki wa chombo chochote kile kubadilisha boti au chombo chochote kila kikaleta madhara au sauti yoyote katika kwa mujibu wa sheria hii.

b) Lakini vile vile kifungu namba 22 kinaelezea vile vile sio mwenye *garage* yoyote anayeruhusiwa au mwenye kutengeneza mabodi yote kufanya hiyo kazi na iwapo sasa kitapatikana kimefanyiwa *modification* ya aina yoyote basi tunatoa adhabu kubwa sana ni *fine* isiopungua $120 kwa sasa na pesa TZS au vile vile kifungo kisichopungua miezi sita.

Sasa sisi tunatowa wito na tunaendelea kutoa wito Jeshi la Polisi linafanaya kazi nzuri sana kuhakikisha kwamba kwanza *T ONE* sasa hivi wamepungua sana Mkoa wa Mjini Magharibi nimshukuru sana kamanda Mkadam anayeshughulika na usalama barabarani amekuwa anaifanya kazi nzuri sana kupitia Masheha juzi kawafanyia semina tumewaambia kwamba wale wazazi ambao wataruhusu watoto wao wafanye mashindano au watumie hizi vespa katika kuziharibu basi tunaenda kuwachukua kulekule au tunawachukua sehemu yoyote tunayowakuta na kuwapa adhamu kwa mujibu wa sheria yetu.

Lakini sheria yetu vile vile inasema kwamba Mkaguzi au Afisi wa Polisi yoyote anao uwezo sasa wa kusimamisha chombo chochote na kuipeleka polisi au sehemu nyengine yoyote kwa kwenda kuifanyia ukaguzi na ikibainika kwamba chombo kila kina matatizo basi mtengenezaji wa kila chombo au yule mwenye chombo anapigwa faini isiopungua $50. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa muda wa maswali umekwisha. Waheshimiwa tangazo la wageni, naomba kuwatambua wageni wetu wa leo, wageni waliopo ni kutoka matawi ya CCM Dunga Kiembeni na Dunga Kinyongo ni wageni wa Mhe. Simai Mohammed Said na jumla yao ni kumi. Mgeni wa kwanza ni Juma Mchenga Haji, Mwenyekiti Dunga Kiembeni naomba asimame ili aonekane; wa pili ni Bwana Mussa Makame Yussuf, katibu na yupo Bwana Mussa Peter Michael, huyu ni Katibu Mwenezi wa Tawi; yupo Bi Riziki Khamis Yussuf, Katibu wa Wazazi; Bi Mwanahamis S. Ali, Katibu UWT; wengine ni Bwana Mbaraka Soud Hassan, Mwenyekiti Dunga Kinyongo; Bwana Amour Hassan Ubwa, Katibu wa Tawi; Bi Ziada Ubwa Haji, Mwenyekiti UWT; Bi Atka Mohammed Haji, Mjumbe wa Kamati ya Siasa na Mwantajo Silima, Katibu Mwenezi. Ahsanteni sana karibuni. *(Makofi)*

Wageni wanaofuata wengine ni wageni wawili wa Mhe. Miraji Khamis Mussa, Bi Sihelime kutoka South Korea, *welcome.* Huyu ni mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Chung-Ang na wa pili ni Ndugu Machano Ali Machano ni diwani wa kuteuliwa Manispaa ya Mjini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa napenda kuwatangazia pia kwamba wale Wajumbe wa Kamati ya Uongozi mara baada ya kuakhirishwa kikao leo mchana kutakuwa na kikao cha dharura cha Kamati ya Uongozi. Baada ya hapo naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma ili naye aje aongoze kikao karibu.

(Hapa Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Ripoti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pili

kukukaribisha wewe nyumbani karibu sana Zanzibar tunaendelea vizuri na kazi zetu kama tulivyopanga. Pole kwa uchovu wa safari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba nichukue nafasi hii kwa kuweza kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutukutanisha hapa tukiwa wenye afya njema. Kwa mara nyengine naipongeza Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Omar Seif Abeid kwa miongozo, maelekezo na ushirikiano wanayonipa katika kutekeleza majukumu yangu na majukumu ya ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii adhimu kwa namna ya kipekee kumshukuru kwa dhati Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake kwangu na kunipa dhamana hii. Namuahidi kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uwezo wangu wote katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020 kwa kushirikiana na Watendaji na Viongozi wenzangu kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani zangu ziende pia kwa viongozi na watendaji wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano wanaonipa. Aidha, nawapongeza kwa utendaji wao mzuri wa ufanisi katika kutekeleza majukumu yao. Nawasihi waendelee na moyo wa kujituma katika kuwahudumia wananchi kwani huo ni wajibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mkutano wa Tano wa Baraza la Wawakilishi, Kamati za Kudumu ziliwasilisha katika Baraza la Wawakilishi taarifa za shughuli zao kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 108(15) ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016. Katika ripoti hizo, kamati zilitoa ushauri na maagizo mbali mbali ambayo yalitakiwa yatekelezwe na wizara husika. Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2016/2017 ilifanya kazi zake katika mizunguko mitatu kwa muda wa wiki sita. Katika muda huo, kamati ilipata fursa ya kuyatembelea maeneo mbali mbali katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kupokea taarifa za utekelezaji pamoja na kukagua baadhi ya maeneo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba huo, naomba kuwasilisha katika Baraza lako Tukufu ripoti ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama ifuatavyo:

UTEKELEZAJI WA MAAGIZO

Mhe. Mwenyekiti, kwa jumla, ushauri na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa yamegawika katika sehemu kuu sita zifuatayo:-

i. Kuimarisha hali ya mazingira na mandhari ya Nyumba zote za Ikulu;
ii. Kudhibiti mmong'onyoko na matengenezo ya Nyumba za Ikulu;
iii. Kuimarisha mawasiliano Ikulu;
iv. Kuimarisha shughuli za Ofisi ya Usalama wa Serikali;
v. Kuimarisha Maktaba ya Ofisi ya Baraza la Mapinduzi; na
vi. Kuimarisha shughuli za Diaspora Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika Ofisi ya Faragha ya Rais Kamati ilitoa maagizo manne yafuatayo:-

Agizo la 1: Kamati imeshauri kuimarishwa mazingira ya Ikulu ndogo ya Migombani ili kuweka haiba ya kuzidi kupendeza kwa eneo hilo.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeweka mfumo wa kuhifadhi taka kwa kuweka makontena mawili, imeimarisha maeneo ya bustani na imewasiliana na Baraza la Manispaa la Mji wa Zanzibar kwa ajili ya kuimarisha bustani iliyopo mbele ya jengo la Ikulu ya Migombani.

Agizo la 2: Kamati imeshauri, kupimwa maeneo yote ya nyumba za mapumziko za Mheshimiwa Rais, kwa ajili ya kuwekewa uzio na kupatikana kwa nyaraka za umiliki wa eneo husika kwa nyumba hizo za Serikali.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilikwishayapima maeneo yote ya nyumba za Ikulu na imekabidhiwa hati tangu mwaka 2013. Kazi ya kujenga uzio wa *wire* wa muda katika Ikulu ya Bwefum imekamilika. Aidha, hatua za kupata fedha kwa ajili ya kazi ya kujenga uzio katika Ikulu ndogo ya Micheweni na Mkokotoni zitachukuliwa kwa haraka kwa vile zimeshatengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Agizo la 3: Kuhusiana na suala la mmong'onyoko wa ardhi, Kamati imeshauri kuongeza kasi ya ushughulikiaji wa tatizo hilo, ukizingatia kila siku tatizo linazidi kuongezeka hasa katika Ikulu ya Mkoani ambayo tayari hatua za ujenzi na ukarabati zinaendelea. Sambamba na ukarabati huo, Kamati inasisitiza hatua za upandaji miti ni muhimu kuzingatiwa katika maeneo yalioathirika na mmong'onyoko wa ardhi.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imetathmini athari ya mmong'onyoko katika maeneo yote ya Ikulu. Katika Ikulu ya Mkoani kazi ya kuzuia mmong'onyoko wa ardhi kwa kutumia ujenzi maalum wa kujenga vikuta vya mawe (*stone patching)* imefanyika kwa hatua ya kwanza. Aidha, awamu ya pili ya ukamilishaji wa ujenzi huo utakamilika katika robo hii. Malipo kwa ajili ya kazi hii tayari yameshafanyika kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kwa upande wa Ikulu ya Migombani, ofisi imejenga misingi ya kupitishia maji ya mvua ili kuzuia mmong'onyoko wa ardhi. Aidha, katika Ikulu ndogo ya Bwefum na Kibweni, Wataalamu wa Shirika la Bandari wameshauri kujenga ukuta au kuweka mawe makubwa ili kudhibiti mawimbi ya bahari yasiendelee kuathiri eneo husika. Ofisi imepokea ushauri wa wataalamu na inafikiria kuwa na mradi wa kudhibiti uharibifu wa mazingira, unaofanana na mradi uliopo Kilimani katika bahari ya Kizingo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Agizo la 4: Kamati imeagiza kufanyiwa ukarabati mkubwa katika nyumba ya Rais ya Laibon – Dar es Salaam, ili kuendana na hadhi ya Mhe. Rais.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, matengenezo ya Ikulu ndogo ya Laibon yamefanyika ikiwa ni pamoja na kuongeza nyumba za wafanyakazi, uwekaji wa vipoza hewa vipya, kuziba uzio kwa *plastic screen*. Aidha, hatua za kupaka rangi zinakamilika katika mwezi Oktoba, 2017.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Mawasiliano na Habari - Ikulu Kamati ilitoa maagizo matano yafuatayo:-

Agizo la 1: Kamati imeshauri Idara kuchukua hatua za makusudi kutoa taarifa kwa umma kwa haraka kuhusiana na upotoshwaji wa ukweli kuhusiana na mambo yanayomgusa Mheshimiwa Rais moja kwa moja, kupitia vyombo vya habari kama TV na Radio, kwani kufanya hivyo kutalinda na kuonesha uwezo, hadhi na heshima aliyonayo kiongozi huyu mkuu wa nchi.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeshachukua hatua mbali mbali ili kuhakikisha kuwa taarifa sahihi zinawafikia wananchi kwa wakati. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea kuchapisha nakala 3,000 za jarida la Ikulu ambazo zinasambazwa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba, Taasisi za Serikali, Baraza la Wawakilishi na kwenye Vituo vyote vya Walimu. Kadhalika, ofisi imeendelea kutoa vipindi vya redio na televisheni kila wiki mara moja, kurusha taarifa katika mitandao ya kijamii kwa kuonesha moja kwa moja matukio muhimu (*livestream*) katika "*facebook*" ya Ikulu. Miongoni mwa matukio yaliyorushwa moja kwa moja ni mkutano wa Mhe. Rais na Wazee Gombani Pemba mwezi Oktoba, 2016, Mkutano wa Mhe. Rais na Viongozi na Waaandishi wa Habari mwezi Aprili, 2017, sherehe ya kutunuku nishani kwa Wananchi, Viongozi, Wafanyakazi na Wapiganaji wa SMZ mwezi Julai, 2017 na kilele cha Sherehe za Elimu bila ya Malipo Gombani Pemba tarehe 23 Septemba, 2017.

Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu imeweka utaratibu wa kuwapeleka maofisa wake katika vijiji mbali mbali Unguja na Pemba kwa ajili ya kupata maoni ya wananchi kuhusiana na mambo mbali mbali ya kijamii na kimaendeleo. Katika mwezi wa Septemba, 2017, maofisa hao walitembelea Vijiji vya Ngomeni, Chokocho, Mkanyageni, Kisiwapanza na Fundo. Vijiji vyengine ni Mgonjoni, Fumba, Tumbatu, Jendele na Cheju.

Vile vile, ofisi imefanya mikutano na Wakuu wa Vyombo vya Habari vya Serikali mwezi Machi, 2017 katika ukumbi wa mikutano Ikulu. Kadhalika, mwezi Septemba, 2017 Ofisi

ilifanya mkutano na Maofisa wa Habari wa Taasisi za Serikali katika ukumbi wa Idara ya Habari Maelezo katika ukumbi mdogo wa Baraza la Wawakilishi la zamani Kikwajuni pamoja na kukutana na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Zanzibar mwezi Septemba, 2017.

Katika hatua nyengine, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliandaa Semina ya Viongozi wa Serikali na Waandishi wa Habari iliofanyika tarehe 1 Aprili, 2017 katika Ukumbi wa zamani wa Baraza la Wawakilishi. Kupitia semina hiyo, alitoa wito kwa washiriki wa semina hiyo kuchukua juhudi maalum kuhakikisha kuwa taarifa zote muhimu juu ya utendaji wa serikali zinawafikia wananchi tena kwa wakati.

Agizo la 2: Kamati ilishauri idara kuandaa jukwaa maalum, ambalo litamkutanisha Mhe. Rais na wadau wengine wakiwemo wanaotoka katika Sekta za Habari na Biashara kwa lengo la kuboresha taswira ya Mhe. Rais na kumsogeza karibu zaidi na wananchi wake.

Utekelezaji:

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais amekuwa na utaratibu wa kukutana na wahariri na waandishi wa habari mara kwa mara. Mikutano ya hivi karibuni ni mkutano wa tarehe 23 Machi, 2017 ambapo Mhe. Rais alikutana Ikulu na waandishi wa habari kutoka vyombo mbali mbali vya habari vya Zanzibar na Tanzania Bara. Aidha, tarehe 1 Aprili, 2017 alikutana na Viongozi wa Serikali pamoja na waandishi wa habari katika Ukumbi wa zamani wa Baraza la Wawakilishi.

Katika hatua nyengine, Mhe. Rais amekuwa akikutana ana kwa ana na kuzungumza na wananchi kila anapofanya ziara katika maeneo mbali mbali. Katika ziara zake alizozifanya hivi karibuni katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba kuanzia tarehe 12 hadi 26 Agosti, 2017. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein aliwataka Waheshimiwa Mawaziri na viongozi wengine aliofuatana nao kutoa ufafanuzi kuhusiana na masuala mbali mbali ya wizara ama taasisi zao ambayo yameulizwa na wananchi wakati wa ziara hizo.

Aidha, Mhe. Rais ni Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la Taifa ambalo ni jukwaa rasmi la kukutanisha serikali na wafanyabiashara. Kwa kutumia Baraza hilo, Mhe. Rais anapata fursa ya kutosha ya kujadili na kubadilishana mawazo na sekta binafsi. Baraza la Biashara la Taifa linatarajiwa kufanya kikao chake kabla ya mwisho wa mwaka huu 2017.

Agizo la 3: Kamati imeshauri idara kuanzisha mahusiano ya karibu zaidi (*networking*) na vyombo mbali mbali vya habari na wizara nyengine, kwa lengo la kuhakisha na kuleta ufanisi wa mchakato mzima wa kuiarifu jamii juu ya shughuli za maendeleo anazozifanya Mhe. Rais.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tayari imeanzisha mahusiano ya karibu zaidi "*Networking*" na vyombo vyengine vya habari na wizara nyengine kwa lengo la kuhakikisha kuwa inaleta ufanisi zaidi kwa kupeleka taarifa kwa wananchi. Kupitia utaratibu huo, Idara ya Mawasiliano na Habari

Ikulu imekuwa ikiwaalika waandishi wa habari kutoka vyombo tofauti vya habari vya ndani vikiwemo *ZBC, TBC1, ITV, Star TV,* Zanzibar leo, Nipashe, *Daily News, Bomba FM, Bahari FM, Zenj FM* kutembelea miradi ya maendeleo pamoja na kuzungumza na wananchi ili kupata maoni yao kuhusiana na mwenendo wa serikali. Miradi iliyotembelewa na waandishi wa habari ni pamoja na barabara za Mzambarautakao – Madenjani; Pandani inayotokea Mzambarau Karimu kupitia Finya; Wete - Konde, Bahanasa kwenda Mtambwe. Skuli zilizotembelewa ni Dole Unguja na Utaani Pemba. Katika maeneo ya utalii ni Kiwengwa, Jozani na Kizimbani.

Agizo la 4: Kamati imeagiza, kutokana na mabadiliko ya teknolojia, idara ielekeze nguvu zake zaidi katika kutumia njia mpya za upokeaji na utumaji wa habari (*New Media*) kama mitandao ya kijamii, ikiwa ni pamoja na "*facebook*", na "*Twitter*" ambazo zina watumiaji wengi hususan vijana, mawanda mapana na haihitaji gharama kubwa.

Utekelezaji: Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia kitengo cha TEHAMA imeendelea kutoa taarifa kwa wananchi kupitia mitandao ya kijamii kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Hivi sasa, taarifa zinatolewa moja kwa moja kwa wananchi kutoka kwenye tukio (*live Stream*) ya "*Facebook*", "*tweeter*" na "*youtube*" na kupata mrejesho. Kwa hivi sasa ukurasa wetu wa "facebook" unatembelewa na wastani wa watu 8,000 kutegemea na tukio. Kadhalika, karibuni Mheshimiwa Rais atafungua ukurasa wake wa *personal* wa "*tweeter*".

Agizo la 5: Mhe. Mwenyekiti, kamati pia imeshauri juu ya kuboresha tovuti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ili kuifanya iwe ni yenye kutembelewa na watumiaji wengi na yenye kwenda na wakati zaidi.

Utekelezaji: Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeimarisha tovuti ya Ikulu pamoja na kuweka baadhi ya maeneo mapya ili kuzidisha mvuto kwa watembeleaji. Maeneo yaliyoongezwa ni pamoja na kuwekwa "*link*" mbali mbali na kuwa na *BLOG*. Katika kuongeza mvuto, maeneo yafuatayo yamefanyiwa mabadiliko:-

i. Idadi ya picha zinazoonekana kwenye *"home page"* zimeongezeka kutoka nne za sasa hadi kufikia zaidi ya picha sita;
ii. Katika "galary" picha zinaonekana na maelezo (*captions*), lakini pia picha zinaonekana katika mtindo wa albamu kama ilivyokuwa hapo nyuma;
iii. Tovuti mpya imeimarishwa kwa kuwa na uwezo wa lugha mbili, ambapo mtumiaji anaweza kubadilisha lugha anayoitaka kati ya KISWAHILI na KIINGEREZA;
iv. Vile vile kuna *link* ya *blog*, ina *subdomain* yake kwa maana ni *independent* kutoka kwenye *website* ili mtu aweze kuitembelea kuweka link tu ya *blog* ambayo mtu atakapoibonyeza itampeleka moja kwa moja kwenye *blog*; na
v. Tovuti mpya imewekewa teknolojia ambayo inamuwezesha kufunguka katika simu ya mkononi bila ya kupoteza ubora wa muonekano wake pamoja na kuweza kupeana taarifa ku-*share* na mtandao wa kijamii wa *facebook*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, kamati ilitoa agizo moja tu.

Agizo: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya haraka ya kiulimwengu katika masuala ya kiteknolojia, kamati imeshauri zoezi la kuanzisha maktaba katika Ofisi za Baraza la Mapinduzi liende sambamba na kuanzishwa kwa maktaba ya kielektroniki "*e-library*", ili kuwawezesha Waheshimiwa kutumia huduma hizo katika muda na mahala popote.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa uwepo wa Maktaba ya Ofisi ya Baraza la Mapinduzi itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi wa kazi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, Makatibu Wakuu, Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi na wote wanaoitumia. Matarajio ya Ofisi ni kuona kuwa Maktaba hii inajitosheleza kwa huduma na vifaa mara tu itakapoanza kutumika. Ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa Maktaba hii, Ofisi itaandaa utaratibu wa kuhakikisha kuwa huduma za Maktaba zinawafikia walengwa kwa wepesi kadri iwezekanavyo ikiwemo uwezekano wa kuifanya Maktaba kuwa ya Kielektroniki kulingana na miongozo ya Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi (*Diaspora*), Kamati ilitoa agizo moja lifuatalo:-

Agizo la 1. Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeagiza kuanza kufanyiwa kazi zaidi na kutekelezwa kwa maazimio yatokanayo na makongamano yanayoendelea kufanyika kila baada ya muda kuhusiana na Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi - Diaspora.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimewaandikia Taasisi na Sekta husika kuhusu utekelezaji wa maazimio hayo. Maazimio ambayo yanatekelezwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni kama yafuatayo:-

Kukamilisha Sera ya *Diaspora* itakayowatambua na kuwawezesha *Diaspora* kuchangia/kushiriki katika maendeleo ya Nchi yetu.

Kuandaa Kongamano la nne la *Diaspora* lifanyike Zanzibar mwezi wa Agosti, 2017. Kupitia Kongamano la Nne la *Diaspora*, Wanadiaspora wamehamasishwa kuwa wazalendo kwa Nchi yao ya asili na kutumia fursa zilizopo ili kuja kuwekeza nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba, Kamati ilitoa maagizo mawili yafuatayo:-

Agizo la 1: Kamati imeshauri kufanyike kwa taratibu wa kuyapiga mnada magari chakavu ya serikali katika ofisi hii kwa kufuata utaratibu wa uuzaji wa mali za umma.

Utekelezaji: Kwa sasa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba haina magari yaliyolala ambayo hayafanyi kazi.

Agizo la 2: Kamati imeshauri kutengwa eneo kwa ajili ya ujenzi wa maegesho maalum ya kuhifadhiwa magari ya Viongozi katika Ofisi hizo.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, Kwa kujua umuhimu wa kuwa na eneo maalum la maegesho ya magari ya Viongozi, Ofisi tayari imetenga eneo maalum lililopo karibu na jengo jipya la ukumbi wa mikutano kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya magari ya viongozi. Hata hivyo, ofisi inatarajia kuitekeleza shughuli hii kwenye bajeti ya 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Usalama wa Serikali (*GSO*), Kamati ilitoa maagizo manne yafuatayo:-

Agizo la 1: Kamati imeagiza kulifanyia ukarabati mdogo jengo linalotumika kwa sasa ili liweze kuwa na hali nzuri.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa mwaka wa fedha 2017/18 imepanga kulifanyia matengenezo madogo Jengo la Ofisi ya Usalama wa Serikali kupitia Mradi wa Maendeleo. Kazi zinazotarajiwa kufanyika kwa mwaka huu ni kuezeka upya, kuweka dari, ukarabati wa ndani na matengenezo ya vyoo. Kazi hii inatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2017.

Agizo la Pili: Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeshauri Wizara kuipatia Idara nyenzo za msingi za utendaji kazi ikiwa ni pamoja na samani za ofisi kama vile meza, viti, kompyuta n.k.

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imenunua gari moja kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za Ofisi ya Usalama wa Serikali. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha (2017/18) itapatiwa samani na zana za kufanyia kazi kwa mujibu wa mahitaji yake.

Agizo la 3: Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeshauri kufanyiwa marekebisho Sheria inayohusiana na uwepo wa Idara ya Usalama wa Serikali Zanzibar, ambayo kimsingi ni moja ya sababu ya kuwepo kwa changamoto nyenginezo.

Utekelezaji: Sheria ya Ofisi ya Usalama wa Serikali namba 5 ya mwaka 1983 ni ya muda mrefu inahitaji kufanyiwa marekebisho ili iendane na mahitaji halisi ya serikali kwa sasa. Hata hivyo, kutokana na muundo uliopo wa Ofisi ya Usalama wa Serikali, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itashauriana na Mamlaka nyengine za Kisheria ili kupata namna bora ya kulifanyia kazi jambo hili.

i. **Agizo la 4:** Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeagiza kuongezewa bajeti Idara hii katika bajeti ya mwaka 2017/2018 kwani ni muhimu sana kwa Serikali na watumishi wake kwa ujumla.

Utekelezaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Usalama wa Serikali imeongezewa bajeti kutoka TZS. 40 milioni hadi TZS. 75 milioni. Hata hivyo, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itaangalia uwezekano wa kuongeza bajeti ya Ofisi ya Usalama wa Serikali kwa mwaka wa fedha ujao (2018/2019) ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

HITIMISHO:

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamaliza uwasilishaji wa taarifa hii, nachukua fursa hii kukushukuru kwa namna unavyokiongoza chombo hiki. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa namna walivyokuwa watulivu katika kusikiliza taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wajumbe wataipokea na watatoa michango mizuri ili kuisaidia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, natoa shukurani maalum kwa wananchi wa Jimbo langu la Chwaka kwa kunivumilia wakati nikiwa katika majukumu mengine ya Serikali. Nawaahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia na kutekeleza ahadi nilizozitoa zote namuomba Mwenyezi Mungu anipe nguvu za kufanikisha azma hiyo.

Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza wana CCM wezangu wote nchini kwa kuendeleza demokrasia kwa chaguzi zinazoendelea katika ngazi mbali mbali kutoka ngazi ya shina hadi ngazi ya wilaya tunakwenda kutekeleza hivi karibuni. Hiki ni kielelezo cha kukomaa kwa demokrasia ndani ya Chama chetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja. (Makofi)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uwasilishaji wa ripoti yako. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi wakuu wa serikali.

Mhe. Ame Haji Ali: (kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa) : Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyezi wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu sasa naomba idhini yako ili nitoe hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu utekelezaji wa maagizo ya kamati ya mwaka 2016/17 ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa sina budi kupeleka shukrani zangu kwa mwenyezi mungu mwingi wa rehema, muumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia, uhai na afya njema na kuweza kukutana katika Baraza hili tukufu kwa lengo la kutimiza wajibu wetu uliotuweka baraza hili tukufu kwa lengo la kutimikia wananchi wetu waliotuleta humu wa Zanzibar .

Pia naomba kutumia fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe Spika pamoja na watendaji wote wa Baraza hili kwa kutuongoza vyema kwa ustadi, uwelidi na umakini wa hali ya juu na kutuwezesha sisi Wajumbe kufikia malengo tuliyojiwekea katika Baraza hili. Ni

matumaini yangu kuwa kwa uwezo wake *Allah* utaendelea kuliongoza Baraza letu hili. Wewe kwa ustadi wako pamoja na wasadizi wako wengine wote.

Mhe. Mwenyekiti, sitaacha kutumia fursa hii adhimu kumshukuru na kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu Rais wetu mpendwa Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa ustadi, umahiri, uweledi na busara kubwa ya aina yake anayotumia katika kuiongoza nchi yetu hii. Ukweli usiofikichika kwamba amekua mahiri na mbele katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ili wapate maisha bora. Hivyo, ni wajibu wetu sote kumuombea kiongozi wetu huyu kwa, Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na maisha marefu, busara, hekima na afya njema ili aweze kutuongoza kwa umakini zaidi na tuweze kuendelea kuishimaisha ya amani na utulivu wa hali ya juu zaidi katika nchi yetu.

Aidha sina budi kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Issa Haji Ussi kwa umahiri wake katika kuiongoza Ofisi hii ambayo ni muhimu kwani ndiyo Ofisi ya kiongozi mkuu wa nchi yetu. Vile vile nawapongeza watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Salum Maulid Salum na watendaji wenzake kwani utendaji wao wa kazi ndio chachu ya mafanikio katika Ofisi hii. Niwaombe wazidi kuzidisha bidii katika utendaji ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kusudiwa.

Lakini pia kwa namna ya upekee, nawashukuru Wajumbe na makatibu wa kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi zao nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za Kamati, jambo ambalo limeipa wepesi wa kuiongoza Kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza, Waheshimiwa wote waliomo katika Baraza lako Tukufu, kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi wetu waliotuchagua. Ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi hatuna budi kurejesha imani hiyo kwao, kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote, kwa dhamira na lengo la kuleta maendeleo ya nchi yetu kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu wote kuwatumikia katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako, na kwa heshima mbele yako naomba sasa niwatambue Wajumbe wa kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:

1. Mhe. Omar Seif Abeid — Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Iddi Mabrouk — Mjumbe
4. Mhe. Ame Haji Ali — Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu — Mjumbe
6. Mhe. Mussa Ali Mussa — Mjumbe
7. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame — Mjumbe

Aidha Kamati hii inafanyakazi na makatibu wawili ambao wamekuwa wakitusaidia na kutushauri kwa karibu kabisa katika kutekeleza wajibu wetu wa kuitumikia makati hii. Kwa heshima naomba niwatambue Makatibu wao ni ndugu yetu:

Ndg. Karima Abdul-Wahab	Katibu
Ndg. Talib Enzi Talib	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la lazima kwa kila wizara kuwasilisha mbele ya Baraza Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati katika Mkutano wa Baraza wa mwezi wa Septemba au Oktoba kwa kila mwaka. Kwa mujibu wa Kanuni ya 108(15) ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016 ambapo kwa mujibu wa Kanuni hii, Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ni lazima kwanza iwasilishwe katika Kamati za Kudumu ya Baraza inayosimamia ofisi hizo baada ya kuwasilishwa katika Baraza.

Kwa hivyo, Kamati ya Kusimamia Viongozi wakuu wa Kitaifa inawasilisha mbele ya Baraza lako tukufu taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya kamati ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 108(15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi**.**

Mhe. Mwenyekiti, Taarifa hii ya utekelezaji inatokana na Maagizo ya Kamati yaliyojitokeza baada Kamati kuwasilisha ripoti yake ya utekelezaji wa wizara na kujadiliwa na Baraza katika Mkutano wa Mwezi Febuari kama Kanuni ya 108(14) ilivyotuelekeza.

Katika Bajeti ya 2016/17 Kamati yangu ilitoa maagizo kadhaa kwa Taasisi inazozisimamiwa na wizara hii. Hivyo taarifa hii inatoa muelekeo wa hali halisi ya utekelezaji wa maagizo hayo, Kwa upande wa Ofisi ya Rais Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2016/17 iliagizwa na Kamati kutekeleza maagizo ambayo yalielekezwa na kuchukuliwa hatua kupitia Idara tofauti, ambapo kwa mgawanyo wa Kiidara ni kama ifuatavyo:

Ofisi ya Faragha:

Mhe. Mwenyekiti, Nianze uchambuzi wa ripoti hii kwa kuiangalia Ofisi ya Faragha ya Mhe.Rais. Nachukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya faraha ya Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la mapinduzi kwa kutekeleza baadhi ya maagizo na ushauri uliotolewa na Kamati, ikiwa ni pamoja na kuweka makontena ya kuhifadhi taka katika Ikulu ya Migombani kwa lengo la kuimarisha usafi wa mazingiza katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inaipongeza wizara na serikali kwa ujumla kwa kuhakikisha kuwa imepima na kuyapatia hati za umiiki maeneo yote ya nyumba za mapumziko za Mhe. Rais.

Pia Kamati yangu inaipongeza Ofisi ya Rais Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutenga bajeti kwa kazi ya ujenzi wa uzio wa ukuta katika Ikulu ndogo Michewezi na Mkokotoni katika mwaka wa fedha 2016/17. Aidha kwa upande wa ikulu ya Bwefum Ofisi ya Rais imefanya jitihada kubwa za kuweka uzio wa waya katika Ikulu hiyo. Kamati inasisitiza suala la ujenzi wa ukuta wa kudumu katika maeneo hayo ni jambo muhimu kwa ajili ya usalama wa nyumba hizo.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo Kamati yangu imebaini kuwa tatizo hilo bado ni kubwa mno kwa karibu Ikulu zote za makaazi ya viongozi wetu wa kitaifa. Hali hii inatishia usalama na amani ya nyumba hizo.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo Kamati yangu inaishauri serikali kulizingatia suala hili na kulipeleka katika miradi ya maendeleo ya kitaifa ili iweze kulishughulikia kwa umuhumu wa aina yake, vyenginevyo linaweza likaleta madhara makubwa katika nyumba hizo. Kamati imeona kuwa suala hili si busara kuendelea kuliachia bila ya kulishughulikia pamoja na kwamba bajeti ya wizara husika pekee haiwezi kukidhi huduma zinazohitajika ili kujenga na kudhibiti mmon'gonyoko katika majengo yetu ya nyumba za mapuumziko za Mhe. Rais. Kamati inaiomba serikali kuipa kipaumbele miradi ya kuhifadhi nyumba zote za Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Ikulu ya Mkoani licha ya jitihada zinazochukuliwa na Afisi ya Rais kukabiliana na kukabiliana mmong'onyoko wa ardhi katika Ikulu hiyo kwa kutumia ujenzi maalum wa kuweka kuta na huku ikiwa tayari Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano imeshakabidhiwa fedha kwa kazi hiyo. Kamati inasisitiza kuwa Afisi ya Rais walipe uzito suala hili ili kuwaharakisha kwamba Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano kukamilisha ujenzi huo kuenda haraka kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Afisi ya Rais kuufanyia kazi ushauri wa Kamati kwa kuchukuwa hatua za kuzuia mmong'onyoko wa ardhi katika Ikulu ya Migombani kwa kujenga misingi ya kupitisha maji na kuzuia kutokea kwa mmong'onyoko wa ardhi. Pamoja na kufanya Matengenezo makubwa katika Ikulu ndogo ya Laibon ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba ya wafanyakazi, kuweka uzio na vipoza hewa. Aidha Kamati inashauri katika maeneo ya Ikulu ya Bwefum na Kibweni, kuchukuliwa hatua za haraka za kuzuia mmong'onyoko unaosababishwa na mawimbi ya bahari yasiendelee kuathiri zaidi maeneo hayo.

Ofisi ya Baraza ya Mapinduzi

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeitaka wizara kufanya jitihada za kuiboresha maktaba katika ofisi ya Baraza la Mapinduzi sambamba na kuanzisha maktaba ya kielektroiniki yaani "*E -Library*" ili kuwawezesha Waheshimiwa viongozi kuweza kutumia maktaba hiyo mahali popote.

Idara ya Mawasiliano na Habari

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na jitihada zinazochukuliwa na Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu katika kutangaza habari na matukio mbali mbali ambayo yanamuhusu Mh.Rais. Miongoni mwa kazi nzuri wanazofanya ni kutoa jarida la Ikulu ambalo limesheheni taarifa mbali mbali za Mhe. Rais pamoja nakurusha shughuli za Mhe.Rais Moja kwa moja.

Aidha Kamati inaipongeza Afisi ya Rais kupitia Idara ya Mawasiliano kwa kuratibu shughuli za Mhe. Rais pale anapoongea na wadau na kuwezesha taarifa hizo kufika haraka kwa wananchi. Pia tunaipongeza Idara ya Mawasiliano na Habari kwa kuweza

kujikita na kasi ya ulimwengu wa habari inavyokwenda kwa kutumia mitandao ya kijamii kuweza kufikisha taarifa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mawasiliano na Habari imeweza kuimarisha Tovuti ya Ofisi ya Rais na sasa imekuwa na watumiaji wengi na imekuwa na taarifa nyingi zaidi.

Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi (*Diaspora*)

Kamati inaipongeza Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuweza kukamilisha Sera ya Diaspora pamoja na kuandaa Kongamano la Diaspora kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa kuyafanyia kazi masuala muhimu yanayowagusa Wazanzibari walipo nje ya nchi. Aidha, Kamati inasisitiza Sera ya Diaspora ifanyiwe utekelezaji wa haraka. *(Makofi)*

Afisi ya Rais Pemba

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza Afisi ya Rais Pemba kwa kupokea ushauri wa kamati wa kutenga eneo maalum la kuegesha magari ya Viongozi Pemba ambalo wanatarajia kulitekeleza kwenye bajeti ya 2018/19. Kamati inasisitiza kuwa suala hilo la kutenga eneo la kuegesha magari ya viongozi Pemba ni muhimu na linapaswa kupewa uzito unaostahiki.

Ofisi ya Usalama wa Serikali - GSO

Kamati yangu inaipongeza kwa dhati Ofisi ya Rais kwa kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti katika ofisi hii na Idara ya GSO ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Aidha, kamati inapongeza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hatua za kuandaa Sheria na Kanuni zake za uwepo wa Idara ya GSO Zanzibar. Kuwepo kwa Sheria hiyo kutaiwezesha taasisi hiyo kufanya kazi zake kwa nguvu zaidi za kisheria .

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kamati inaipongeza Ofisi ya Rais kwa kuuzingatia ushauri wa kamati kupanga kulifanyia matengenezo na kuweka thamani katika Ofisi za GSO katika mwaka wa fedha 2017/2018, ambapo kamati imeona kuwa suala hili ni muhimu na lipewe umuhimu uanaostahili. Aidha, ni jambo jema kwa ofisi hiyo kupatiwa gari kwa lengo la kurahisisha utendaji wao kwa ufanisi zaidi.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maoni ya kamati ambayo yamejaribu kwa kiasi kikubwa kuakisi hali halisi ya utekelezaji katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, ni imani yangu kuwa taarifa hii ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa yatasaidia sana kuimarisha utendaji katika ofisi hii.

Hivyo, nawaomba wajumbe wengine wa Baraza lako tukufu, waichangie vyema taarifa hii, kwa lengo la kupata utekelezaji bora wenye maslahi kwa wananchi wetu.

Mwisho ila si kwa umuhimu, napenda tena kuchukua nafasi hii binafsi kumshukuru Mhe. Spika, wa Baraza hili pamoja na watendaji wake wote kwa kutuwezesha vyema kufanya kazi zetu ipasavyo. Kwa niaba ya kamati yangu pamoja na kuwashukuru wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa. Sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili ili wamuwezeshe waziri kufanikisha kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nungwi walioniingiza Barazani hapa, naomba wawe watulivu na wastahamilivu wakijua kwamba tunafanyakazi ya kuwatumikia.

Mwisho naomba kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa, utulivu wa hali ya juu na busara zilizowatawala. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ame Haji Ali Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa uwasilishaji wako na mimi nakushukuru pia.

Waheshimiwa Wajumbe, mjadala unaendelea. Mchangiaji wetu wakwanza naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, akifuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Abdalla Ali Kombo ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kuchangia ripoti hii ya Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kazi katika Ofisi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze kamati kwa kupitia Mwenyekiti wake na wajumbe wake wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya ili kuhakikisha wanatuletea taarifa nzuri ambayo inakidhi haja katika maendeleo na utekelezaji wa shughuli mbali mbali katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nimpongeze Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Kiongozi, Watendaji wote wa wizara hii, Baraza la Mapinduzi kwa jumla kwa kusimamia vyema kazi zake na kuhakikisha kwamba nchi yetu inakwenda vizuri na kuhakikisha kwamba lililopangwa lolote linaleta mafanikio katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema shughuli zetu za nchi hii na kuhakikisha kwamba maendeleo yetu yanapatikana kwa kasi, kiasi kwamba inafaa tumpongeze kwa kila sehemu.

Mimi kwa upande wangu Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii nitaipongeza katika sehemu chache sana, na nitapata kuongeza kidogo ili twende vizuri. Mhe. Mwenyekiti, tunajua tu kwamba katika nchi yetu tuna historia kubwa ambayo inafaa kuwekewa au historia hiyo iwekwe kumbukumbu kwa sisi wenyewe na vizazi vyetu ili twende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wetu amefanya mengi na mengi aliyofanya yanaonekana. Tunaamini kwamba suala kubwa la wazee, wazee ni jambo zito na lina historia katika nchi yetu, kwamba Rais wetu wa kwanza Mhe. Abeid Aman Karume, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi alianzisha kuwatunza wazee, akawaweka nyumba za Sebleni na nyenginezo zikafuata. Pia aliwaenzi wazee hao kwa kuwapa pesa, ambapo wakati huo zilikuwa ni shilingi tano au mia tano nakumbuka nikiwa mdogo, lakini ilikuwa inakidhi haja kwa wakati huo uliopita. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini leo Mhe. Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein ameona kuna haja yale mazuri yote kuyafuata. Kwa hivyo, niseme tu kwamba nampongeza kwa dhati kabisa kwa kuona umefika wakati wazee wetu kuwaondolea mzigo ule waliokuwa wanapata na kurudisha shilingi 20,000/- kwa mwezi. Hilo Mhe. Mwenyekiti, ni jambo kubwa na la historia katika nchi yetu na linafaa kuwekwa kumbukumbu kama nitakavyoeleza baadae.

Vile vile Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akaona kuna haja mzee kumpunguzia mzigo mkubwa zaidi, akaiweka elimu bure kuanzia darasa la kwanza mpaka sekondari. Lakini kabadilisha *gear* ya pili sasa hivi mzee kumuondolea shida kabisa kwamba anataka kuona kuwa bajeti ya mwaka 2018/2019, kuanzia Julai 01 Mwenyezi Mungu akitujaalia elimu ya Sekondari yote bure. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hii ni ishara tosha kwamba Rais wetu ana imani na wananchi wake na ana imani ya kuwasaidia wanyonge juu ya shughuli zao za kila siku. Kwa hivyo, suala hili nitalitolea ushauri kama ufuatao.

Mhe. Mwenyekiti, kuiga zuri sio vibaya na kuiga zuri ndio kupata mafanikio. Haya mafaniko yaliyopatikana Rais baada ya kukumbuka elimu tokea mwaka 1964 ilikua bure, yaani mambo yote yalikua bure. Mimi pia niliwahi wakati ule nilikuwa mdogo mdogo lakini niliwahi kusoma, nilisoma mpaka nikamaliza sikuwahi kununua peni hata siku moja au pensali, kila kitu naambiwa kachukuwe unachotaka bure. Lakini baadae tena ikaondoka kutokana na hali ya maisha Rais akaona bora airudishe tena.

Kwa hivyo, naiomba wizara Mhe. Mwenyekiti, kwa kupitia hapa kwanza tuweke kumbukumbu ya historia ya nyumba ya Rais wetu wa Zanzibar wa Kwanza aliyefariki Mhe. Abeid Aman Karume, iwe ni nyumba ya kumbukumbu na kumbukumbu hiyo itakuwa ni historia kama nyumba ya Mwalimu Nyerere historia ya Mwalim Nyerere Bara. Naiomba sana wizara ilifikirie hili, kwa kuwa Rais wetu kayafanya mengi, toka kapigania siasa, katawala nchi hii kwa muda wa miaka minane, lakini miaka hiyo minane aliyotawala kaweka historia ambayo haijafikiwa, ingawa tunajaribu. Imeshakuja awamu mpaka ya sita sasa hivi, lakini kitendo alichokifanya Mhe. Rais wa Zanzibar ni historia iwekwe katika makumbusho maalum, jengo maalum ambalo litatupa jina zuri zaidi ili Rais wetu huyu Dk. Shein atapata jina zaidi.

Kwa mfano, tuna nyumba za Michenzani, Kikwajuni, Kilimani, Wete, Mkoani, Chake Chake, Micheweni, Bambi, Makunduchi, Gamba na kwengineko Mhe. Mwenyekiti, hii ni historia tosha, kwamba hii ilifanywa kwa muda wa miaka minane sio jambo dogo. Naamini kwamba mpaka leo wenzetu wanajifunza, au kila anayekuja anastaajabu ilikuwaje.

Mimi kwa bahati Mhe. Mwenyekiti, nilipata safari ya kwenda kama ziara maalum. Nakumbuka wakati huo nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, zamani lakini nilipokuwa kabla sijastaafu Uwakilishi katika awamu iliyopita. Nilipata kwenda Rwanda nilikaa kama wiki mbili nilipokwenda. Kwa Mhe. Kagame nililikuta eneo limezunguzwa anasema hapa tunataka kuanzisha mji mpya, nyumba zaidi ya 2,000 alisema hapa lazima zijengwe, wakandarasi wake wakubwa ni Machina.

Mhe. Mwenyekiti, kwa wale waliokwenda sasa hivi niliuliza wanasema zile nyumba ni kama Ulaya. Sasa hayo ndio maendeleo, na maendeleo kama yale pale yameonekana na ndio maana watu wote wamesema kwamba Rais huyu awe ni wa maisha mpaka kufa kwake, au Rais huyu aongezewe muda. Umefika muda baada ya kuona utendaji wake mzuri Rais yule wamemuongeza miaka saba ili afanye kazi zake vizuri. Kwa hivyo, suala hili nalisema vipi ukifanya vizuri basi watu watakuhitaji. Kwa hivyo, naomba sana hili liangaliwe Mhe. Mwenyekiti.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu. Mhe. Mwenyekiti, mimi navipongeza vyombo vya habari vyote vya nchi hii na vya nje vinavyotuunga mkono, kwa sababu kama hukuvitumia vyombo vya habari basi hupati faida. Mimi navipenda sana *ZBZ, ITV, Channel Ten, Star TV* na vyombo vyote kwa jumla *Zenj FM, Bomba FM, Coconut FM*, yaani sijui niseme nini vyote kwa jumla navipenda na navipongeza. Kwa hivyo, idara hii inafanya mambo mazuri, kwa sababu Mhe. Rais anatakiwa taarifa zake zipatikane na nashukuru zinapatikana vilivyo. Kwa hivyo, niiombe sana wizara iongeze bidii kwa sababu wenzetu hawa kama watatembelea katika maeneo mbali mbali kupata habari kwa wanavijiji wetu, basi maendeleo yataongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona mfano katika ukurasa wa 7 kifungu cha 2, naomba nikinukuu kama kilivyo kwa ruhusa yako;

Kifungu cha 2:

"Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu imeweka utaratibu wa kuwapeleka maofisa wake katika vijiji mbali mbali Unguja na Pemba, kwa ajili ya kupata maoni ya wananchi kuhusiana na mambo mbali mbali ya kijamii na kimaendeleo katika mwezi huu wa Septemba, 2017. Maofisa hao walitembelea vijiji vya Ngomeni, Chokocho, Mkanyageni, Kisiwapanza na Fundo. Vijiji vyengine ni Mgonjoni Unguja, Fumba, Tumbatu, Jendele na Cheju".

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawapongeza sana wenzetu hawa, lakini ningeomba kwa mimi upande wangu watembelee na mjini, sio mjini huko Mji Mkongwe hapana. Watembelee Mkoa wa Magharibi, yaani Mjini Magharibi sehemu ya Wilaya Magharibi A na B. Huko

bado kuna shida nyingi sana. Kwa hivyo, nawaomba sana wenzetu hao watembelee huko wayaone.

Kwa mfano, ukitembelea Jimbo langu mimi la Tomondo ni kwa hala kugumu na mazingira yake ni magumu, kuna mahitaji mengi ambayo kama watapata kusikia shida za wananchi basi yanaweza kufika kwa Mhe. Rais yakapatiwa ufumbuzi, kwa sababu tatizo kubwa linalotuathiri kwa upande wetu sisi ni tatizo la maji ambalo bado ni kiu na bado ni tatizo kubwa katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, ukenda Tomondo, Kwarara, Kijitoupele yaani kwa jumla Jimbo zima la Kijitoupele lina matatizo, ukenda Melinne na kwengine maji yapo ya kuchuja sana. Kwa hivyo, naomba idara hii ifanye utaratibu maalum za kuwasikiliza wananchi maoni yao. Suala la maji ni muhimu, lakini nitakulizungumza siku ya wizara husika ambapo ndugu yangu Mhe. Waziri....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Shihata naomba umalizie.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Eee. Sawa. Mhe. Mwenyekiti, mwanzo ulituambia hakuna watu wengi. Ahsante naendelea. La mwisho Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache niseme tu kwamba naiomba tena Idara ya Mawasiliano Ikulu ifanye bidii ya kufuatilia mambo mbali mbali katika maeneo mbali mbali.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ripoti hii na naipongeza kwa asilimia mia moja mimi na wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwakumbushe kwa mujibu wa kanuni ya 58(6), kila mchangiaji atakayechangia ana dakika 15, naomba niwakumbushe hilo. Kwa hivyo, kila mchangiaji ajijuwe tu kwamba yeye anachangia kwa muda wa dakika 15. Kwa hivyo, nawaomba tuzitumie dakika 15 vizuri ili nisikunyime ile raha ya kuchangia. Naomba tuendelee. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said, atafuatiwa na Mhe. Abdalla Ali Kombo, na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Saraha Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache ili kupata mustakabali wa kuweza kufanikisha katika masuala yetu ya kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza niwapongeze Marais wetu wote, nikianzia na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais John Pombe Magufuli, kwa jitihada zake kubwa sana ambazo analeta maendeleo ya haraka pamoja na kukiimarisha Chama cha Mapinduzi kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein na yeye katika jitihada

zake kubwa za kuimarisha Zanzibar na maendeleo yake na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee tena kumshukuru sana Dk. Ali Mohammed Shein. Naweza kuthubutu kusema, siwezi kupima lakini naweza kusema katika Marais ambao tumepata Rais ambaye mwenye hekima, busara na mwenye kutaka na kuleta maendeleo katika nchi hii na ni Rais asiyekuwa na tamaa, basi ni Dk. Ali Mohammed Shein Rais nambari moja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nichangie kwa kuelezea zaidi masuala ambayo tunatakiwa tuyasemee sana kwa hali na mali ambayo Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein anayafanya maendeleo makubwa sana katika nchi yetu, lakini baadhi ya watu wakisema hawayaoni, basi ni sawa sawa mtu anaweza kusema kwamba yeye kila siku anaota ndoto haidhuru anaona lakini hasikii.

Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein ameshafanya mambo mengi sana. Maana kwenye suala la afya sina la kusema, kwenye suala la elimu hakuna asiyeona, masuala anayoyapiga vita ya kudhalilisha kijinsia pamoja na jitihada za kupiga vita madawa ya kulevya na vyote vinavyohusiana na mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze tena Rais juzi tu katika Sherehe za Elimu bila ya Malipo alisema kwamba tayari anatoa au anaondosha malipo ya Sekondari. Kwa hivyo Mheshimiwa inaendelea ile ile hatua ya Elimu Bila ya Malipo, elimu siyo mas-hara kwa kiwango cha sasa kinahitaji pesa nyingi, wanaosomesha Shule za kulipia wanajua gharama yake. Lakini Dkt. Ali Mohammed Shein mzigo wote huu amejibebesha yeye na serikali yake yote haya kwa ajili ya kuwapenda wananchi wake ili wapate maendeleo ya elimu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kidogo pamoja na hotuba zilizosomwa lakini naona bado kuna haja katika Ikulu zote za Unguja na Pemba, bado kutizamwa upya na kuzifanyia maendeleo mengine ambayo yanalingana na hadhi ya Ikulu.

Mhe. Spika, mimi nataka nisemee Ikulu ya Chake Chake, kwanza pale Chake Chake barabara ya kwendea Ikulu kama Ikulu ile ya ndani bado barabara ni nyembamba sana ni hatarishi naweza kusema Mheshimiwa. Kuna haja ya ile barabara kufanyiwa ukarabati ikajazwa ni hatari dereva akiteleza kidogo hasa wakati wa mvua au likitokea jambo la dharura ni hatari kubwa sana. Ningeomba ile barabara inayokwenda Ikulu ya Chake Chake basi itizamwe upya kwa sababu ni hatari sana imekaa vibaya sana, Mwenyezi Mungu aepushie mbali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini chengine pia nataka nizungumzie barabara inayokwenda Ikulu hapa Tibirinzi, bado ile barabara imeingiwa na chaka kubwa la bahari ambayo ni mikoko au ni miti lakini ni pori na ile ni sehemu ya bahari ambayo watu wengi wanapita lakini ina pori kubwa sana. Zamani ilikuwa eneo lile linasafishwa lakini sasa imeachwa miti mikoko imeota mpaka barabarani, ni hatari si vizuri. Ningeomba kama kutakuwa na utaalamu wa mazingira pahali pale pakasafishwa ili barabara na maeneo mengine yakawa yanaonekana kwa wazi ili kuweza kuleta maendeleo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimpongeze tena Rais kwa ziara ya Wilaya zake zote za Unguja na Pemba alizozifanya na kuwakaribia wananchi kuungana nao pamoja katika kukagua mashamba ya karafuu, mashamba ya maendeleo na pia kuchuma nao karafuu. Hiyo ilikuwa ni dhana tosha ya kuona Rais wetu nini anachokizungumza katika wananchi wake na kuwapenda kwa karibu na hasa kwa zao la karafuu ambalo wanachuma na kuchambua pamoja na kukagua mashamba kwa mashamba. Hili ni lazima tumpongeze aliwapa moyo sana na aliwatia hamasa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi najaribu kusema kwamba nampongeza sana katika ushirikishwaji huo ambao ameuonesha. Sifikirii kama kuna kiongozi ambaye anaweza kuungana na wananchi kwa kiasi kile. Kwa kweli anafanya jitihada kubwa sana, kwenye makosa anatoa, kwenye mambo ambayo wananchi wanataka kutoa maoni yao anawapa ruhusa lakini pia anawashirikisha katika mambo mbali mbali, hilo lazima nimpongeze.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nimpongeze sana kwa kufungua soko la Tibirinzi hivi karibuni ambalo ni soko la kisasa kwa Zanzibar nzima hakuna. Pale katika jambo ambalo lilizungumzwa ukiachia uzuri na ukubwa wa soko ni kwamba kutakuwa na *cold room* pamoja na mashine ya kuzalisha barafu ambayo kwa siku moja inazalisha vinoo 150 na ina uwezo wa kuhifadhi tani sita za barafu. Mimi naona ni maendeleo makubwa kwa watu wa Chake Chake na maeneo mengine ambayo watakuwa na vitu vyao vya kuharibika kati ya samaki, nyama na mboga mboga, ambalo soko lile alilifungua mwenyewe na alitahadharisha sana kwamba soko lile alifungua mwenyewe na aliweka jiwe la msingi na alitahadharisha sana kwamba soko lile lilikuwa likiitwa soko la Qatar.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nithibitishe hapa kwamba mwenyewe amekataza kuitwa soko la Qatar, liitwe soko la Tibirinzi, lakini nataka kumthibitishia tu kwamba wananchi tayari wameanza kuhamasika na linarudi katika koso lake la asili, Soko la Tibirinzi. Kwa hivyo leo tunamshukuru Mhe. Rais ambaye amelifafanua hilo neno na bado linaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la Manispaa ukiachia suala la Zanzibar kwamba upande wa Forodhani nataka tuangalie kwamba upande wa Forodhani umebadilika vibaya sana. Kwa mtu ambaye anarushiwa picha ya Forodhani ya Miaka ya nyuma kwa kweli akiiona forodhani ya sasa hawezi kupajua kama pale ndio forodhani.

Mimi natoa pongezi sana kwa Rais na pongezi sana kwa Wizara inayohusika, Wizara ya Serikai za Mitaa na kazi maalum, pale wamefanya kazi nzuri sana ambayo naweza kusema lile eneo linavutia sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, ipo haja sana ya mji wetu kuutengeneza zaidi kama vile na tuliwahi kutoa maelekezo katika kuchangia tukasema basi kila mji unachangiwa kutokana na kupendezeshwa na maeneo ambayo naweza kusema matunda au miti ya asili. Tukasema kama Forodhani pamoja na mji wake wote huu basi ukipandwa mikarafuu na minazi kama ilivyopangwa kule itapendeza kweli kweli. Kwa hivyo nilikuwa nachangia sana bado kuna haja ya mji wetu kuupamba lakini sio bustani tu pamoja na miti asili ambayo inaweza ikaleta maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme upande wa barabara bado naweza kusema kwamba tuna uwezo wa kujivunia pamoja na kwamba kuna changamoto za barabara ndogo ndogo ambazo bado. Lakini nataka niseme kwamba Mhe. Rais amejitahidi sana katika kuweka mawasiliano haya ya barabara kwa Unguja na Pemba lakini mimi naweza kusema Pemba ni zaidi kwa sababu labda barabara zilizobaki ni moja, mbili ambazo ndio changa moto. kwa hivyo nasema kwamba tujitahidi sana kuzitunza zile barabara ili kuweza kuweka mambo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimpongeze Rais tena kwa juhudi zake za kuwalea wazee pamoja na kuwapa kifuta jasho cha mwezi ambacho ni nchi pekee ambayo inaweza kufanya vitu kama hivi. Kwa hivyo lazima nimpongeze sana na kwa kweli wananchi pamoja na wazee wanamshukuru sana kwa suala hilo. Lazima nimpongeze na nimuombee na duwa Mwenyezi Mungu amjaalie aendelee kuwa na afya njema pamoja na kuweza kuliendeleza taifa letu hili.

Mhe. Mwenyekiti, bado nataka nizungumze kitu kimoja ambacho kinamuelekeo wa watu ambao wanakuwa wana sura ya kuweka mambo ambayo kila siku ya kuwambia watu. Mimi nataka niweke wazi kwamba Dkt. Ali Mohammed Shein ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, hatuna budi tukubaliane na hilo na huyo ndie Rais ambaye ameapishwa, kwa hivyo mimi ningeomba wale wananchi ambao wanapoteza muda wao wanahangaika, wangine wanadanganywa danganywa, wengine wanambiwa. Ningeshauri wangefanya kazi zao wakasubiri ambalo litasemwa na serikali kwa niaba ya neno ambalo ni la uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wananchi wetu ni watu ambao wasikivu, wanakubali maendeleo lakini kuna baadhi ya watu wanapita na kuwaambia maneno ambayo hayana maana. Kuna baadhi ya watu ambao wanapita wakipotosha maneno ya maendeleo anayoleta Dkt. Shein. Mimi ningewashauri sana ndugu zangu wakati umefika asiyekubali kushindwa si mshindani, tuendelee kuijenga nchi yetu kwa pamoja, tuwe wamoja, tusifarikiane, tuweze kupata maendeleo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze kwamba Dkt. Ali Mohammed Shein amejipanga kweli kweli na amekubali kuleta maendeleo ya nchi hii. Naomba tumuunge mkono kwa asilimia mia moja na kwa wale aliowapa nyadhifa wamsaidie vya kutosha na wale waliokuwa nyuma yake basi tukubaliane na maamuzi anayoyatoa ili tuendeleze gurudumu la nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuwa na mengi sana maana mwenye macho haambiwi tazama. Dkt. Ali Mohammed Shein ni Rais ambaye amefanya mambo mengi, tunatakiwa tuyasemee sana na tuyasemee hasa. Tukubabaliane na vyombo vya habari kwa wale wenye nafasi na vyombo vya habari wayatoe na wayasambaze maendeleo anayoyafanya ili yajulikane kutoka kwenye ilani. Maana mimi nataka niseme ilani ya Chama cha Mapinduzi Dkt. Shein ndiyo anayeifata lakini mimi nina uhakika badala ya Ilani hayo anayoyafanya yeye ni asilimia mia moja tena. Ni mtu ambaye amejitahidi kuiendeleza nchi yetu katika usalama na amani na na mimi naomba Mwenyezi Mungu amjaalie maisha ambayo kwa kweli Mwenyezi Mungu amjaalie maisha marefu ambayo yatakuwa yenye afya.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja Mwenyezi Mungu atubariki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea kumwita mchangiaji mwengine kuna tangazo kidogo au taarifa ya kwamba Ijumaa kulitolewa vitabu vya ripoti ya Afisi ya Rais, Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora, lakini leo vimetolewa vitabu vyengine kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe mnatakiwa mtumie hivyo vitabu ambavyo vinagaiwa sasa na sio vile ambavyo vimegaiwa siku ya Ijumaa.

Sasa naomba nimwite Mhe. Abdallah Ali Kombo akifuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy na Mhe. Shehe Hamad Mattar ajitayarishe.

Mhe. Abdallah Ali Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwa dhati nashukuru sana kuishukuru Serikali yetu ya Mapinduzi iliyoasisiwa Januari 1964 na jemedari Mkuu wa Wakwezi na Wakulima hayati Mzee Karume. Pili kwa dhati kabisa nampongeza na kumshukuru Dkt. Shein kwa kazi zake nzuri. Pia nampongeza Waziri katika Afisi ya Rais kwa ripoti yake na nawapongeza Wajumbe wa Kamati hii kwa jinsi walivyoandika ripoti yao.

Mhe. Mwenyekiti, naishukuru tena serikali hasa kupitia maafisa wa Ikulu, Idara ya Mawasiliano na Habari kwa kazi ambayo wameifanya. Hii ni kazi moja nzuri ambayo wanajua kuna nini katika nchi yetu na nadhani ndiyo dhana kubwa ya ugatuzi sasa hivi. Maeneo ambayo yametajwa nimeyafahamu miaka 20 yalikuwa nyuma sana lakini sasa hivi kutokana na kazi ya serikali yetu imekuwa nzuri, maeneo kama Tumbatu, Fundo, Cheju nayajua na kwa mtu ambaye anaijua Cheju, ilikuwa usafiri wake mkuu ilikuwa trekta aina ya Ford na Masai Fagazon, hasa wakati wa masika. Nashukuru sasa hivi Cheju ukenda Chuchumile, Unguja Ukuu Jendele, unapita hamna shida. Naishukuru sana serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa upande wa jimbo langu la Mwanakwerekwe na hasa kwa barabara nashukuru sana niko vizuri, kuna barabara Kuu lakini pia kuna barabara ya Nyumba Mbili na tatu kabisa kuna barabara mpya ya Kwamabata Kijitoupele. Naishukuru sana Wizara ya Tawala za Mikoa kwa kunisaidia kazi hii. Lakini Wahenga wanasema "Ukishiba msaidie na mwenzako kama ana njaa".

Ningewaomba sana Maofisa hawa wa Ikulu waongeze juhudi ya kufika katika vijiji tofauti zaidi ya hivi na hasa ningewaomba wakafanya juhudi wakenda vijiji kama vya Makunduchi, wakatizama na barabara nyengine ambazo sasa hivi zinatumika kuchukua abiria kutoka Michamvi kuja Makunduchi na sio kwa wenyeji tu sasa hivi hata Wazungu wanaitumia barabara ile. Ningewaomba wao hawahusiki na ujenzi wa barabara ni Tawala za Mikoa na Mawasiliano lakini wanaweza wakenda baadaye wakaja wakaishauri Wizara hii, baada ya kwisha kusikiliza maoni ya wananchi wa Kijiji cha Makunduchi ama kijiji cha Kae.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitazungumzia Ikulu ambako kwenye kitabu hiki imezungumzwa. Ikulu ni sehemu kubwa, sehemu nzuri ni sehemu ya Mkuu wa nchi ambapo anapumzika na kupanga nini kifanyike katika nchi. Lakini sehemu kama za Makunduchi bahati mbaya hakuna Ikulu ya kiongozi yeyote wa nchi ya kwamba apumzike na kupanga mambo yake. Sasa ningeiomba Afisi hii wakatafuta maeneo angalau nako kukawa na Ikulu japo kuwa siyo kubwa lakini Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akifuatana na AG na Mawaziri wengine wote wakafikia pahali wakazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi shida ambayo ipo unaweza ukenda inabidi ikaazimwe nyumba ya mtu binafsi, nyumba zetu tunazifahamu hata ungekuwa mkubwa vipi kuna mambo hayo lazima uweke. Unaweza ukafuga mbuzi, ng'ombe sasa mpaka ufagie mavi ya mbuzi, hilo inakuwa sio vizuri. Lakini kubwa zaidi namshukuru Mhe. Rais hapa wengine wananambia wewe bwana ni mwakilishi wa wapi? Mimi kwangu kupo vizuri ukiacha maji Mwanakwerekwe kwa hivyo nimeshiba inanipasa niwasaidie na wengine wote.

Mhe. Mwenyekiti, namsifu Mhe. Rais mwezi mmoja uliopita alikwenda kwenye mwitu wa Mnywambiji Kibuteni, akawasaidia wananchi kwa kutoa maagizo ya kwamba maji ni lazima yapatikane na kwenda Makunduchi kijijini. Lakini kwa taarifa ni kwamba ukiacha maji ambayo yatakwenda kijijini kule kule kuna mashamba sasa hivi maji haya yatawasaidia wananchi vya kutosha, kwa hivyo kwa hili namshukuru sana Mhe. Rais.

Kama kawaida yangu sina maneno mengi naishukuru serikali, Ofisi hii bado ifanye kazi isiwe mwisho wa kwenda Fundo, Tumbatu, waongeze kwenda na maeneo mengine, wanaweza wakenda Fumba tumesikia juzi kuna shidashida kidogo wanaweza wakenda na sehemu nyengine kuwasikiliza wananchi wanataka nini na baadaye kupewa ripoti. Naunga mkono ripoti.

Mhe. Mweyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdalla Ali Kombo, Mwakilishi wa Mwanakwerekwe kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Said Soud Said na yeye ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Bismillahi Rahmani Rarahi, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Ofisi ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, mimi kwa kweli nitachangia mambo machache sana kwa sababu nimehisi tuchangie kwa sababu ni Rais wetu, Nchi yetu, Serikali yetu tusiache tu tukapita pita.

Jambo la mwanzo namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima wa afya kwa kuweza kufika leo hii hapa salama lakini vile vile nimpongeze sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake anazozichukua nzuri zenye utulivu zenye hekima na maendeleo.

Kwa kweli kama nilivyosema sitochangia mengi lakini nitazungumza machache ambayo yamo humu ndani ya ripoti pamoja na mawazo yangu ambayo nitayatoa kumuomba Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed na Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Jambo la mwanzo nimpongeze sana kwa juhudi zake zote anazozichukua katika nchi yetu ya Zanzibar kuhakikisha kwanza ina amani, ina utulivu na ipo katika njia ya salama kabisa hili ni jambo kubwa sana kwa viongozi ambao wachache duniani wanaopenda utulivu na wenye hekima na busara kama Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein.

Lakini vile vile nimpongeze kwa utekelezaji wake mzuri wa kufata ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi 2015 mpaka 2020 ya kutekeleza Miradi ya Mandeleo kama mfanya biashara Bakhresa miradi mikubwa miwili kwa mitatu wameifanya ikiwemo Bandari ya Zanzibar, *Mtoni Marine Hotel Project na Fumba Development y*a Fumba mambo ya mji mpya. Hili nampongeza sana Mhe. Rais kwa kum *support* na kumpa nguvu ndugu yetu Bakhresa mzalendo kuweza kui *invest* kwa masikisio si chi ya bilioni mia tano au bilioni mia sita au mi saba za Tanzania kwenye nchi yake za uzalendo kabisa.

Na vile vile tuendelee kwenye miradi mingi ambayo tunaiona wakati wa Uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tukiona Kariakoo zimejengwa upya, tukiona mambo ya Miundo mbinu yamejengwa upya, mambo ya Bandari yamo katika *procedures* yakujengwa *Airport* japo kuwa imekwama kwama kwa mambo machache tunazidi kuona itazidi kuendelea na mambo mengineyo.

Vile vile nimpongeze sana kwenye maswali ya hospitali ambayo wanajitahidi kwenye swali la afya kuhakikisha kwamba Zanzibar tutajitahidi kusahau yake mambo ambayo ya nyuma tumekuwa tukipata tabu katika masuala ya afya, nimpongeze sana kwa imani yake kuweze kusaidia sana suala la afya na kuipa vile vile bajeti nzuri kuikubalia ili wanyonge wa Zanzibar waweze kutibiwa Zanzibar na bila yakupata matatizo yoyote.

Vile vile kwenye suala la elimu pongezi zangu nampa sana kwa kuondosha michango ambayo imo ndani ya nchi midogo midogo iliyokuwa walimu wanawatolesha wazee ambao hawajiwezi na hili suala lilikuwa zito sana na linasumbua sana wazee wanyonge nampongeza sana kwa suala hili ambalo ameweze kuondosha pamoja na malipo na vitu vyengine na *uniform* kutowa bure ili suala nalipongeza sana Mwenyezi Mungu amjalie yeye Mhe. Rais Chama chetu pamoja na viongozi wake wote ambao waliomzunguka wazidi kuendesha haya maswali kwa imani.

Lakini vile vile ningemuomba Mhe. Rais akawashughulikia ipasavyo wale wote ambao watakaosababisha matatizo ndani ya nchi hii ya kuhujumu uchumi na hasa katika *project* za Serikali, tukiangalia vitu vingi vya Serikali ndani ya nchi hii vingi sana watu wawili watatu ambao wanajaribu kupenyenza mikono yao michafu ili kujipatia fedha na mambo yakienda vibaya ambayo zi mazuri kwa vile yalivyotarajiwa, tunaona mifano vitu vingi haviko katika *stage* nzuri maswali kama barabara imenyesha mvua juzi barabara karibu Zanzibar zimejaa mashimo hazifahamiki, kuna mambo yanajengwa yanakwama kwa kusingizia tuu pesa hazitoshi lakini tutizame vile vile miradi mingi ya Serikali utakuta wanapofunga *first contract* utakuta bilioni 2,000,0000,0000 lakini haujawahi kumaliza utaambiwa maana yake tumekwama kitu fulani, tumesahau kitu fulani zinaongezwa fedha kwa njia ambazo sio za ukweli.

Mimi ningemba sana kwa unyenyekevu kabisa kwa Mhe. Rais haya mambo ya watu wawili watatu yanayosababisha Serikali yake na yetu sisi kwa sote ya Chama cha Mapinduzi inayosababishwa na watu wachache ambao wanaharibu na ikaonekana Serikali nzima inafanya si vizuri wakashughulikiwa hawa watu na wakatuma akatuma watu wake akaona yeye anawaamini wachunguze haya mambo *project* nyingi za Unguja zinazofanyika Unguja na Pemba zina mikono michafu ndani yake zina mikono michafu baadhi ya watu wachache tuu ambao wanasababisha masuala haya.

Mimi namuamini Mhe. Rais na ndio maana nikasema sina tatizo naye na kwenye hotuba zangu zote najaribu kuwa muwazi kabisa kwamba Dkt. Ali Mohammed Shein pamoja na Viongozi wake wengine siwezi kusema wote kwa sababu hakuna alokamilika wapo katika safu nzuri Mhe. Rais wetu tunafahamu hana ma *scandals* ya mambo ya ajabu ajabu kama viongozi wengine wa nchi nyengine tunaowaona, mtulivu hana vurugu, hapigi watu, haiibii watu, hajachukuwa kitu cha mtu yuko safi kama na mengine madogo madogo kibinadamu hajakamilika kila mtu hajakamilika hayo ni mambo ya Mwenyezi Mungu.

Lakini vile vile nimpongeze sana Viongozi wake ambao wa Ikulu nzima Wizara nzima yake ambayo wanajitahiti kufanya mambo yake mazuri na amini mambo yake ni mazuri na tunaona hasa kwa upande wa utendaji wako vizuri, usalama wako vizuri sina haja ya kuchangia lakini ningeomba kwenye Ofisi ya Usalama wangepatia basi angalau wale usalama ambao wanamlinda Mhe. Rais nje nyuma, pembeni wavae miwani maalum zinazokuwa na *scanning* ambazo zitaweza mtu kwa kuvaa zikam-*scan* ndani ana kitu kavaa kitu cha hatari kwenye kushiriki kwasababu Mhe. Rais anajichanganya kila sehemu anakwenda maharusini, anakwenda mazishi, anakwenda kwenye mikutano angalau akivaa ile ataweza kuona mtu ndani katia kisu au kavaa kitu kibaya basi tunaomba sana na mbwa vile vile wawepo katika sehemu anayokwenda Mhe. Rais japokuwa naamini wanakuwepo mwanzo lakini wasiondoke katika eneo wazunguke zunguke Mbwa wa kunusa mambo, wa kunusa watu wabaya wawezi kuwakamata.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye jambo la Diaspora. Diaspora ndugu zetu hapa tumeona kifungu cha Diaspora kinaeleza vizuri lakini ndugu zetu hawa waliondoka Unguja sio kwa sababu hawataki nchi yao wameondoka Unguja kwa sababu hali ngumu Unguja na Serikali tukitaka tusitake hatuwezi kuwaajiri watu wote wa nchi hii tukawapa ajira na ndio maana Serikali ikandaa miradi tofauti nchi ya Wizara nje ya Serikali ili kuweza kuwasaidia wananchi wake. Hawa ndugu zetu waliokuwepo nchi tofauti Wazanzibari tunawajua wana *passport* mbili au wana *passport* ya nje tuseme *British USA* na nchi nyengine ambao wameenda kujiripua au kwa nje nyengine yoyote.

Ningeomba Mhe. Rais awaruhusu waingie imani yeye na Serikali nzima waweze kumiliki nyumba hapa maana yake nyumba wanazo lakini hawamiliki wanawapa watu wao kwa jina jengine wanatafuta njia kwa sababu wanaogopa waweze kumiliki kwa jina lao hata kama wana uraia wa *UK* wa *USA* kwa sababu tunawajua hawa ni Wanzanzibari lakini waliondoka kutokana na shida ambazo hawajaweza kujiendesha katika maisha yao na ni ndugu zetu na tunaushahidi nao hawa kweli ni Wazanzibari si watu ambao waliojipachikiza tu, ningeomba sana Mhe. Rais na Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi waweze kuwafikirika ndugu zetu hawa hata kama wana uraia wowote wa nchi

yoyote waweze kumiki nyumba kama tunavyomiki sisi wawe na haki kama tulivyokuwa tuna haki yetu sisi, mambo mengine madogo madogo si tatizo lakini kwenye masuala ya muhimu au anapokuja kufungu biashara hata kama ana *passport* ya nje waweze kupewa *priority* sawa sawa na mzalendo mwenyewe.

Hii yote imetokana kutokana na maisha magumu hali ngumu na hao hao Diaspora ndio waliochangia asilimia kubwa katika ujenzi wa nchi hii ukiangalia hii Mbweni nzima imejengwa asilimia 70 na Diaspora ambao wako nje ya nchi, mimi ombi langu lilikuwa hilo kwa Mhe. Rais.

Lakini vile vile tutamuomba Mhe. Rais kuna sheria ambayo naamini itapita kwake mwanzo kabla ya kuja kwetu sisi ambayo na mimi nilipendekeza sana katika Baraza hili wale wote ambao wabakaji Unguja kushakuwa kuna ubakaji mkubwa ndani ya nchi hii tunaipendekeza wabakaji wanoleta madawa ya kulevya, majambazi wanatumia silaha na mashoga. Mhe. Rais tunaomba atie saini waje wanyongwe ndani ya nchi hii na sisi tuko tayari kuipitisha tuko tayari kupitisha na tusipokuwa tayari tutakuja kuigundua ndani ya Baraza hili kwamba kuna watu wanasaidia haya mambo, naamini kwa Mhe. Rais imani yake na mambo yanavyokwenda ndani ya nchi na baya watu madawa ya kulevya mingi, wabakaji wanazidi, ujambazi unazidi, tunaona watu kila siku wanauliwa hatufahamu mambo yanaendelea vipi tungeomba Mhe. Rais mswada huu unapokwenda kwake auruhusu upite tunamuomba autie saini tuje tuupitishe na sisi mambo yaanze kazi. Kwa sababu naamini mitandao hii mengine ya ujambazi na madawa ya kulevya wamo watu wakubwa wa nchi hii si lazima wawemo Serikali inawezekana wafanyabiashara wakubwa watu maarufu watu wenye nguvu wamo wanaoshiriki.

Na wale ambao wabakaji wanaakili zao ningeomba sana utapoenda kwake Mhe. Rais huu mswada aukubali ausaini na sisi tutaupisha kwa nguvu zetu zote ili tuoneshe imani kwa wananchi nje kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatulitaki suala hili na tunalipinga kwa kauli zote.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Rais vile vile akaangalia hali sasa hivi ya nchi sasa hivi nchi, sasa hivi watu wauliwa nje bila ya kujulikana nini kiendelea mimi niko China kwenye *face book* kwenye mitandao yote Zanzibar ina jina baya, watu wamepigwa hivi karibuni wamechoma bisibisi, wamechomwa, wametupwa mashambani wengine watoto wadogo wametiwa kwenye magari sijui wanne wamefungiwa wamekuja kufungiwa wengine juzi kwa Mheshimiwa pale Magomeni kapigwa mengine kavunjika miguu laki 700,000/= katowa tungeomba sana Mhe. Rais aangalie sasa hivi nchi inapokwenda na wakati mwenye mtulivu, Serikali tulivu, Chama cha Mapinduzi tulivu kuna mambo nje sasa hivi yanafanyika ya majabu ajabu sasa hivi ambayo yanaiangiza nchi Zanzibar katika hali ilioyokuwa si nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, najua unataka kubinya lakini mimi nashukuru nai *support* hii ripoti asilimia mia kwa mia yale niliyoyaomba *Inshaallah* Mhe. Rais ayafikirie pamoja na Uongozi wake na yale ambayo tunaona mengine tutasaidiana tunaenda hivyo hivyo nashukuru Mhe. Mwenyekiti, namshukuru na Mwenyezi Mungu kunijaalia kuniwezesha kuzungumza haya. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-latif Mwakilishi wa Chaani sasa na mchangaji wetu wa mwisho Mhe. Waziri Said Soud na Mjumbe wa Baraza la Mapunduzi Mhe. Waziri.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum): Ahsante Mhe. Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi na awali ya yote napenda nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi hii ya kuborosha maisha ya Wazanzibari siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida ya Tanzania hapo ninapoikumbuka mimi kila inapotokea au anapotokea kiongozi ambaye anawafanyia mema Wanzazibari au anawafanyia mema Watanzania basi Serikali huwa zinawajibika pamoja na vyama vinavyotawala kufanya maandamano ya lazima kwa ajili ya kupongeza watu kama hawa, kwa vile ipo haja Zanzibari pamoja na Tanzania Bara kuandaa maandamano ya kumpongeza Rais wa Zanzibar pamoja na Rais Magufuli kutoka na harakati zao za kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kiuchumi wakati wa kati katika mazingira ambayo sasa Watanzania wanajivunia.

Mhe. Mwenyekiti, awali tulikuwa tunaandama sana kumpongeza Mwalimu Nyerere awali tulikuwa tunampongeza sana kumpongeza Rais Karume pamoja na Jumbe na wenziwao sasa mimi nashangaa kwamba ikiwa kutakuwa hakuna sababu ya kumpongeza Rais Magufili, hakuna sababu ya kumpongeza Rais Shein kwa maandamano yaani tukaandamana barabani kwa ajili ya kupongeza harakati wanazozichukuwa viongozi hao.

Nasema hivyo kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein anajali maisha ya Wazanzibari mpaka hao hawajiwezi wale ambao wako majumbani basi amepangia elfu 20,000/= kila mwezi ili na wao wajisikie kama ni raia wema katika nchi hii na wanastahiki kupata keki ya Taifa kwa namna yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuwajali wa wafanyakazi wa nchi hii amewaongezea mishahara asilimia mia kwa mia hii ni dalili ya kuwa kiongozi wa aina yake ni dalili ya kuonesha kwamba hayuko pamoja na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Rais wa Zanzibar amewakaribisha Wanzanzibari na Watanzania waliokimbia ambao wanatambuliwa kama *Diaspora* kuja Zanzibar na kufanya kama wanavyoweza katika kusogeza maendeleo, hii ni fursa ya aina yake tena ya aina yake kweli kweli kwa sababu wenzetu wale waliondoka lakini leo kutokana na ushauwishi mkubwa alioufanya yeye basi wanakuja kifua mbele na wanatembea Zanzibar kwa kifua mbele na wanaonesha dhamira ya maendeleo mbali mbali ndani ya nchi hii, Mheshimiwa hayo ni maendeleo makubwa yaliyofanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar.

Lakini pia nataka nimpongenze Mhe. Rais wa Zanzibar na Ofisi zake zote Pemba, Unguja, Tanzania Bara, Dodoma kwamba wote hawa wanafanya kazi ya kusikiliza na kutatua matatizo ya Wanzanzibari pale wanapo pelekewa, hongera sana ofisi hizi za Rais wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwambia Wanzanzibari waitumie nafasi iliyotangazwa juzi ndani ya Baraza hili la Wawakilishi kuwepo na Baraza la Wafanya biashara Zanzibar Rais wa Zanzibar kama Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na ndio Mwenyekiti wa Baraza hilo *actual* ni kwamba sasa atakuwa tayari kuowaongoza Wazanzibari katika nchi mbali za dunia kwa ajili ya kuwapeleka kuwa na wao wafanyabiashara hili ni jambo la kupongeza sana sana. Kwa sababu tumekwisha shuhudia maraisi wengi wakija na watu wengi wengi katika nchi hii wakiwa kama ni wafanya biashara. Sasa sisi Rais wetu wa Zanzibar na yeye ameanzisha Baraza na limepita humu humu ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa maana sasa na yeye ataaongoza ujumbe wa wafanyabishara kuwapeleka katika dunia hii ni bahati ya Wanzanzibari pekee sasa Wanzanzibari hii nafasi yetu na ni lazima tuutumie.

Lakini vile vile nachukua nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndani ya Bara la Afrika ni Kiongozi wa aina yake na nasema hivyo kwa sababu ameweza kuidumisha amani ya Zanzibar pamoja na Tanzania kwa jumla kwa namna yoyote ile, amani Zanzibar ipo watalii wanaingia Zanzibar usiku mchana na hawasikii hata mpira wa baskeli kupasuka pale Darajani paa hawasikii. Yote ni amani ya Zanzibar inayosimamiwa na Rais Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa vile katika mazingira ya kunyanyua uchumi wa Zanzibar iko haja ya kumpongeza sana Rais wa Zanzibar kwa maana ya kwamba uchumi wa Zanziabr umenyanyuka na maisha ya Wazanzibari yameboreka na kila siku hatua za maendeleo zinachukuliwa. Nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hatua zake za kueneza umeme katika visiwa vidogo vidogo vya Pemba vyote hii ni hatua kubwa na ya aina yake na ninasema kwamba aluta kontinyua.

Mhe. Mwenyekiti, ningetaka niseme pia kutokana na uvumilivu wake alionao Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein wa kisiasa tumeweza kufikia hatua ya kwamba sasa Zanzibar tunafanya siasa katika utaratibu wa amani na utulivu na hakuna mtu yoyote anayekerwa hii ni siasa amabayo yeye mwenyewe kwa uweledi wake au uwezo wake wa kisiasa basi vyama vyote viko huru, vyama vyote vinafanya siasa hatukuna bugudha, hakuna kelele watu wanafanya vile ambavyo sheria inawaruhusu hii ni hongera sana kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza za Mapinduzi.

Vile vile katika hatua ya mwisho kabisa nachukua nafasi hii kuwambia Wazanzibari kwamba Dkt. Ali Mohamed Shein anavijali vyama vilivyoingia katika Serikali yake ya Mapinduzi ya Zanzibr katika muundo wa Serikali yake ya Umoja wa Kitaifa, anashirikisha kwa namna zote na anawashauri wahusika wale ambao wameunda Serikali kwa pamoja bila ya vikwazo hii ni hongera sana na tunasema kwamba yule ambaye atakuja kuchukuwa nafasi yake au kukamata kijiti chake aige mfano wake. Naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nashukuru sana Mhe. Waziri Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutoa ufafanuzi wa Michango iliyotolewa na Wajumbe.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweze kuisimama

hapa tukiwa na afya njema lakini pili kuweze kukushukuru wewe kwa kuweza kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi yake ambayo yameweza kusemwa na waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, kiujumla taarifa yetu imepata wachingiaji sita (6) ukijumuisha na uchangiaji wa kamati. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu niwatambue wachangiani hao.

1. Mhe. Ali suleiman Ali
2. Mhe. Suleiman Sarahan Said
3. Mhe. Abdalla Ali Kombo
4. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
5. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum) ukijumuisha na wachangiaji wa kamati tutakuwa tuna jumla ya wachangiaji sita.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa waliochanga ni wachache sana lakini kwa sababu ya kuridhika na taarifa yetu namna ilivyowakisi yale maelekezo, maagizo na ushauri uliotolewa na kamati. Naomba niende kwa mchango wa mmoja mmoja na kile ambacho tunaweza kukitolea ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali alizungumza kiujumla mambo matatu, alizungumzia suala la elimu bila ya malipo, alizungumzia suala la kuanzisha kumbukumbu, lakini pia suala la kuhamasisha uwekezaji kwa ajili ya nyumba za makazi hasa za bei nafuu. Haya yote Mhe. Mwenyekiti, kiujumla sisi tunayachukua na kwa kuwa yote hayahusiani na utekelezaji wa shughuli zetu za kila siku, tutachokifanya sisi ni kuyaratibu kuyafikisha katika taasisi ama wizara husika kuona masuala haya yanafanyiwa kazi.

La pili alilolisema Mhe. Ali Suleiman ni suala la kutuomba tuongeze bidii katika kutembelea vijiji mbali mbali. Tumuahidi kwamba tutaongeza nguvu yetu, fedha na taratibu nyengine ili kuweza kuona kwamba watembeaji au maafisa wetu wanaokwenda kufuata taarifa za utekelezaji wa shughuli za Mhe. Rais tunawaongezea maeneo ya kwenda kutembea. Kama vile ambavyo yeye amependekeza ni kweli kwamba eneo la magharibi kwa maana ya Magharibi 'A' na Magharibi 'B' ni miongoni mwa maeneo ambayo yana wakaazi wengi na imani yetu kwamba tukiweza kufikisha maafisa wetu huko tunaweza tukapata taarifa nyingi zaidi za mwenendo na mrejesho juu ya utekelezaji wa shughuli za Mhe. Rais na serikali yetu kwa ujumla.

Mhe. Menyekiti, mchangia wa pili Mhe. Suleiman Sarahan Said, yeye baada ya pongezi alizungumzia suala la kupima kasi ya maendeleo baadhi ya watu wanavyolalamika ambao wanabeza. Mimi nimuombe kitu kidogo tu Mheshimiwa, kwamba Mwenyezi Mungu alivyotujaalia suala la macho linaona lakini wakati mwengine macho unaona kwa kulinganisha na kasi ya kitu chenyewe. Utakapotizama feni au pangaboi kikawaida linazunguruka lakini mwendo wa pangaboi ukiwa mkubwa zaidi kwa macho yako huwezi kuona kama lile pangaboi linazunguruka, aidha utaona upepo kwa maana ya kwamba utahisi upepo au sauti ya mzunguuko wenyewe.

Kwa hiyo, nimthibitishie kama kuna watu hawaoni maendeleo yanayofanyika nchini ni uthibitisho kwamba kasi yetu inakwenda vizuri na inaridhisha, asipate hofu aendelee kutimiza wajibu wake kuwatumikia wananchi wa Chake Chake na sisi serikali tutaendelea kutimiza wajibu wetu kuwatumikia wananchi wote wa Zanzibar katika shughuli za maendeleo.

La pili, Mhe. Suleiman Sarahan alizungumzia suala la eneo la Ikulu ya Chake Chake, suala la mikoko, suala la barabara. Naomba nimuahidi kwamba suala la barabara tutakaa na wenzetu na suala la mikoko tutakaa na wenzetu. Sote tunajua changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, athari za kimazingira, lakini pia na kuwa na umuhimu wa maisha ya kijani kwa maana ya kwamba uwepo wa mikoko katika eneo lile naamini kwa sehemu moja litakuwa ni jambo ambalo linashajihishwa na wenzetu wanaolinda mazingira. Kwa hiyo, hatutochukua hatua ya kukata mikoko mpaka pale wenzetu wanaosimamia suala la mazingira watakapotupa miongozo na maelekezo mazuri ili tusiathiri mazingira, lakini pia tuweze kulinda eneo letu kuwa na usalama mzuri zaidi lakini kwa kuzingatia kwamba tuna haja ya kuendelea kuwa na uoto wa kijani ili kupata neema nzuri zaidi ikiwemo mvua na mazingira safi na mazuri zaidi.

Suala jengine alilolitoa suala la Soko la Tibirinzi pamoja na eneo la Forodhani ukuta mpya na eneo la kutembea. Naamini kwamba taarifa ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itakapowasilisha basi eneo hili litakuwa ni eneo zuri na kuweza kupata tija, malengo, faida itakayopatikana kutokana na mradi huu kukamilika kwake.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Ali Kombo alikuwa na mambo mawili kiujumla. La kwanza lilikuwa suala la kuongeza maafisa wetu wanaokwenda kutembea kwa ajili ya kupata mrejesho wa taarifa na walituomba kwamba tuongeze maeneo.

Majibu ni kama ambavyo nimeweza kusema kwa upande wa mchangiaji wa kwanza, kwamba tutahakikisha maafisa wetu wanakwenda maeneo mengi zaidi ili kuweza kupata taarifa nzuri kwa ajili ya kutupa mrejesho kuweza kupima na kufanya tathmini ya utendaji kazi wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Abdalla Ali Kombo la pili alitaka kujua kwa nini Kusini hatuna nyumba ya mapumziko ya Mhe. Rais. Mhe. Mwenyekiti, suala la nyumba ya mapumziko ya Mhe. Rais maana yake tunazungumzia kuwa na Ikulu ndogo, tunapozungumzia kuwa na Ikulu ndogo tunakusudia kusema kwamba tunatakiwa tuwe na Ikulu kiukamilifu wake sio tu kwa sababu ya kwenda kupumzika Mhe. Rais, maana yake tujenge Ikulu, tuajiri wafanyakazi, tuitunze siku zote. Sasa hili si wazo baya, lakini imani yetu kwamba kwanza sasa hivi wajibu wetu wa msingi ni kuona Ikulu zilizopo tunazitunza na kuziendeleza kufikia malengo tuliyoyakusudia na pale hali ya uchumi itakaporuhusu hatuoni kikwazo cha kuweza kujenga kuwa na nyumba nyengine kwa ajili ya mapumziko ya Mhe. Rais katika maeneo ya Kusini. Lakini matarajio na imani yetu kwamba atapofanya ziara Mhe. Rais sasa hivi katika maeneo ya Kusini yapo maeneo ambayo anaweza kupata hifadhi ya kuweza kupumzika kwa ajili ya kuendelea na ziara yake.

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji mwengine ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy baada ya kutoa pongezi amezungumzia suala la kudhibiti ubadhirifu na upotevu wa fedha za serikali hasa katika maeneo ya miradi. Naomba nimhakikishie Mhe. Nadir Abdul-latif kwamba Ofisi ya Rais na serikali yote kwa ujumla haina sababu wala hakuna swalia Mtume katika kumvumilia mbadhirifu yeyote katika serikali. Lazima hatua za kisheria zichukuliwe kwa mbadhirifu yeyote kwa sababu fedha za serikali ni fedha za wananchi na malengo ya wananchi ni kuona faida ya maendeleo wanayoyapata na sio kumnufaisha mtu mmoja mmoja mifukoni mwake. Nafasi ambazo tunazitumikia wengine ni nafasi ambazo waliondoka wenzetu tumekaa sisi na sisi tutaondoka watakuja wenzetu, lazima tuoneshe *accountability* kwa hao ambao watakuwa wametumia fedha za serikali kinyume na utaratibu na maelekezo ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kiujumla mambo matatu yamejitokeza, ukitizama taarifa ya kamati imezungumzia zaidi katika masuala ya ushirikiano, umoja wao pamoja na uhusiano baina yao kamati na ofisi yetu.

Naomba niwaahidi kamati kwamba sisi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tunawathibitishia kwamba tuko tayari kushirikiana nao na tutaendeleza mashirikiano yetu katika kutimiza malengo na azma ya kuwatumikia wananchi wetu. (*Makofi*)

Tunaamini tukifanya hivyo tutakuwa tunatimiza malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini pia faida tutakayoipata tutapata faida kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu wa Unguja na Pemba. (*Makofi*)

Suala la pili lililozungumzwa kiujumla lilikuwa ni suala la kutangaza taarifa za mafanikio ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Awamu ya Saba na awamu zilizotangulia. Mhe. Mwenyekiti, niliombe Baraza lako tukufu wengi wetu tuliomo humu tunatokea katika Chama cha Mapinduzi na Chama cha Mapinduzi kilikwenda kunadi Ilani kwa wananchi wetu, basi niahidi kupitia Ilani ya Mwaka 2015 hadi 2020 kwamba tutatekeleza ilani. Tunayoyafanya serikalini ni kutekeleza ilani kwa wajibu wa kuyasema hayo ni wajibu wetu sote. Twende sote kama Wawakilishi wa CCM twende tukaseme mazuri yanayotekelezwa na serikali ya CCM. Sisi kama serikali tutasema upande wetu lakini na nyinyi kama viongozi mnaotokea katika Chama cha Mapinduzi nanyi kama viongozi mliopo katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni wajibu wenu kwenda kusema mazuri yanayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ikitokezea wamenyamaza hawasemi mazuri hii itakuwa ni adhabu kwetu sote kwa sababu kilichotuleta hapa ni Chama cha Mapinduzi tuna wajibu wa kusema mazuri yanayotekelezwa na serikali kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi, wala tusione muhali lazima twende tukaseme yanayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

La tatu, Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni suala la amani, utulivu na mshikamano katika jamii yetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba Baraza lako tukufu likubaliane na rai yangu ya kuviomba na kuvitaka lakini pia niwasihi tuviache Vyombo vya Ulinzi na Usalama vitimize wajibu wao. Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa kutulinda vina wajibu wa

kuchunguza, vina wajibu wa kubaini na atakaethibitishwa ni lazima afikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Niwasihi na niwaombe tunaporudi kwenye jamii mitaani tuendelee kuwasihi ndugu zetu, watoto wetu na jamaa zetu kuendelea kuhubiri amani, umoja, mshikamano na utulivu na wala tusiwe sehemu ya kushajihisha machafuko, uhasama, chuki na kupandikiza bughudha baina ya mtu mmoja na mtu mwengine, lakini baina ya jamii moja na jamii nyengine.

Niwaombe sote kwa umoja wetu tukirudi mtaani tuendelee kuwasihi vijana na ndugu zetu, tuendelee kuhubiri amani, umoja, lakini pia tutambue vyombo vya dola vitaendelea kufanya kazi zake kwa kubaini kila aliefanya uhalifu na kumfikisha mbele ya vyombo vya sheria.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa majumuisho yako. Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Waheshimiwa Wajumbe wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe na mimi nachukua fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kukutana tena hapa. Lakini pia na kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ripoti yake, lakini pia sitosahau kuwapongeza Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa nao kwa kuwasilisha ripoti yao kwa umakini. Vile vile niwapongeze wachangiaji wote waliochangia taarifa hii au ripoti hii kwa umahiri wao na uchangiaji wao mzuri. (*Makofi*)

Mwisho kabisa kabla ya kuakhirisha kulikuwa kuna tangazo au kuna malalamiko kutoka kwa wenzetu wa *security* pale mlangoni, wakiomba kuwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi tutakapoingia humu Barazani lazima tuwe na vile vitambulisho vyetu ili kuondosha usumbufu kupitia kwao wao pamoja na sisi.

Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe hili tulizingatie suala la uvaaji wa vitambulisho kuwaondolea usumbufu wale *security* wetu.

Waheshimiwa Wajumbe nami nichukue fursa hii kuakhirisha kikao hiki na tukutane tena saa 11:00 jioni kwa shughuli nyengine zinazofuata. Ahsanteni kwa utulivu wenu.

(Saa 6:35 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Ripoti ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Kuhusu Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehma kwa kutujaalia afya njema, hekima na kutuwezesha kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu, azidi kutupa rehema zake tuweze kutekeleza vyema mipango na malengo tuliyojipangia kwa manufaa ya wananchi na Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pongezi pekee nazitoa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa imani yake kwangu na maelekezo na miongozo anayotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi yetu. *(Makofi)*

Aidha namshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Idd kwa kutuongoza vyema hapa na nje ya Baraza. Ushauri wake na hoja zake kwetu zimefanikisha utekelezaji mzuri wa mipango yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa naomba nikushukuru wewe binafsi pamoja na Mhe. Spika, na Wenyeviti wote wa Baraza la Wawakilishi bila ya kumsahau Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndugu Raya Issa Mselem kwa kuliongoza vyema Baraza hili tukufu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nachukuwa fursa hii maalum kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi, Kamati ya Sheria Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Machano Othman Said na Makamu wake Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis pamoja na Wajumbe wote wa kamati kwa ushauri maelekezo na ushirikiano wao walioupatia wakati wa kamati ilipokuwa ikitekeleza shughuli zake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, maagizo tuliyopewa yanaonesha kwa kiasi gani kamati inavyotekeleza kwa makini na umahiri mkubwa makujumu yake katika kuhakikisha ofisi yangu inafikia malengo na matarajio yalijiwekea ikiwa pamoja na kutoa bora kwa jamii.

Mhe. Naibu Spika, taarifa hii inawasilishwa hapa kwa ajili ya kutoa majibu mbele ya Baraza lake tukufu juu ya Maagizo na ushauri kutoka Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Sheria ya Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ kwa wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Sheria ya Utawala Bora Idara Maalum za SMZ yalilenga katika maeneo yafuatayo:-

(a) Usimamizi wa demokrasia na utalawa bora nchini
(b) Usimamizi wa masuala ya sheria
(c) Usimamizi wa utumishi wa umma.

Utekelezaji wa Maagizo. Katika utekelezaji wa maagizo ya sehemu (a) yaani usimamizi ya demokarasia na utawala bora.

Agizo la 1. Mhe. Naibu Spika, kamati imeishauri serikali kuzingatia suala la bajeti katika Ofisi ya *CAG* kwa kuiongezea kifungu cha bajeti katika ofisi hiyo, ambayo umekwamisha shughuli zao.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu ilitengewa jumla ya shilingi bilioni moja, thamanini na sita milioni na mia sita kwa matumizi ya kawaida kwa matumizi wa kawaida. Kwa bajeti ya mwaka huu wa fedha 2018/18 imetengewa shilingi bilioni moja mia mbili thalathini na nane milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Mbali ya ongezeko hili wizara itazidi kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha bajeti ya Ofisi ya *CAG* inaonagezewa zaidi kwa mwaka wa fedha 2018/2019, ili iweze kutekeleza kazi zake au kazi zao ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu katika masuala ya ukaguzi kwa fedha za serikali.

Agizo la 2. Mhe. Naibu Spika, kamati inaishauri serikali katika kuhakikisha inafatilia vyema matumizi wa fedha zake ikiwapatia *CAG* wakafanyakazi wenye taalamu kwa upande wa Unguja na Pemba.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika Ofisi ya *CAG* imewasilisha mahitaji ya wafanyakazi kwa mwaka wa fedha 2017/18 na hatua za uajiri zimeanza kuchukuliwa ili kuhakikisha ofisi hii ina wafanyakazi wa kutosha na wenye taalamu wanazozitoa wanaweza kufatilia vyema matumizi ya Fedha za Serikali katika taasisi na miradi mbali mbali ya serikali.

Agizo la 3. Kamati ilimuagiza Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu kuwachukulia hatua wale wote wanasiotoa ushirikiano katika utekelezaji wa kazi za ukaguzi.

Mhe. Naibu Spika, agizo hili limepokelewa na kuzingatiwa ipsavyo kwa mujibu wa sheria hii, ili kuwachukulia hatua wale wote wasiotoa mashirikiano katika utekelezaji wa kazi za ukaguzi.

Agizo ya 4. Mhe. Naibu Spika, kamati inaishauri serikali kulingalia suala la maslahi kwa wafanyakazi wa Ofisi ya *CAG*.

Utekelezaji. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mwezi wa Aprili 2017 iliongeza maslahi ya watumishi wote wakiwemo Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu Serikali. Hatua zaidi za kuongeza maslahi ya watumishi hasa kwa Ofisi ya

CAG zitafuata kwa kadri hali ya uchumi inavyoruhusu na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Agizo la 5. Kamati inashauri Tume ya Maadili kupatia mafunzo wafanyakazi wake, kwani waliopo wameazimwa pia mazingira ya ofisi hayaridhishi kutokana na uchakavu wa jengo. Aidha, kamati imeagiza kuongezwa kwa wafanyakazi wa Tume kwa Unguja na Pemba.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Tume ya Maadili imewasilisha mahitaji yake ya wafanyakazi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na hatua za kuajiri zitachukuliwa kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu. Aidha wizara iko katika hatua ya kuwahamisha moja kwa moja wafanyakazi walioazimwa na kuwa wa kudumu wa tume. Kuhusu suala la ofisi tume inatarajiwa kuhamia katika jengo lililokuwa la balozi wa Misri baada ya kukamilika kwa matengenezo yanayoendelea.

Agizo la 6. Kamati inaagiza Tume ya Maadili kupatiwa bajeti itakayotosheleza katika utekelezaji wa kazi zake. Ushauri umechukuliwa na wizara itahusika na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Idara ya bajeti ili kulipatia ufumbuzi suala hili kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Agizo la 7. Kamati inaagiza Tume ya Maadili kupatiwa vitendea kazi na utekelezaji wake Mhe. Naibu Spika, wizara imeshauri Tume kupanga bajeti ya vitendea kazi katika bajeti yake ya mwaka 2017/2018 kwa mujibu wa fedha zilizopatiwa.

Agizo la 8. Kamati inaitaka wizara kufanya jitihada ya makusudi kuipatia usafiri Tume ya Maadili kwani hadi hivi sasa haina gari. Ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi kadiri hali itakavyoruhusu.

Agizo la 9. Kamati inashauri Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuzingatia Taasisi nyeti za SMZ ambazo zinahitaji kusaidiwa kimaslahi kutokana na kazi zao hasa zile kama za *ZAECA.*

Utekelezaji. Kwa mwaka wa fedha 2016/18 Maafisa wetu walishikiri kikamilifu katika zoezi la tathimini la kazi yaani *job evaluation* lililoratibiwa na kuedeshwa na Serikali ya Jamhuri ya Tanzania huko Tanzania Bara. Hivyo, baada ya kupata taaluma na uzoefu huo wizara inakusudia kufanya zoezi hilo hapa Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Baada ya kukamilika kwake kutatua suala zima la kimaslahi kwa taasisi nyingi za serikali ambazo wafanyakazi wake wanafanyakazi katika mazingira magumu. Ushauri unashughulikiwa ipasavyo hali itakavyoridhisha.

Agizo la 10. Kamati inashauri kuangaliwa suala la bajeti kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/18 Mamlaka ya Kuzuia Rusha Uhujumu Uchumi imepangwa shilingi milioni mia tano na thamanini mia saba elfu kwa matumizi ya kazi za kawada ikilinganishwa na shilingi mia nne na thamanini milioni

kwa kipindi kilichopita. Wizara itawasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Idara ya bajeti kuhusu ushauri huu na bajeti ya *ZAECA* kuongezwa, ili kuleta ufanisi na tija kwa mamlaka ya kupambana kikalifu na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi kwa faida ya taifa na wananchi kwa jumla.

Agizo la 11. Kamati inaushauri suala la usafiri lipewe kipaumbele katika mamlaka kwani linawakazwa katika utekelezaji wa shughuli zao za kazi.

Utekelezaji. Ushauri umepokelewa na hatua zitachukuliwa kadri ya hali ya bajeti itakavyoruhusu mamlaka itapatiwa magari kuwezesha kutekeleza majukumu yake.

Agizo la 12. Kamati inasisistiza kuchukuliwa hatua na kupatiwa Ofisi ya Mamlaka ya kuzuia rushwa Unguja uhujumu uchumi na wizara itajitahidi kuwapatia ofisi ya kudumu kwa upande wa Pemba.

Utekelezaji. Hatua zimechukuliwa kupatia mamlaka ofisi ambapo kwa upande wa Pemba imefungua ofisi katika mikoa yote miwili. Aidha ya jengo jipya ya wizara huko Gombani Chake Chake utakapokamilika mamlaka itapatiwa ofisi ya kudumu ya uhakika.

Agizo la 13. Kamati inaagiza kupatiwa vifaa vya kufanyia kazi Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Utekelezaji agizo hili limepokelewa ambapo kwa hatua ya awali wizara kushirikiana na mamlaka itaanda andiko la mradi kuhusu ununuzi wa vifaa uliowasilishwa Tume ya Mipango. Aidha mamlaka imechukuwa hatua za makusudi kuanza kununua baadhi ya vifaa na vitendea kazi.

Agizo la 14. Suala la ushirikiano katika jitihada za kupambana na rushwa kamati imeitaka wizara kuchukuwa hatua kwa wale wote wasiotaka kutelekeza azimio hilo.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, hatua hizi zinaendelea kuchukuliwa wizara imeandaa mpango mkakati wa mashirikiano na uadilifu katika kupambana na rushwa kati ya wahusika kwa masuala la kupambana na rushwa ili kuimairisha mashirikiano katika kupamabana na rushwa. Mpango huo tayari umewasilishwa kwenye kikao cha bajeti kwenye Baraza la Mapindizi.

Agizo la 15. Kamati inaagiza mamlaka kwa ajili ya wafanyakazi wenye ujizi maalum katika fani ambazo wanazihitaji kutekelezaji zao.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, mamlaka tayari imeshawasilisha serikalini nafasi za uajiri kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba mamlaka liwaajiri watu wenye sifa maalum katika fani maalum mbali mbali zinawezesha kutekeleza kazi zao katika taasisi hii.

Agizo la 16. Kamati inashauri kuangaliwa suala la usalama kwa wafanyakazi wa *ZAECA.*

Utekelezaji. Mawasliano na Serikali Kuu yanaendelea kuhusiana na usalama wa wafanyakazi wa *ZAECA* ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao bila ya woga wala vitisho.

Mhe. Naibu Spika, katika kusimia utekelezaji wa sekta ya sheria nchini kamati ilitoa maagizo yafuatayo kifungu b hicho cha pili.

Agizo la 1. Kamati inaagiza wizara kuwashikisha wanasheria wa serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tokea hatua za awali na sio kuwapatia wanasheria hao mswada husika kwa ajili ya kufanyia kazi ili kuepusha ucheleweshwaji katika miswada pamoja na miswada kuwa na mapungufu.

Utekelezaji. Ushauri umepokelewa, hata hivyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imehakikisha kuwa kila wizara kuwe na Mwanasheria wa Serikali alietangazwa katika gazeti rasmi la Serikali na Mwanasheria Mkuu. Hatua hii imesaidia ushirikishwaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika hatua za awali za uandaaji wa miswada kabla ya kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kufanyiwa kazi.

Agizo la 2. Mhe. Naibu Spika, kwenye eneo hili, kamati inaishauri serikali kupitia taasisi zake kuzingatia na kusimamia kwa umakini mkubwa masharti ya mikataba.

Utekelezaji. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeanzisha utaratibu wa kusajili mikataba yote ya serikali na kuifanyia mapitia ili kubaini kasoro zilizomo na kuzishauri mamlaka husika ipasavyo. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inaendelea kutoa mafunzo ya mikataba kwa taasisi za serikali ili kuimarisha usimamizi wa mikataba hiyo.

Agizo la 3. Kamati inaagiza kufanyiwa kazi suala zima la udhalilishaji kwani limekuwa ni changamoto kubwa inayokabili jamii na hata kukosekana imani kwa chombo cha Mahakama na jamii.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, suala la udhalilishaji limeanza kufanyiwa kazi tokea mwezi Machi, 2017; ambapo mikakati maalum ya kupambana na kesi za udhalilishaji umeanzishwa kwa mashirikano makubwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mahakama pamoja na Jeshi la Polisi. Hali hii imepelekea Mahakama kusikiliza kesi za udhalilishaj kwa muda mfupi na kutoa maamuzi na kusaidia jamii kuanza kujenga imani kwa mahakama.

Agizo la 4. Mhe. Naibu Spika, kamati imebaini kuwepo kwa idadi kubwa kwa rumande kuliko wanafunzi, kitu ambacho kinapelekea kutia hasara serikali. Kamati inaagiza Mahakama kuzifanyia kazi haraka kesi hasa za mazao na mifugo na kuzitolea maamuzi kwa lengo la kupunguza mrundikano wa rumande.

Utekelezaji. Hivi karibuni Mhe. Jaji Mkuu ametembelea magereza yote ya Unguja na Pemba, ili kubaini changamoto iliyoko na ameanza kuchukua hatua kwa kuwaagiza Mahakimu kutoa dhamana kwa rumande kwa mujibu wa sheria pamoja na kusikiliza kesi za mazao na mifugo kwa muda mfupi. Aidha, suala hili kwa upande mwengine

linachangiwa na wanafamilia kutokuwa tayari kuwadhamini wahalifu wa mazao na mifugo.

Agizo la 5. Kamati inaagiza kufanyiwa kazi suala la vitendea kazi kwa Mahakama zote za Unguja na Pemba.

Utekelezaji. Suala la vitendea kazi limekuwa likifanyiwa kazi kadiri ya fedha zinapopatikana. Hata hivyo, ufinyu wa bajeti wa Mahakama umechangia ukosefu wa vitendea kazi vya kutosha ikilinganishwa na wingi wa Mahakama zetu katika maeneo ya Unguja na Pemba.

Agizo la 6. Kamati inaishauri kuanza mara moja ukarabati wa jengo la Mahakama ya Mwanakwerekwe kwa fedha walizotengewa kwani liko katika hali mbaya.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, ukarabato wa jengo la Mahakama ya Mwanakwerekwe umeanza tokea Aprili na uko katika hatua za mwisho kabisa kukamilika na kukabidhiwa. Ukarabati wa jengo hilo umefanywa na Mkandarasi kutoka Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo KMKM na fedha zote za ukarabati huo ambazo ni shilingi milioni 131 zimeshalipwa.

Agizo la 7. Kama inaishauri wizara kufanya jitihada za makusudi kujenga Mahakama ya Mfenesini, Wete, Konde na Kengeja. Ushauri umepokelewa na wizara kwa kushirikiana na mahakama na imeanza jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga Mahakama ya Mfenesini, Wete, Konde na Kengeja. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kipaumbele kimewekwa kwa kuanza ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu.

Agizo la 8. Kamati inashauri kufanya jitihada za matengenezo ya jengo la Mahakama ya Mkoani kwa upande wa ndani ambao haukukarabatiwa na mradi wa *ZUSP*.

Utekelezaji. Ushauri umepokelewa na ukarabati wa jengo la Mahakama ya Mkoani utafanyika kama ulivyoshauriwa.

Agizo la 9. Kamati inaishauri Mahakama kuandaa programu maalum ya kutoa elimu kwa jamii juu ya Sheria ya Ushahidi katika masuala ya kesi ya udhalilishaji, ili jamii kuwa na muwamko juu ya ushahidi vipi ushahidi unaotakiwa kisheria.

Mhe. Naibu Spika, ushauri huu ni mzuri sana na katika kuufanyia kazi Mahakama imeandaa programu maalum ya kutoa elimu ya jamii juu ya Sheria ya Ushahidi ikiwemo ushahidi upi unatakiwa kisheria na hatua ya kuchukuliwa kuupata ushahidi bila ya kuharibu ushahidi wakati tukio lilipotokea.

Aidha, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nayo imekuwa na programu maalum kutoa elimu ya jamii kuhusu umuhimu wa ushahidi. Kauli mbiu ya ofisi hii ni hakuna hatia bila ya ushahidi, usikatae, usidharau kutoa ushahidi. Halikadhalika hatua zimechukuliwa kwa kushirikiana na asasi zisizo za serikali zikiwemo Chama cha Wanasheria Wanawake (*ZAFELA*) na Kituo cha Huduma cha Sheria (*ZLC*), kutoa elimu kwa jamii juu ya masuala ya ushahidi hasa katika kesi za udhalilishaji.

Agizo la 10. Mhe. Naibu Spika, kamati imeshauri katika masuala ya kesi za utoaji wa ushahidi ni vyema ikawepo Sheria ya *Protection Act* ambayo itawalinda watoaji ushahidi kama ilivyo Kenya.

Utkelezaji. Ushauri umepokelewa na tayari vyombo vyetu vya sheria vimeanza kujadili uwezo wa sheria ya *Witness and Victim Protection Act* hapa petu Zanzibar kama vile nchi nyengine ikiwemo Kenya. Hivyo, katika miaka ijayo sheria hiyo itakuwa imeanzishwa kuweza kusaidia jamii kujitokeza kutoa ushahidi Mahakamani.

Agizo la 11. Kamati imeona ni busara kuwepo kwa kifungu maalum cha kuwalipa mashahidi angalau fedha za nauli, ili kuwashajihisha kutoa umuhimu wa kutoa ushahidi mahakamani. (*Makofi*)

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Mahakama imekuwa na utaratibu uliojengeka miaka mingi kwa kuwalipa mashahidi wote wanaofika Mahakamani kutoa ushahidi katika kesi za jinai. Kifungu hicho cha malipo kwa mashahidi kimezingatia zaidi pesa za nauli kutegemea na sehemu anayotoka shahidi husika kama ni ndani au nje ya nchi Mahakama inawalipa.

Agizo la 12. Kamati inaliona suala la nyumba ya kukaa majaji litizamwe kwani ni muhimu hasa kwa upande wa Pemba.

Utekelezaji. Ushauri umepokelewa na tunaahidi kuufanyia kazi.

Agizo la 13. Kamati inashauri kurejeshwa utaratibu wa Mahakama kuwa na kuachanga na kutegemea fungu kutoka wizarani, ili kupunguza changamoto zinazojitokeza katika utaratibu huo.

Mhe. Naibu Spika, Mahakama haijawahi kuondolewa fungu la bajeti na kutegemea fungu kutoka wizarani, isipokuwa Mahakama inaendelea kwa fungu lake la bajeti ambalo ni GO2. Kilichojitokeza katika mwaka wa 2016/2017 kwa kupitia mradi wa mageuzi ya sekta ya sheria, fedha za ukarabati wa Mahakama ya Mwanakwerekwe na mtayarishaji wa ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu, zimeingizwa katika fungu la wizara. Hata hivyo, mwaka wa fedha wa 2017/2018 fedha za maendeleo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Mahakama ya Tunguu zimeingizwa kwa kupitia fungu la Mahakama moja kwa moja.

Agizo la 14. Mhe. Naibu Spika, Kamati inaishauri Ofisi ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kufuatilia na kufanya uwadilifu wa hali ya juu katika kesi zinazohusu madawa ya kulevya.

Utekelezaji. Ushauri umepokelewa na kwamba Mkemia Mkuu wa Serikali amekuwa muadilifu sana katika kesi za madawa ya kulevya, kwani kwa kipindi kirefu sana haijajitokeza Mkemia kutoa majibu ya uchunguzi yasiyokuwa sahihi.

Agizo la 15. Kamati inaagiza kupitiwa upya na kufanyiwa marekebisho Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya mwaka 2004. Mhe. Naibu Spika, sheria hii tayari imeshafanyiwa

mapitio na rasimu ya sheria mpya imeandaliwa, inayopendekeza kufuta sheria ya sasa namba 6 ya mwaka 2004.

Aidha, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya mwaka 2004, nayo imefanyiwa mapitio na kupatikana na rasimu mpya inayopendekeza kufuta sheria hii iliyopo. Sheria hizi mbili zinakwenda sambamba na maisha na zinategemeana katika utekelezaji wake. Hivi ninavyozungumza sheria hizi zimeshawasilishwa kwenye kikao cha Makatibu Wakuu na kutegemea kuwasilishwa hapa Barazani katika kikao kijacho.

Agizo la 16. Kamati inashauri kuwepo kwa mashirikiano kati ya Jeshi la Polisi na *DPP*.

Utekekezaji. Mashirikiano yameimarishwa kati ya Jesho la Polisi na *DPP*, ambapo kila mwezi tumekuwa na kikao cha pamoja kati yao kujadili masuala mbali mbali ya upelelezi wa kesi ya uendeshaji wa mashtaka na kukubaliana juu ya hatua stahiki za kuchukuliwa katika suala zima la mashtaka.

Agizo la 17. Kamati inaagiza kufanyiwa marekebisho Sheria Nam. 4 ya mwaka 2005 ya Kuwalinda Wari na Wajane, ambayo ina matatizo kwani haiwezi kumshtaki mtu ambaye atampa mimba mtoto chini ya umri wa miaka 18 na kusababisha upande mmoja kukosa haki ya kesi hiyo.

Utekelezaji. Sheria Nam. 4 ya mwaka 2005 itafanyiwa mapitio na kurekebishwa kasoro ziliopo. Hata hivyo, mtu ambaye atampa mimba chini ya umri wa miaka 18 basi atashtakiwa chini ya Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya mwaka 2004 kwa makosa mawili, ambayo ni kubaka pamoja na kumpa ujauzito msichana.

Agizo la 18. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua za haraka za kuwaajiri waendesha mashtaka na wafanyakazi wengine, hasa kwa upande wa Pemba, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu hayo.

Utekelezaji. Hatua zimechukuliwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, ambapo mwezi Juni 2017 imeajiri jumla ya waendesha mashtaka 13 na dereva mmoja, ili kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu yao. Hatua zaidi za kuajiri zitachukuliwa kadiri hali ya fedha ya serikali itakaporuhusu.

Agizo 19. Kamati inaagiza wizara kulifanyia kazi suala la usafiri katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba. Wizara imemshauri Mkurugenzi wa Mashtaka kutenga bajeti ya ununuzi wa gari katika bajeti yake ya mwaka 2018/2019 kwa lengo la kulifanyia kazi suala la usafiri huko Pemba.

Agizo la 20. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua wale wote wanaofumbia macho vitendo vya udhalilishaji, kumalizana wenyewe kwa wenyewe na kutuma maombi ya kufuta kesi. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, inaendelea kuelimisha jamii juu ya athari za kufumbia macho matendo ya udhalilishaji. Hata hivyo, serikali haitasita kuwachukulia hatua wale wote wanaoyafumbia macho vitendo vya udhalilishaji kwa mujibu wa sheria. Aidha, kukataa kutoa ushahidi ni kosa kisheria na hatua zimekuwa zikichukuliwa kwa wale wote wanaokataa.

Agizo la 21. Kamati inaagiza kuwa suala la mashirikiano katika masuala ya haki za jinai, liwe ni suala la lazima kwa wale wote ambao wanahusika, ili uendeshaji wa kesi na upatikanaji wa haki uwepo kwa wakati.

Utekelezaji. Vikao vya Mashirikiano katika Masuala ya Haki za Jinai, vimekuwa vikifanyika kwa wahusika wote, ambapo kila muhusika anashurutishwa kutekeleza wajibu wake. Aidha, wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 inakusudia kuandaa Sera ya Mashtaka, ambayo itasaidia kutoa muongozo wa suala la mashirikiano katika masuala ya upatikanaji wa haki za jinai.

Agizo la 22. Kamati inaagiza wizara kwa kupitia Wizara ya Afya, kufanya utaratibu wa kuongeza waanyakazi wa Ofisi ya Wakala wa Mkemia Mkuu Pemba, ili kesi zote zinazohusu madawa ya kulevya ziweze kuendelea kwa kiutaratibu na kuondokana na malalamiko yaliopo kwa sasa vyombo vya upatikanaji haki.

Utekelezaji. Suala la kuongeza wafanyakazi linategemea bajeti na mpango wa rasimali watu ulioandaliwa na wizara husika. Hata hivyo, wizara itakaa na Wizara ya Afya, ili kulijadili suala hili kwa upande wake ili kuondosha kasoro hiyo.

Agizo la 23. Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti kuwa na mashirikiano na Ofisi za *DPP* katika kesi za walimu wa madrasa, ili kuwezesha kujua na kupata taarifa juu ya kesi hizo.

Utekelezaji. Ushauri umepokelewa na Ofisi ya Mufti inashirikiana kikamilifu na Ofisi ya *DPP* pamoja na Jeshi la Polisi, ili kupata takwimu sahihi za walimu wa madrasa wanaotuhumiwa na kushtakiwa kwa kesi za udhalilishaji dhidi ya watoto.

Agizo la 24. Kamati inashauri suala la vitendo vya jinsia moja. Ofisi ya Mufti itowe barua kwa Maimamu wote ili watowe elimu ndani ya Misikiti kwa lengo la kuisaidia jamii kwa kesi hizo.

Utekelezaji. Ofisi ya Mufti hivi karibuni imezitembelea wilaya zote za Unguja na Pemba na kutoa elimu juu ya ubaya wa vitendo vya jinsi moja, kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto na mmong'onyoko wa maadili, ambapo Maimamu wote wamesisitizwa kuendelea kutoa elimu hiyo kwa kupitia mihadhara na hotuba za Ijumaa.

Agizo la 25. Kamati imeagiza Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kulichukulia hatua suala la Ofisi ya Mufti kupatiwa *vote* yake na kuongezewa bajeti kwa mwaka ujao.

Mhe. Naibu Spika, suala hili tayari limeshawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango. Wizara inategemea kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Mufti itapatiwa *vote* yake. Aidha, katika kufanikisha suala hili, wizara imeanza kuchukua hatua ya kuipandisha hadhi Ofisi ya Mufti kwa kufanya mapitio ya sheria ya Mufti ili kuwezesha kupatiwa *vote* yake.

Agizo la 26. Kamati inaagiza kuwachukulia hatua wale wote ambao watatoa kazi za wasanii kinyume na utaratibu. Ofisi ya Haki Miliki itawachukulia hatua wanaotoa kazi za wasanii kinyume na utaratibu, na imekuwa ikiwaelimisha wafanyabiashara na watumiaji wa kazi za wasanii kuzisajili na kulipia mirahaba.

Agizo la 27. Kamati inaishauri serikali kutilia mkazo suala la Sheria ya Ndoa za Kiislamu, ambapo hadi sasa haipo na ni tatizo. Mhe. Naibu Spika, suala la Sheria za Ndoa za Kiislamu inahitaji majadiliano ya kina, kwa sababu ni suala la kidini ambapo taratibu zake na miongozo yake imeelekezwa kwenye *Qur-an* tukufu na *Sunnah*, pamoja na sheria za Kiislamu kwa ujumla.

Hata hivyo, Ofisi ya Mufti kwa kushirikiana na Mahakama ya Kadhi kumekuwa na utaratibu wa kuwaelimisha wananchi kwa kupitia Maimamu wa Misikiti, juu ya masuala ya ndoa za Kiislamu na utatuzi wake wa migogoro hiyo. Kesi zinazotokana na ndoa za Kiislamu.

Aidha, wizara imeshaandaa Sheria mpya ya Mahakama ya Kadhi na itawasilishwa Barazani, ikiwa ni kwa lengo la kusaidia kuondosha au kupunguza kasoro hizo.

Agizo la 28. Kamati imeishauri Tume ya Kurekebisha Sheria, kufanya jitihada za makusudi kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na mambo ya sheria.

Utekelezaji. Tume inazo programu maalum za elimu kwa ujumla juu ya mambo ya sheria, ili kuwezesha jamii kupata uelewa na mwamko juu ya mambo ya kisheria, hasa katika ufuatiliaji wa haki. Aidha, wizara kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia imekuwa ikitoa elimu kwa jamii kuhusiana na mambo mbali mbali ya kisheria.

Agizo la 29. Kamati imeiagiza Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kufanya mawasiliano juu ya ushiriki wa maofisa kutoka katika taasisi mbali mbali za serikali, na kuhakikisha wanashiriki katika mapitio ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria.

Utekelezaji. Tume ya Kurekebisha Sheria itawashirikisha kikamilifu maofisa kutoka taasisi mbali mbali za kisheria na za kiraia, pamoja na wananchi wa Wilaya zote za Unguja na Pemba kila wanapopitia sheria. Moja ya tatizo inalokabili Tume ya Kurekebisha Sheria, ni baadhi ya sheria ya kufanya mapitio ya sheria bila ya kushirikisha na tume hiyo, ambapo ndio yenye jukumu la kurekebisha sheria nchini.

Mhe. Naibu Spika, natoa wito kwa taasisi husika zote kushirikiana na tume katika mapitio ya sheria zao.

Agizo la 30. Kamati inaishauri wizara kutenga fungu maalum ambalo litawezesha taasisi kupata vitabu vya kutosha kuweza kukidhi mahitaji ya tume.

Utekelezaji. Wizara kwa kupitia mradi wa mageuzi ya sekta ya sheria, umetenga fedha maalum chini ya ushirikiano na *UNDP*, ili kusaidia upatikanaji wa vitabu vya Tume ya Kurekebisha Sheria, vitabu ambavyo vinatarajiwa kuwasili mwaka huu wa fedha 2017.

Aidha, wizara imeagiza tume kuwa na utaratibu wa kutenga fedha za bajeti kwa ununuzi wa vitabu ili kuwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Agizo la 31. Kamati inasisitiza kuwepo kwa mashirikiano kati ya Ofisi ya *DPP*, Polisi, Mahakama na jamii katika kuleta ufanisi wa uendeshaji wa kesi.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, hatua mbali mbali za ushirikiano kati ya Ofisi ya *DPP*, Polisi, Mahakama pamoja na jamii zimekuwa zikichukuliwa. Kwa mfano, Mahakama inaratibu na kuendesha kikao cha kuharakisha usikilizaji wa kesi kila robo mwaka, ambapo wajumbe wake ni vyombo vyote vinavyohusika na upatikanaji wa haki za jinai. Kama vile *DPP*, Polisi, Chuo cha Mafunzo, Mkemia Mkuu wa Serikali na wengineo.

Eneo la C na la 3 ni Usimamizi wa Masuala ya Utumishi wa Umma:

Mhe. Naibu Spika, katika kusimamia Utumishi wa Umma na Maslahi ya wafanyakazi ya watumishi. Kamati ilitoa maagizo yafuatayo.

Agizo la 1. Kamati inashauri kuchukuliwa hatua kwa kulifanyia kazi suala la maslahi ya wafanyakazi nchini.

Utekelezaji. Hatua za kulifanyia kazi suala hilo la kuzingatia maslahi ya wafanyakazi kwa kima cha chini cha mashahara zimechukuliwa. Serikali imepandisha mshahara wa kima cha chini kwa asilimia 100, maslahi ambayo yameanza kulipwa tokea mwezi wa Aprili, mwaka 2017.

Agizo la 2. Kamati inashauri kuangaliwa muongozo wa watumishi wa umma kwa watu wenye ulemavu katika suala la ajira.

Utekelezaji. Tume ya Utumishi Serikalini inatoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu au mahitaji maalum, kama ilivyoelekezwa na Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kwa mujibu wa kifungu cha 30.

Agizo la 3. Kamati inaagiza kufanyiwa kazi kwenye Tume ya Utumishi Serikalini, upatikanaji wa vitendea kazi vya wafanyakazi.

Utekelezaji. Wizara imeishauri tume kupanga bajeti ya vitendea kazi katika bajeti yake kwa mujibu wa fedha zilizopatikana. Aidha, tume imeshawasilisha mahitaji yake ya wafanyakazi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na hatua tayari inachukuliwa kadiri ya hali itakavyoruhusu.

Agizo la 4. Mhe. Naibu Spika, kamati inashauri kuangaliwa suala la bajeti ya tume kwa mwaka ujao wa fedha iongezwe na ipatikane kwa wakati. Ushauri huo umepokelewa na wizara itawasilisha ombi hili Wizara ya Fedha na Mipango, ili kuangalia bajeti ya tume kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Hata hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango inaanza kulipatia ufumbuzi suala la upatikanaji wa fedha kwa kutoa fedha za bajeti kwa wakati kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa.

Agizo la 5. Kamati inashauri kufanyiwa kazi suala la nidhamu kwa wafanyakazi ili kufanya huduma hizo kuwa bora zaidi.

Utekelezaji. Wizara imetoa muongozo unaoelekeza ofisi zote za serikali kuandaa mikataba ya utoaji wa huduma kwa mteja, ili kuimarisha uwazi, uwajibikaji, nidhamu, uwadilifu na utoaji wa huduma bora wa jamii. Karibu ofisi zote zimeshakamilisha maandalizi ya mikataba hiyo.

Aidha, hatua mbali mbali za nidhamu zimechukuliwa za kila muajiri na wengine zitawasilishwa Tume ya Utumishi kwa hatua zaidi.

Agizo la 6. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tume ilitarajiwa kununua gari moja ambalo litasaidia katika kutekeleza kazi zake na hatua zaidi za ununuzi wa gari zitachukuliwa katika bajeti ijayo.

Agizo la 7. Kamati imeagiza wizara kwa upande wa Pemba kupatiwa jengo lake ili kuepuka changamoto zinazojitokeza hivi sasa.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, imelifanyia kazi suala la ukosefu wa ofisi ambapo kwa sasa jengo jipya la kisasa linajengwa maeneo ya Gombani Chake Chake. Kukamilika kwa jengo hilo kutatatua kwa kiasi kikubwa changamoto za ukosefu wa ofisi Pemba.

Agizo la 8. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua suala la upungufu wa wafanyakazi katika kitengo cha usajili wa haki miliki. Wizara imeshatoa kibali cha uajiri wa nafasi 17 kwa ofisi ya haki miliki kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Nafasi hizo zitaondoa changamoto na upungufu wa wafanyakazi kwa Unguja na Pemba.

Agizo la 9. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua suala la usafiri kwa upande wa Pemba katika Ofisi ya Haki Miliki. Mhe. Naibu Spika, agizo hili litatekelezwa kadiri hali ya fedha itakapoturuhusu kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kwani kwa fedha za mwaka 2016/2017 ofisi hii iliweza kununua gari moja ambalo linatumika katika ofisi hapa Unguja.

Agizo la 10. Kamati inashauri katika kupambana na tatizo la uhaba wa wafanyakazi huko Chuo cha *IPA*, kufanywe utafiti ili kujua chanzo cha tatizo na kuweza kutoa elimu iliyobora. Ushauri huu umepokelewa na chuo kitafanya utafiti.

Agizo la 11. Kamati inaishauri serikali kutumia Chuo hiki cha *IPA* kufanya tafiti mbali mbali za kitaaluma na kuweza kutambulikana na kuwa na hadhi ya kitaifa.

Utekelezaji. Ushauri huu umepokelewa hasa ikizingatiwa madhumuni ya kuanzisha chuo hiki ni pamoja na kufanya tafiti mbali mbali zinazohusiana na taasisi hiyo.

Agizo la 12. Kamati inaagiza wizara zote za serikali ziwe na bajeti ya kusomesha watumishi wao kama sheria ya uajiri inavyopendekeza.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kila wizara na taasisi zote za serikali zimekuwa zikitenga bajeti za kusomesha watumishi wao. Aidha, wizara yangu imeandaa rasimu ya Sera ya Mafunzo kwa Watumishi wa Umma, kutoa miongozo kamili wa mpango wa kuendeleza watumishi kitaaluma, na suala zima la utengaji wa fedha za bajeti kwa kusomesha watumishi wao. Sera hiyo imeshapitishwa na wahusika wote wa utumishi wa umma, wakiwemo mashirika ya umma ya serikali na wakala tendaji.

Hatua iliyobaki ni kuwasilisha rasimu hiyo katika ngazi za wizara na hatimaye kuwasilisha katika vikao vya Makatibu Wakuu.

Agizo la 13. Kamati inashauri katika bajeti inayokuja chuo kizingatie mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa kuwapatia vifaa vya kisasa. Ushauri huu umepokelewa na tutaufanyia kazi katika bajeti ya mwaka 2018/2019.

Agizo la 14. Vile vile kamati inaagiza chuo kwa ajili ya wakalimani ambao watawasaidia wanafunzi wenye ulemavu na viziwi.

Utekelezaji. Chuo kitaendelea kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu katika bajeti hiyo ijayo, na kwamba uajiriwa wa wakalimani utafanyika ili kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu na uziwi.

Agizo la 15. Kamati inaagiza waajiriwe wafanyakazi wa chuo kwa Tawi la Pemba.

Utekelezaji. Agizo hili limeanza kufanyiwa kazi, ambapo kwa hatua ya awali watumishi 6 watahamishiwa kutoka katika wizara kwenda chuo, ili kuwa walimu wa kudumu.

Agizo la 16. Katika suala la watumishi wa serikali wanaostaafu kuongezewa muda. Kamati inaomba serikali itamke rasmi kada maalum ambazo zinafaa kuongezwa muda watumishi wake. Suala hili ni la kisheria ambapo Sheria ya Utumishi wa Umma kupitia *notice* ya Mhe. Waziri anayeshughulikia Utumishi wa Umma, imeweka masharti maalum ya wastaafu kuongezewa muda, masharti ambayo yamekuwa yakitekelezwa kikamilifu.

Agizo la 17. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua za ununuzi wa vifaa katika idara na taasisi za serikali.

Hatua za utekelezaji zimechukuliwa ambapo kila idara na taasisi zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vitendea kazi.

Mhe. Naibu Spika, Agizo la 18. Kamati inashauri vifungu vya fedha vya Taasisi ya Nyaraka viwe vinaingiziwa Idara ya Nyaraka moja kwa moja badala ya kupitia wizarani.

Utekelezaji. Ushauri huu ni mzuri na utasaidia sana idara kutekeleza majukumu yake ya uhifadhi na uhaulishaji wa nyaraka na kumbukumbu, na kuweza kusaidia taasisi mbali mbali katika uwekaji wa kumbukumbu zake.

Aidha, wizara tutawasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu ushauri huu hasa ikizingatiwa miaka ya nyuma taasisi hii ilikuwa na voti yake.

Agizo la 19. Kamati inashauri suala liliopo sasa kwa wizara za serikali zinazotaka kuondoka na mfumo wa Nyaraka *document* na badala yake kuwa na mfumo wa *digital* kuwa zisibadilike na badalayake wawe na mifumo yote miwili, kwani mfumo wa *digital* siyo wa kuaminika sana.

Utekelezaji kwa shauri hilo. Ushauri umepokelewa na kwamba wizara za serikali zitatumia mifumo yote miwili. Aidha, wizara itaandaa Sera ya Nyaraka na kumbukumbu, ili kutoa muongozo sahihi juu ya udhalishaji na uhifadhi wa matumizi ya nyaraka na kumbukumbu.

Agizo la 20. Kamati inashauri kuitafutia usafiri Idara ya Nyaraka, ili kutekeleza kazi zake ipasavyo.

Utekelezaji. Wizara imepokea ushauri huu na juhudi za kulipatia ufumbuzi suala hili litachukuliwa katika Bajeti inayokuja 2018/2019

Agizo la 21. Kamati inaagiza suala la upimaji wa afya wa wafanyakazi wa Idara ya Nyaraka ufanyike katika muda unaostahiki. Ushauri huu ni mzuri na unafanyiwa kazi ambapo kwa sasa wafanyakazi wa Idara ya Nyaraka wanapimwa afya zao kila muda unapowadia.

Agizo la 22. Kamati inashauri serikali kulichukua suala la Kituo cha Kuhifadhia Kumbukumbu. Wizara imeshaandika andiko la mradi juu ya uwanzishwaji wa Kituo Maalum cha Kuhifadhia Kumbukumbu, ili kutafuta usaidizi wa fedha. Oneo la Koani limependekezwa na maombi yamepelekwa kuliomba eneo hilo litumike kwa shughuli hiyo.

Agizo la 23. Kamati inaagiza kupatiwa mafunzo watendaji kazi wa Idara ya Nyaraka hasa wanaohudumia chumba cha kuhifadhia nyaraka. Agizo hili limetekelezwa lipokelewa kufanyiwa kazi kwa kuandaa mpango wa mafunzo hayo kwa mujibu wa bajeti inavyoruhusu.

Aidha, rasimu ya Sera Mafunzo imeandaliwa na wizara ipotoamuongozo wa mafunzo kwa watumishi wote wa umma wakiwemo wale wanaofanya kazi katika mazingira magumu kama wale wanaohudumia chumba cha kuhifadhia nyaraka.

Agizo la 24. Kamati inasikitishwa na taarifa za ukosefu wa vitendea kazi muhimu katika Idara ya Nyaraka. Utekelezaji, andiko la mradi lilivyoandaliwa limehusisha pia upatikanaji wa vitendea kazi muhimu katika Taasisi ya Nyaraka, vina gharama kubwa kuvinunua lakini hata hivyo hasa vifaa vya uhuishaji wa nyaraka ambapo kuvipata

kwakwe kunahitaji *order* maalum kiwandani. Hata hivyo kwa kipindi hichi Julai/Septemba baadhi ya vitendea kazi muhimu vimenunuliwa ikiwemo madawa ya kuhuisha nyaraka, vipoza hewa vitatu, kwa ajili ya *(strong room), files jackets* na vifaa vyengine vinavyowezesha utendaji wa kazi kwa kuendelee na kufanya kazi zao ipasavyo.

Agizo la 25. Kamati inaagiza kuimarisha usalama katika Idara ya Nyaraka kwa kuwekewa vifaa maalum ambavyo vitatoa ishara endapo mtu atapata tatizo. Vifaa maalum vya usalama kama kamera imewekwa idara ya nyaraka, hatua zaidi za kuimarisha usalama zitachukuliwa ipasavyo kupitia ushauri wa kitaalamu.

Agizo la 26. Kamati inaagiza nyumba iliyopo ndani ya eneo la Idara ya Nyaraka inunuliwe, serikali ilifaya tathmini bei ya nyumba hiyo na taarifa zake zimeshawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua za upatikanaji wa fedha za ununuzi, ili nyumba hiyo inunuliwe na alipiwe fidia muhusika.

Agizo la 27. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua zinazofaa, suala la kutoingizwa fedha za matumizi moja kwa moja katika baadhi ya Idara Pemba.

Utekelezaji. Wizara itawasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Idara ya Bajeti kulipatia ufumbuzi suala hili. Kiutaratibu fedha zinaingizwa wizarani hugaiwa kwa mujibu wa idara ambapo Pemba hupatiwa fedha kwa mujibu wa shughuli zilizopangwa na idara husika.

Agizo la 28. Kamati inaagizwa kufanyiwa haraka uwepo wa taasisi zilizokosa ofisi huko Pemba. Wizara itashirikiana na taasisi husika juu ya uwezekano wa kufungua Ofisi Pemba. Hata hivyo, kwa huu wa fedha 2017/18 Afisi ya Mwanasheria Mkuu imepanga kufungua Ofisi yake Pemba. Afisi ambazo hadi sasa hazijafunguliwa Pemba ni Tume ya Kurekebisha Sheria, Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi na Idara ya Serikali Mtandao.

Hitimisho.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kukumbusha kuwa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayo dhima ya kuhakikisha kuwa masuala yanayohusu ufikishwaji wa huduma kwa wananchi pamoja na upatikanaji wa haki zao kwa wakati yanasimamiwa ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kuihakikishia Kamati ya Baraza lako Tukufu kwamba maagizo, maelekezo na ushauri unaotolewa utaendelea kufanyiwa kazi kwa ustawi wa taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba Waheshimiwa Wajumbe waipitie taarifa hii kwa kina, na hatimaye watoe michango yao kwa lengo la kuifanyia iwe bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora nakushukuru sana, sasa tumkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum Kuhusu Utekeelzaji wa Maagizo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai pamoja na afya njema, ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu tayari kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kiujumla. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.
Mhe. Naibu Spika, napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako, Mhe Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Vile vile, pongezi za pekee ziende kwa Uongozi mzima wa Wizara hii kwa juhudi zao kubwa na mashirikiano wanayotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu. Kamati inawataka wazidi kutekeleza na kusimamia majukumu yao kwa ubora na ufanisi zaidi ili kufikia hatua iliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yetu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu. (*Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Nadir Abdul–latif Yussuf	Mjumbe
4.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5.	Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
6.	Mhe. Ali Khamis Bakari	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
8.	Nd. Ali Alawy Ali	Katibu
9.	Nd. Haji Jecha Salum	Katibu

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imetoa fursa ya lazima kwa kila Kamati kutayarisha ripoti ya mwaka itakayowasilishwa katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kila mwaka.

Mhe. Naibu Spika, aidha, Kanuni ya 108(15) ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa maagizo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati kwa kutumia Kanuni ya 106(3) imepewa jukumu la Kufuatilia Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotanguali, ambapo kazi ilifanywa vyema katika kipindi kilichopita, na bado Kamati inazidi kufuatilia utekelezaji wa maagizo hayo kila inapoona inafaa.

Mhe. Naibu Spika, ripoti hiyo hujumuisha ushauri na maagizo ya Kamati kwa wizara na Taasisi zake inazozifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inazifanyia kazi wizara mbili (2) ambazo ni:

(a) Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na

(b) Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, hotuba hii inaelezea utekelezaji wa maagizo kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Utekelezaji wa Maagizo:

Mhe. Naibu Spika, jumla ya maagizo 87 yaliagizwa na Kamati katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, kamati imefarijika sana na inatoa shukurani zake za dhati kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa jinsi walivyoweza kutekeleza vyema maagizo hayo hali inayoonesha ukomavu mkubwa katika utekelezaji wake pamoja na jitihada njema za kuleta maendeleo nchini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, licha ya wizara kutekeleza vyema maagizo yaliyotolewa na kamati, kuna wastani wa maagizo kumi (10) ambayo kamati imeona ni vyema kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, kamati imeitaka wizara kufuatilia zaidi utekelezaji wa maagizo kwa kutoa maelekezo yafuatayo:

(a) Kamati inashauri vifungu vya fedha vya kuhifadhi Nyaraka vilivyopo serikalini viwe vinaingizwa Idara ya Nyaraka. Wizara ifuatilie utekelezaji wa agizo hili na kuandika upya majibu yake kama ilivyoaigizwa.

(b) Kamati inaagiza kupatiwa mafunzo watendaji wa Idara ya Nyaraka hasa wanaohudumia chumba cha kuhifadhia nyaraka *(strong room).* Kamati imeitaka wizara ieleze kwa usahihi hali halisi ilivyo hivi sasa kuhusiana na agizo hili.

(c) Kamati inasikitishwa na taarifa ya ukosefu wa vitendea kazi muhimu katika Idara ya Nyaraka. Kamati imeitaka wizara kuorodhesha vitendea kazi vilivyopatikana hadi sasa badala ya kueleza kuwa vifaa mbali mbali vimenunuliwa.

(d) Kamati inaiagiza kufanyiwa haraka uwepo wa taasisi zilizokosa ofisi kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kamati imeitaka wizara kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kwamba ofisi zote zilizo chini ya wizara hii ambazo hazijafungua Ofisi Pemba, zifungue, ili wananchi waweze kupata huduma hizo kwa haraka na kwa wakati.

Aidha, Kamati inashauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuandaa utaratibu maalum wa kuifanyia ukaguzi miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa Fedha za Mfuko wa Jimbo ili ukaguzi wa fedha hizo ufanyike kila mwaka na kwa wakati husika ambao fedha hizo zimetolewa.

(e) Kamati inaishauri wizara kufanya jitihada za makusudi kujenga Mahakama ya Mfenesini, Wete, Konde na Kengeja.

Mhe. Naibu Spika, kamati ilitaka wizara kuzifanyia ukarabati mahakama hizo ingawa kamati imeelezwa kuwa kwa sasa kipaumbele cha wizara ni kujenga Mahakama Mpya ya kisasa Tunguu pamoja na kuifanyia marekebisho Mahakama ya Mwanakwerekwe ambayo utekelzaji wake unaendelea.

(f) Kamati imeona ipo haja ya kuwepo kwa kifungu maalum cha kuwalipa mashahidi.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelzaji wa agizo hili, kamati imeelezwa kuwa Mahakama inafanya jitihada za kuwalipa mashahidi ila tatizo linajitokeza kutokana na ufinyu wa bajeti kwa fedha za matumizi mengineyo (*OC*) ambako hupelekea mashahidi kuchelewa kulipwa stahiki zao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, aidha, Kamati ilitoa msisitizo katika utekelezaji wa maagizo yafuatayo:-

(a) Kamati inaiagiza wizara kuchukua hatua kwa Ofisi ya Mufti kupatiwa fungu lake na kuongezewa bajeti.

Mhe. Naibu Spika; Kamati inasisitiza kuendelezwa kwa juhudi za kuipatia fungu lake wenyewe na kuiongezea bajeti Ofisi ya Mufti Zanzibar, ili iweze kutekeleza vyema majukumu yake.

(b) Kamati inaishauri serikali kutilia mkazo suala la Sheria ya Ndoa ya Kiislamu, ambapo hadi sasa haipo na ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kamati inatoa msisitizo kwa wizara kuhakikisha wanaishajihisha jamii kutoa elimu ya ndoa kabla ya kufungwa kwa ndoa ili kuepuka tatizo la wingi wa talaka. Aidha, kamati imeelezwa kuwa Mswada wa Sheria ya Ndoa upo katika hatua za mwisho kukamilika na umeweka kifungu cha mafunzo ambacho kitapelekea wanandoa kujifunza kabla ya kufunga ndoa.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaagiza wizara kuchukua hatua kwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuharakisha kupatiwa fungu lao. Kwa kuwa, Tume ya Maadili wa Viongozi wa Umma ni Taasisi nyeti na inatakiwa ifanye kazi zake kwa uhuru, hivyo ni vyema kuwa na fungu lao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kamati inatoa pongezi kwa wizara juu ya utekelezaji wa maagizo yafuatayo:-

(a) Kamati iliagiza kuchukuliwa hatua za haraka za kuajiri waendesha mashtaka na wafanyakazi wengine kwa upande wa Pemba.

Kamati inatoa pongezi kwa wizara kwa kutekeleza agizo hili kwa kiasi kikubwa ambapo imeweza kuajiri waendesha mashtaka 13.

(b) Kamati inashauri kuchukuliwa hatua na kulifanyia kazi suala la maslahi kwa wafanyakazi wa chini ambao ni kidogo.

Kamati inatoa pongezi za dhati kwa serikali kwa kutimiza ahadi yake ya kuongeza mshahara wa kima cha chini hali inayopelekea kupunguza ugumu wa maisha kwa wafanyakazi hao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii tena kuishukuru wizara kwa mashirikiano yake inayoipa kamati katika kutekeleza majukumu yake na pia niombe kuzidisha mashirikiano hayo ili kuweza kufikia lengo la serikali kuleta katika maendeleo nchini.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Makamo Mwenyekiti, wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. Waheshimiwa Wajumbe sasa tunaanza na mchango, nimepata wachangiaji watano (5) nitaanza na Mhe. Ali Suleiman Ali, atafuata Mhe. Omar Seif Abeid na baada ya hapo nitampa Mhe. Nadir Abul-latif Yussuf.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wa taasisi zote za wizara hii kwa kazi nzito wanazofanya, hasa tukiangalia kwamba wizara hii ina mambo mengi ambayo yanahitajika wananchi kupata haki zao pale wanapopata matatizo hapa na pale.

Lakini Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze Kamati yetu chini ya Mwenyekiti wake pamoja na wajumbe wake wote kwa kufanya kazi nzuri na maagizo aliyoyatoa yanastahiki vigezo ya kuhakikisha kwamba kuna mambo ambayo yarekebishwe, ili maendeleo yapatikane katika shughuli zetu za kila siku.

Mhe. Naibu Spika, katika mchango wangu nitakuwa na mambo machache kama ifutavyo ukurasa wa 12 agizo la 11, naomba ninukuu kama ilivyo Mhe. Naibu Spika.

> "Kamati imeona ni busara kuwepo na kifungu maalum cha kuwalipa mashahidi angalau fedha za nauli, ili kuwashajihisha kujua umuhimu wa kutoa ushahidi mahakamani"

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wangu hili napongeza, lakini pia ningeongeza tu kwamba hii si angau iseme tu moja kwa moja kuwalipa haki zao za msingi kwa wale wanaokuja kuja kutoa ushahidi ili watu wapate changamoto kuja mara kwa mara katika kutowa ushahidi, maana kuna stahiki maalum ambao hulipwa kwa hivyo angalau apate nauli unamvunja nguvu mtoa ushahidi.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika nikubali tu kwamba tunayo matatizo mengi wananchi wetu hawaelewi, na njia moja inabidi wananchi waelewe ni taaluma naipoingeza wizara kupitia chombo hiki kwamba inatoa taaluma mbali mbali lakini taaluma ni muhimu ili mwananchi ajuwe haki yake ya kutoa ushahidi pindi linapotokezea tatizo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu naomba nizungumza hapa kwa ufupi ukurusa wa 15 agizo la 20 naomba nikuu Mhe. Naibu Spika, kama lilivyo. Agizo la 20 linasema:

> "Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua wale wote wanaofumbia mambo vitendo vya udhalilishaji kumalizana wenyewe kwa wenyewe na kutuma maombi ya kesi kufutwa".

Mhe. Naibu Spika, hili ni agizo muhimu na tumeambiwa kwamba katika utekelezaji wizara kupitia Ofisi inayohusika Mkurugenzi wa Mashtaka inaendelea kuelimisha jamii, ijuwe tu kwamba panapotokea tendo la uwovu lolote lile udhalilishaji hasa kwenye vijana wetu ambao wanadhalilishwa siku hadi siku hili lisifumbiwe macho. Mhe. Naibu Spika, nashauri sana kupitia Ofisi ya Mkurugenzi Mashataka ifanye kazi zake ipasavyo na kutoa taalu mbali mbali, ili wananchi waelewe faida na hasara yake.

Mwenyezi Mungu tuepueshie mbali hali mbaya inatokea katika nchi yetu siku hadi siku, lakini mara nyingi utasikia mambo wamemalizana wenyewe huko huko mitaani. Kwa

hivyo, niombe tu kwamba hili lichukuliwe hatua, ili lisiendelee na kuleta athari kwa jamii yetu.

Mhe. Naibu Spika, vijana wetu tunaamini kwamba wanapata madhara makubwa na wanapata hali mbaya baadaye ya maisha kutokana na kadhia hii inayotokea.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, nije ukurasa wa 16 kifungu cha 23 naomba ninukuu Mhe. Naibu Spika, usione tabu.

> "Kamati inashauri Ofisi ya Mufti kuwa na mashirikiano na Ofisi ya *DPP* katika kesi za walimu wa Madrasa, ili kuweza kujua na kupata taarifa juu ya kesi hizo"

Naomba niendelee utekelezaji unasema, ushauri umepokelewa na Ofisi ya Mufti inashirikiana kikamilifu kikamilifu na Ofisi ya *DPP* pamoja na Jeshi la Polisi kupata takwimu sahihi za walimu wa madrasa wanaotuhumiwa kushtakiwa kwa kesi za udhalilishaji dhidi ya watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Ofisi ya Mufti kupitia vyombo mbali mbali ikiwa vya ibada au wapi na kwengineko au makongamano izidishe bidii kutoa taaluma hii, tunaamini kwamba nia njema kwa mzazi mtoto wake kumpeleka Madrasa akapate elimu ya kesho tunakokwenda duniani na akhera, kwa sababau ukisoma vizuri katika elimu ya dini pande zote mbili unafaidika, duniani utajua vipi vya kuishi na kesho akhera utapokea thawabu zake. Hivyo, naomba tuongeze bidii hizi na mashirikiano yaongezwe zaidi, ili tuhakikishe kwamba tatizo hili linaondoka na wala halitokei tena katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa kweli, tunaamini kwamba walimu wote ikiwa wa shuleni au madrasa, madrasa ndio wamepewa kipaumbele waongoza jamii elimu ya dini duniani na akhera kesho, lakini wao ni wengi kwa bahati mbaya baadhi yao ndio wadhalilishaji wakubwa. Kwa hivyo, ninaomba tu sheria au taaluma ifanywe na wanaopatikana na hatia achukuliwe hatua, ili kulikomesha tatizo hili lisiendelee kwa sababu mzazi anapoondoka mtoto wake na kwenda kwenye madrasa fulani, anamini anakwenda kwenye salama, lakini kumbe anakwenda kwenye maeneo ya hatari.

Hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba tuwaombe sana walimu wetu wa madrasa baadhi yao wajielewe wanalolifanya, kwa sababu wanategemewa na wanapotegemewa na wao wajiamini kwamba wanategemewa kwa maslahi ya watoto wa watu.

Mhe. Naibu Spika, jengine ukurusa wa 19 agizo la 31 Mhe. Naibu Spika kamati inasisitiza kuwepo kwa mashirikiano kati ya Ofisi ya *DDP*, Polisi, Mahakama na Jamii katika kueleta ufanisi wa uendeshaji wa kesi. Kwa kweli, ndio ni yale yale kwamba taaluma itolewe, taaluma iwaelekeze jamii, ili wafanye kazi zao vizuri lakini naamini kwamba haya yote Mhe. Naibu Spika yakipata mashirikiano haya tunayolalamikia yote yataondoka.

Lakini la mwisho Mhe. Naibu Spika, katika kamati wametoa taarifa katika kueleza taarifa yao wamesema kama ifuatavyo ujenzi wa Mahakama ya kisasa Tunguu unaendelea katika maandalizi mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, naipongeze sana wizara hasa tukiangalia kwamba wakati wa sasa hivi umekua na mji wetu mkuu unaelekea Tunguu mji wa pili. Kwa hivyo, ujenzi huu utaleta nafasi nzuri ya wenzetu mahakimu na majaji kufanya kazi zao vizuri, na katika mazingira ya salama zaidi na tukizingatia kwamba mahakama yetu ipo au zipo lakini ufinyu vile vile upo.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kabisa naunga mkono hotuba hii au taarifa hii ya Kamati kupitia Wizara ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora naunga mkono kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Omar Seif Abeid ajitayarishe Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf atuatiya Mhe. Masoud Abrahman Masoud

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ambayo Mhe. Waziri ameiwasilisha vizuri sana. Awali ya yote napenda kuchukuwa nafasi hii kumpongeza kwa uwasilishaji wake lakini pia nachukua hii nafasi kuipongeza sana kamati. Kwa kweli, Kamati imefanya kazi nzuri sana imetoa ushirkiano wa hali ya juu, imeonesha umahiri wake, imeeleza zile sehemu ambazo ni changamoto, hivyo kamati naipongeza sana hasa, kwa sababu kadiri unavyoisoma utaona kwamba kitabu hiki Kamati wametoa miongozo, ambayo inasaidia. *(Makofi)*

Lakini, katika mchango wangu nataka niende kidogo nianze kwenye *page* ya 4 inayozungumizia Agizo la 5. Kamati inashauri tume ya maadili kuwapatiwa wafanyakazi wake, kwani waliopo wameazimwa pia mazingira ya ofisi hayaridhishi kutokana na uchakavu wa jengo. Aidha kamati imeagiza kuongezwa wafanyakazi wa tume kwa Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ukitizama mantiki ya hii ya hili agizo, ni agizo la kitaalamu Tume ya Maadili ndiyo inayowasimamia viongozi, yaani viongozi wote wako chini wanatizamwa na maadili haya ya tume hii. Lakini ni jambo la kusikitishwa kwenye tume kwamba kuna uchakavu wa majengo. Kwa kweli, na mimi naungana na kamati kupeleka kilio changu, hivi ni kwa sababu gani iliyofanya mpaka leo ikawa hatujawekea sawa hawa, na bidii au juhudi gani za makusudi zinachukuliwa juu ya kuwapatia hawa jengo linaloendana na hadhi yao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hawa wanatutizama sisi viongozi, sisi tukikosea kuvaa tai hawa watutizame sasa ikiwa wao tunawaona wanafunga tai upande sisi watatukosoa vipi. Mhe. Naibu Spika, naomba wizara katika mambo yote Tume ya Maadili ya Utumishi itizamwe vizuri ipewe stahiki kama ilivyo, wapewe vitendea kazi, waongezwe wafanyakazi na kwa nini tuwe na wafanyakazi wa kuazima wakati wizara ni ile ile inashughulika na watumishi na yeye ndiye anayewahamisha na kuwaweka. Sasa iweje mpaka leo hawajahamishwa kutoka kitengo kile kwenda chengine, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri

ndiye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naona suala la kuwathibitisha kutoka taasisi zilizoazimwa kutoka kule kwenye taasisi zao, lisichukuwe tena muda, isipokuwa lifanywe haraka sambamba na ukarabati wa jengo. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na maombi ya kamati, kwamba hili ni jambo si la kuchekewesha tena ni lakuchukuliwa hatua haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukienda *page* ya 5 tunaona kuna agizo la kupatiwa vitendea kazi. Wizara inapanga bajeti kwenye taasisi zake, sasa leo tukisema kwamba taasisi ipange bajeti ya matumizi ya kununua vifaa au vitu vya usafiri, ina maana lazima wapunguze wamege kutoka huku waingize upande mwengine, kama watafanya hivyo lile lengo lao walilolikusudia je linafikiwa, kama halikufikiwa si unaona tutakuja kuwauliza tena kwa mara ya pili hapa kwamba mwaka jana tuliwapa pesa mkashindwa kufanya hili. Kwa hivyo, naomba sasa kama haitawezekana kwa mara hii bora tuseme kwa mara hii haiwezekani, lakini mwaka ujao iingizwe kwenye bajeti kubwa bajeti kuu ya wizara, ili tatizo hili liweze kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, tukienda kwenye ukurasa wa 6 kamati imeshauri suala la usafiri lipewe kipaumbele kwa agizo la 10 utekelezaji lakini hilo. Mhe. Naibu Spika, tuliache twende kwenye *page* ya 10 kabla ya kurudi ya 8 kwasababu nilitaka hili lisije likanipita kutokana na muda.

Mhe. Naibu Spika, mimi niko pale Konde mbele yangu au ndio ilipo Mahakama ya Konde. Mahakama ya Konde ina choo kimoja, ambacho kinatumiwa na wafanyakazi leo pale wafanyakazi wetu wakitoka pale kama kunanyesha mvua na ikiwa hakuna mwamvuli wanakwenda mbio kwa ajili ya kuingia kwenye choo si jambo la kupendeza. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naomba pamoja na kutoa ushauri kwamba wizara ifanye itakavyo wezekana iwapatiwe vyoo, na choo chenyewe ni kimoja wanawake na wanaume. Kwa hiyo, naomba kwamba ifanye itakavyowezekana lakini vijengwe vyoo kimoja kikiwa cha wanawake kimoja cha wanaume.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Omar Seif Abeid zungumza na mimi nielekee mimi.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, sawa. Hivyo, naomba pale vijengwe vyoo viwili kimoja cha wanawake, kimoja cha wanaume, ili kuweka sasa kama maeneo mengine yalivyokuwa yanaelekeza hiki cha wanawake hiki cha wanaume na pale kwenye ile mahakama naomba iwe hivyo hivyo. Sambamba na ukarabati wa lile jengo lenyewe zima, kwa sababu lile jengo la Konde lina tatizo la mchwa, ambapo wanapenda kulishambulia sana lile jengo kila wakati linafanyiwa ukarabati na dari inaanguka. Kwa hiyo, naomba kwamba wizara ijitahidi kulijenga jengo lile na itumie *material* ambayo itaweza kukimbiza mchwa wasiweze kuishambulia kwa muda wa haraka haraka.

Vile vile, Makahama ya Mwanakwerekwe tumeona hapa Mahakama ya Mwanakwerekwe KMKM walipewa shilingi milioni 131,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa

hiyo Mahakama ya Mwanakwerekwe. Mhe. Naibu Spika, naomba nijuilishwe ni lini hawa KMKM wamepewa hizi pesa, maana yake KMKM ninavyowahamu ukiwapa kazi wanafanya haraka. Lakini leo tumeambiwa leo wamepewa na bado hili jengo halijamalizika sijui kuna nini, labda tupate jibu ni kitu gani kilichosabisha ikiwa mpaka leo haijapata kumalizwa ile Mahakama ya Mwanakwerekwe ikatumika kama ilivyokudiwa. *(Makofi)*

Lakini pia kulikuwa na agizo la 11. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naangalia kipengele kinachohusiana na *ZAECA* nimeona kwamba na wao wana upungufu wa jengo hawana ofisi, yaani taasisi nyingi ambazo ziko chini ya wizara hazina ofisi. Kwa hiyo, naishauri wizara na wala tusishauri idara kwamba zipange bajeti yake, ambazo zimeshapewa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hii itakuja kuiathiri taasisi yenyewe, itabidi ipunguze fungu kama nilivyosema ipeleke kwengine matokeo yake lile lengo lilokusudiwa halitofikiwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu kwamba wizara ndio kama nikumega wamege wao wizara kwenye fungu langu la wizara, wazipe taasisi zinunue vyombo vya usafiri na mambo mengine ambayo yana umuhimu, lakini bajeti za taasisi zinakuwa ni ndogo. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa hili naomba sana kwamba Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndiyo kioo kinachotakiwa kifanye mambo mazuri na Mwalimu Haroun Ali Suleiman, ambaye ni Mhe. Waziri tunakupongeza yeye ni mzee mwalimu wetu umetusomesha amefaahamu. Kwa maana hiyo, wizara nayo inatakiwa iwe kigezo kizuri kama yeye mwenyewe anayoiongoza wafuate maadili pamoja na maagizo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda mchango wangu ni mdogo ambao sikutaka niingie sana. Baada ya haya nasema naunga mkono asilimia tisini na tisa nikipewa majibu nitamalizia hiyo moja sina tatizo, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf atafuata baada ya hapo Mhe. Masoud Abrahman Masoud ajitayarishe Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bissimillah Rahman Rahim* Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana jembe letu tunakuamini kwa kunipatia nafasi, na kwa kuwa mimi ni mjumbe wa kamati wa wizara hii na nilikuwa sipo nitachangia machache, ambayo itakuwa kama ni mawazo au fikra.

Jambo la mwanzo nitaanza kuzungumizia Kitengo cha Rushwa na Uhujumu Uchumi. Mhe. Naibu Spika, kitengo hiki ni kitengo muhimu sana lakini ningeomba sana wizara kwa kuwa mimi ni mjumbe wa kamati hii watizamwe vizuri sana kwenye suala la ulinzi. Vile vile kwenye suala muhimu la kupatiwa mfuko maalum wa kupewa fedha kitengo kile wanapohitaji *information* kutoka kwa watu fulani, ili kuweza kutekeleza kazi zao. Hawana Mfuko madhubuti kabisa wa kuweza kumlaghai mtu au kwenda kumu-*offer* kwamba tutakupa kiasi fulani tupatie *information* ili mambo yao yaende vizuri, yaani wanafanya kazi katika wakati mgumu na kazi zao zinakuwa ngumu sana, na hasa kwenye

suala la ulinzi kutokana na kazi yao hatarishi, hawako vizuri kwenye vifaa vya ulinzi hawajapewa.

Mhe. Naibu Spika, naiomba wizara na najaribu kuzungumza mambo haya pole pole, kwa sababu mimi ni mjumbe wa kamati hii, najaribu kufahamisha na kuomba haya mambo yaangaliwe, ili yaende vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningekwenda kwenye suala la Mwanasheria Mkuu, aliwahi kuniahidi kwamba ataleta Mswada wa Sheria wa Wabakaji, Majambazi, Waletaji Unga, Wauzaji, pamoja na Mashoga, jinsia moja amesema ataleta kwenye ukumbi huu ameniahidi, nitaomba aje anieleze lini anauleta ili tuupitishe au tuujadili, kama haukuja huu kutokana na ahadi yake mwenyewe nitamtilia shaka Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala hili ni muhimu kwa sababu taifa linaangamia. Zanzibar suala la ubakaji linajulikana dunia nzima sasa hivi kwamba Zanzibar kutokana na nchi ndogo, *population* ndogo lakini ubakaji ni mkubwa. Vile vile, Zanzibar ni kitovu cha madawa ya kulevya katika sehemu tofauti za *East Africa* na sehemu nyengine, *transit* ziko hapa, usambazaji uko hapa. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ahadi yake mwenyewe aulete mswada huu haraka iwezekanavyo Waheshimiwa Wawakilishi tuujadili na tuupitishe na wale Waheshimiwa Wawakilishi wasioupitisha au kuupinga mswada huu na wale nitawatilia shaka na tutawajua kwamba wanashiriki kwenye masuala haya.

Vile vile, twende kwenye suala jengine ambalo limetokezea karibuni. Nazungumza hivi kwa sababu vitu vina mfano ndani ya nchi yetu. Juzi Hoteli ya Mazsons mjini Shangani, ambayo inafanyika sana mikutano, wamekamatwa mashoga 20 wa kiume. Mashoga wale wamekutikana ndani wakipewa mafunzo maalumu ya kujitetea haki zao pamoja na kushindana na serikali kudai haki zao kuleta ushoga ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ushahidi uko dhahiri asilimia 99.8 ndani ya nchi hii ni Waislamu, ambapo dini yetu inapinga kikamilifu mashoga na mambo ya jinsia moja. Mhe. Naibu Spika, naamini Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein, Mwanasheria Mkuu mswada huu watauleta atasaini Mhe. Rais wa Zanzibar kwa imani yake na sisi tutaupitisha, ili watu wote tuliowataja wanyongwe mambo haya yapungue au yaondoke katika nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nampongeze sana Kamanda wa Polisi wa hapa mjini, Mhe. Hassan Nassir pamoja na Mahakama na watu wote walioweza kushiriki kuwakamata mashoga wale na kuwafunga ikiwezekana wawanyonge huko huko jela.

Mhe. Naibu Spika, suala langu jengine nampongeza sana Mhe. Jaji Mkuu kutembelea mahabusu na sehemu nyenginezo kwenda kujionea hali halisi. Sisi tumepita baadhi ya sehemu lakini nyengine hatujafika, kwa kweli ni kazi nzito, ni kazi ngumu na haya maagizo waliyowapa Mahakimu kwamba waweze kuwapa dhamana na wengine kuwatafutia njia nyengine za wepesi kabisa, kutafuta kesi za mambo ya mifugo na nyengine kwa njia ya haraka ni jambo zuri sana.

Kwa kweli, waliowekwa ndani wengi kesi zao ni ndogo, wanadhulumika ndani bila ya sababu ya msingi, kwa sababu ukiangalia vitu vyengine wengi unakuta matatizo waliyowekewa ndani wamezuliwa hawajafanya, wengine ukiangalia kesi zao kaiba kuku, nazi, watu wamewekwa ndani. Mhe. Naibu Spika, naomba Mahakimu na Majaji tunawaamini ,watu wa namna hii kesi zao ikiwezekana wawasamehe watapofanya tena watafute kesi ngumu, lakini mtu kufungwa miezi sita au saba kwa sababu ya mkungu wa ndizi na mengineyo, inakuwa sio jambo la busara.

Mhe. Naibu Spika, napongeza sana kwenye mahakama hasa Jaji Mkuu kwa kuona katekeleza suala hili kwa upande wake. Lakini pia ningeomba Afisi ya Mufti Mkuu kwamba walimu wa vyuo, walimu wa skuli, wanaoharibu watoto wa kiume na wa kike na wamekiri wenyewe. Mufti Mkuu amekiri kwamba kuna walimu wa madrasa wapo wanaoharibu watoto wa kiume kwa mpango mkubwa kabisa kuwa wengi wapo. Ningeomba sana walimu hawa waliokuwa na uhakika nao na waliokuwa hawana uhakika nao wafanyiwe uchunguzi tena waweze kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria na wao ndio wawe mashahidi wa mambo yale yanayofanyika usaliti kwa watoto. Watoto wanapelekwa kwenda kusoma dini lakini imani imekuwa hamna walimu wengine wa vyuo sio wote wamekuwa hawana maadili wanaharibu watoto.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naomba Ofisi ya Mufti Mkuu sijui kama hili suala linawahusu au vipi, tumeona nchi nyingi watu wanafanya maandamano ya kupinga Waislamu kuuliwa, jambo la kushangaza nchi yetu Waislamu wanauliwa kila nchi kama Myanmar, Iraq, Syria na nchi tofauti. Myanmar juzi wameuliwa Waisilamu na Nabudis watu wanafanya maandamano Waislamu nashangaa kwamba nchi hii imekaa kimya hakuna Muislamu hata mmoja aliyefanya maandamano kupinga mauaji ya Waislamu wenzetu.

Jambo hili linasikitisha sana na jambo kama hili lilitakiwa Ofisi ya Mufti Mkuu wao ndio waandae maandamano haya *official* kwa kibali chao wenyewe watu waandamane waweze kupinga wanaowaua Waislamu. Hivyo, naomba sana Waislamu wa nchi nzima yanapotokezea mambo kama haya Waislamu wenzetu wanauliwa, basi tufanye maandamano ya kibali ya sheria ili tuweze kupinga kama wanavyopinga wenzetu ni aibu kukuta nchi za kikafiri wanapinga masuala haya, sisi Waislamu kwenye nchi hii tumekaa kimya ni aibu sana.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda mbio mbio kwa sababu niwahi muda wangu na hii kama nilivyoeleza mimi ni mjumbe wa kamati. Sasa niende kwenye Mahakama. Naomba sana Majaji, Mahakimu wanapopelekewa kesi za *traffic* waziangalie, kwa sababu wananchi wengi wanaohukumiwa na kesi za polisi wa *traffic* baadhi yao siwaaminifu, wanawasingizia kesi raia huko nje kesi ambazo hazina maana wanawapeleka Mahakamani na imekuwa kigezo kikubwa kitu kidogo nakupiga faini, nakuandikisha karatasi ya mahakama utakwenda kujibu mahakamani wakati hili suala wakati mwengine inakuwa hawana makosa.

Mfano mdogo Kaskazini Unguja, polisi wanakaa na vitochi vya *speed limit* wakati barabara zetu Zanzibar hazina *speed limit sign bord* hazioneshi upite *speed* ngapi halafu wao wanawapiga kamera na kuwalipisha faini au mtu wanampeleka mahakamani.

Kusema kweli kama nchi inafuata sheria ule ni unyanyasaji na naomba mahakama kesi zile wazikatae kwa sababu barabara zenyewe hazina mabango ya *speed limit*, na kwa mujibu wa sheria huwezi kumkamata mtu kama kitu *sign* haipo na mtindo huu upo Kaskazini 'A' zaidi, ukiacha na kesi nyengine ambazo *traffic* wanazifanya kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mfano mwengine njiani sasa hivi zinauzwa *road license, insurance* unasimamishwa unaambiwa *road license fake, insurance fake*. Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango kupitia *ZRB* imepiga watu faini 50,000 Kituo cha Polisi Madema au wengine wamewafunga kabisa waliokuwa hawana uwezo. Mhe. Naibu Spika kwa kweli Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora suala lile wamewanyanyasa sana raia wa Zanzibar na raia wengine kuwapiga faini na kuwakamata kwa makosa ambayo wao wenyewe hawayatambui.

Kutokana na hali hiyo, mwananchi gani ataweza kutambua *road license* na *insurance fake* wakati serikali yenyewe imeshindwa kutambua mwanzo mpaka baada ya miaka ndio imekuja kujua, vile vitu ni vya *computerize* haviwezi kugundulikana mpaka kwa vifaa maalum. Mhe. Naibu Spika, naomba sana kama nchi tunafuata sheria basi vitu kama vile walikuwa wakawakamate waliofanya vile vitu na sio raia ambao wamenunua *insurance* na *road license,* kwa sababu hawakuzipata bure. Suala hili tunaomba sana vile vile mahakimu wanapopelekewa kesi kama hizi wazitafiti, waziangalie na wasiwashtaki watu kwa sababu ya makosa ambayo hayafahamiki.

Mhe. Naibu Spika, jambo langu la mwisho ni la *CAG*. *CAG* ni kitengo, idara au taasisi muhimu sana ya nchi hii, kusema kweli tuje tupate jibu hii *CAG* inahusiana na wizara ipi. Kwa kweli, kipindi cha nyuma kwenye vikao vyetu walikuwa hawahudhurii tunaambiwa hawa wanahusika na *PAC*, wakati sisi Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma ndio wapo chini *CAG* ndani wamo. Hivyo, napenda kufahamu *CAG* hasa wanahusika wapi hata kwenye vikao vyetu huwa hawaji. Nasikia kikao cha hivi juzi mimi nilipokuwa sipo walihudhuria, lakini walihudhuria sijui kwa sababu zipi, vikao vya nyuma vyote walikuwa hawapiti na wala hakuna taarifa inayotolewa. *(Makofi)*

Vile vile, hawa *CAG* tungependa kujua zile taasisi ambazo hawajazipitia mpaka leo mfano Shirika la Meli na mashirika mengine hawajayafanyia mahesabu na uchunguzi na ripoti hazijaja. Kwa hivyo, tunataka kujua matatizo ni yepi, sababu ni zipi ambazo zinawapelekea mpaka leo kufanya *surveillance* au kuangalia *accountability* za mahesabu yao kuweza kutuletea tukajadili.

Mhe. Naibu Spika, pia tungeomba *CAG* wapatiwe kanuni na vitu ambavyo viko *very strong* kwao wao kuweza kufanya kazi bila ya kubughudhiwa. Kwa kweli, wao kazi yao ni kukamata wahujumu uchumi, kuchunguza mahesabu na ukiangalia kama kanuni zao ziko nyepesi na mambo mepesi hawatoweza kufanya haki itavyotakiwa. Mhe. Naibu Spika, tunafahamu ndani ya nchi kuna mambo mengi yanafanyika, kuna viongozi wakubwa pengine wanafanya na kama *CAG* kanuni zao ziko nyepesi wataogopa kuja kufanya na kuweka mambo hadharani.

Kwa maana hiyo, tunaomba sana *CAG* watapofanya mambo yao ya mahesabu walete kinagaubaga wasimuogope mtu yeyote ndani ya nchi hii, kwa sababu nchi hii

inaendeshwa na sheria na Mhe. Rais mwenyewe ameahidi yeyote ambaye atakuwa amefanya kosa aelezwe, aambiwe. Hivyo, naomba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (*CAG)* atuletee ripoti zenye usahihi kabisa zitazohusu madudu yote ya nchi hii, ili tusafishe serikali yetu pamoja na Chama cha Mapinduzi, ili watu wachache wanaosababisha mambo haya tuwafukuze kabla ya muda kumaliza mwaka 2020. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na ripoti hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja kwa sababu mimi ni mjumbe wa kamati ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ingawa mengine najua hutajibiwa leo, lakini naamini majibu yake utayapata kwa sababu leo tunazungumzia ripoti ya utekelezaji. Kwa hivyo, mengine naamini kwamba serikali imeyasikia na basi itaweza kuyafanyia kazi. Sasa mchangiaji wetu anayefuata mwengine ni Mhe. Masoud Abrahman Masoud na atafuata Mhe. Shehe Hamad Mattar. Mhe. Masoud Abrahman Masoud karibu.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii kusimama hapa nikiwa mzima kabisa, lakini nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichangie Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyotusomea tarifa zake vizuri kabisa, lakini pia niwapongeze na watendaji wake jinsi walivyokaa kwa pamoja na wakaweza kutuletea taarifa hii kikamilifu.

Mhe. Naibu Spika, nitachangia mambo mawili matatu na hasa la kwanza ni hili Agizo la 3 la kamati ilioagiza kufanyiwa kazi suala zima la udhalilishaji. Kwanza nimpongeze Mhe. Mkurugenzi wa Mashtaka kwa jinsi alivyofanya kazi zake vizuri na utekelezaji wake hapa unaonesha suala zima la udhalilishaji sasa hivi limedhibitiwa na limewekewa mkakati maalum na kwa sasa kesi zinakwenda vizuri. Lakini, nimuomba kiongozi wa Jeshi la Polisi na yeye aongeze bidii, ili kuwapa imani wananchi wetu kwa sababu sasa hivi imani inaanza kuondoka polisi na baadaye na mahakimu na wao wanaondoshewa imani kwa wananchi, lakini msimamo uliopangwa sasa hivi na serikali wananchi wamepata imani kubwa zaidi na tuwapongeze na waendelee na mkakati huo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Agizo la 4. Kamati imebaini kuwepo kwa idadi kubwa rumande kwa wanafunzi na wananchi walioiwekwa rumande. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli suala hili limekuwa ni zito kidogo, kwa sababu inaonesha walioko rumande ni wengi kuliko waliokwishahukumiwa.

Mhe. Naibu Spika, wiki iliyopita nilikwenda Kituo cha Polisi Mwera, kuna wananchi wangu pale wako rumande waliniomba niende nikawaona, lakini sasa hivi wana mwezi wa nne wako pale rumande. Kwa kweli, inasikitisha afya zao zimekuwa dhaifu,

nilipouliza pale nikaambiwa faili lao tayari lishapelekwa kwa *DPP* lakini lina miezi minne halijafika, polisi halipo kwa *DPP* halipo wao wanaendelea kubakia rumande hali ya kuwa wale wote wana familia zao zinawategemea. Wao wenyewe sasa hivi afya zao sio nzuri.

Kutokana na hali hiyo, naomba polisi lakini pia Ofisi ya *DPP*, sina uhakika mimi sio mwanasheria, lakini kukaa pale miezi minne sijui kwa sheria gani, polisi ana masaa ambayo anatakiwa mwananchi amuweke rumande lakini sasa hivi pale wana miezi minne hali zao sio nzuri, afya zao si nzuri pia na familia zao hazina watu wa kuwahudumia.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Shehia ya Kizimbani walikuwa wanachangishana fedha kwa ajili ya kuwapatia chakula wale walioko kule, lakini sasa hivi mpaka wao wananchi nao wameshachoka familia zetu za kimasikini tumewapa mzigo mkubwa. Kwa hiyo, naiomba serikali iandae utaratibu wale watu kama wana makosa, basi wapelekwe Mahakamani, ili yatoke maamuzi kama kufungwa au kama watapewa dhamana, lakini kuendelea kubakia pale hakuna kinachoendelea kwa kwaeli ni kuwadhalilisha na pia ni kuwapa mzigo walioko nyumbani kwa sababu pale polisi hawawapi chakula lazima chakula kitoke majumbani kwao, kama hawakupelekewa ina maana na wao wanaendelea kubakia na njaa. Kwa hiyo, niombe kwenye hili kwa sababu Mhe. Jaji Mkuu alitembelea na akaikuta hali hiyo naamini pengine na wale yanaweza yakafanya maamuzi yoyote ya kuwasaidia katika sakata lao hilo.

Mhe. Naibu Spika, agizo jengine la 12 kuhusu nyumba za Waheshimiwa Majaji. Kwa hiyo, naiomba serikali kwa sababu Majaji wana kazi kubwa sana hasa tumeambiwa kwa upande wa Pemba lakini pia na upande wa Unguja, kwa sababu wakati mwengine unaweza ukaenda Mahakamani ukafika saa nne Jaji hajaja kwa sababu hakai karibu na eneo ambalo anafanyia kazi. Kwa hivyo, naomba sana hizi nyumba zipate kujengwa kama zipo zilizokuwa hazijajengwa, basi zikarabatiwe ili ziweze kumalizika na hao Majaji wapate kufanya kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwenye hili pia na hawa watu ambao wameshahukumiwa na wamepelekwa kwenye magereza. Sasa hivi kuna maeneo ya Kinumoshi nyumba jamani zimekuwa ziko katika hali ngumu zinavuja hizo nyumba wanazokaa askari lakini pia na hizo nyumba ambazo wanakaa hao wafungwa nazo ziko katika hali ngumu sana. Naiomba serikali kwa kupitia bajeti ambazo zinakuja huko basi waweze kufanyiwa utaratibu zile nyumba ziweze kukarabatiwa, ili na wao baada ya kwenda kufanya kazi za ujenzi wa taifa au za kujifunza huko, basi angalau ikinyesha mvua usiku wapate kukaa katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho nikuombe tu wewe mwenyewe binafsi pamoja na Mhe. Waziri katika maelezo yake yote humu katika vifungu kwenye utekelezaji huwa kuna kauli inayozungumza au anaisema humu iliyoandikwa, kuwa mambo yote haya yatakaa sawa baada ya bajeti. Sasa naomba Mhe. Waziri atakapokuja atwambie bajeti gani haya mambo yatakaa sawa. Kila maeneo kasema yatakaa sawa baada ya bajeti, bajeti ya kipindi gani, tunataka atwambie ili na sisi watu wetu waweze kupata matumaini ya utekelezaji wa hii taarifa ambayo katuwasilishia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Masoud Abrahman Masoud. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Shehe Hamad Mattar ajitayarishe Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machache katika ripoti iliyoko mbele yetu. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na namuomba aniwezeshe nifanye lile ambalo kuwa nimelikusudia.

Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi nitoe pongezi kwa kamati ambayo kuwa imetoa maagizo kwa Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na baadae kutoa pongezi za dhati sana kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba yale maagizo yote yamefanyiwa kazi. Na katika kufanyiwa kazi hii ni imani yangu kwamba mambo yatakwenda sawa, kwa sababu wenzetu wameshayaona na wao wameyatoa kwa maandishi hapa sasa yabakie kwa vitendo.

Mhe. Naibu Spika, katika mchango wangu naipongeze wizara hii pale ilipofanya vyema kuhakikisha kwamba Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu imeongezwa kutoka bilioni moja na thamanini na sita milioni na laki sita hadi bilioni moja mia mbili na thalathilini na nane milioni. Hii itaweza kufanya kwamba sasa hii Ofisi ya Mkaguzi itekeleze lile agizo ambalo kuwa walisema kuwa zamani hawana wafanyakazi.

Kwa kweli, ofisi hii kuwa na wafanyakazi wa kutosha na wataalamu ni muhimu sana kwa sababu inategemea na wengi, kuna wale watu wanaostaafu mara nyingi sana huwa wanachelewa kupata haki zao kutokana na kwamba hesabu hazijafanywa, kwa sababu watu hao hao ndio watakaopita kuja kukagua hesabu za serikali kwenye mawizara. Lakini ndio hao hao watumishi watakaotumika katika kufanyakazi kuona kwamba *files* za wastaafu zinafanyiwa kazi mara moja.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba sasa kazi iliyo mbele yetu ni kwamba kazi hii itafanyika kwa haraka na mtu akistaafu ataweza kupata haki yake kwa wepesi sana. Kama ni hivyo, basi iwe ni hivyo na wafanyakazi sasa wakiwa na imani kila mmoja ana malengo yake kwamba mimi nikistaafu nataka nifanye hili yule afanye lile. Kwa hivyo, wizara sasa pamoja na kwamba idara husika imeshaleta maandalizi kutaka ajira sasa na kusimamia kuajiriwa hawa wafanyakazi ni jambo jengine.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa waziri asimamie hilo kwamba Ofisi hii ya *CAG* inapata wafanyakazi wa kutosha kwa kadiri inavyowezekana mapato yanavyoongezeka na wao waweze kutekeleza majukumu ya kufanya kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe waziri katika ripoti hii inaeleza kwamba wakati wa ukaguzi wanapokwenda katika ofisi au taaasisi za serikali wanakosa mashirikiano. Kwa kweli, najiuliza kwa nini mkaguzi anapokuja umfanye ni adui kama huna makosa. Hivyo, wazo langu kwamba naona kama ofisa yeyote anayekuwa hataki kutoa mashirikiano katika wakaguzi wanapokuja ina maana huyo tayari ana madhambi. Kwa hivyo, huyo mtu ni wa kumuangalia sana kwa nini akatae mkaguzi, akiwa anafanyakazi zake vizuri ana hamu sasa mkaguzi aje akuangalie nini umekosea. Lakini kama una madhambi

utamuona ni adui wako ni sawa sawa ukiwa barabarani kama chombo chako kina makosa unakimbia askari.

Kwa hivyo, suala hili vyema kwamba wale ambao wanafanya mtindo huu wa kuwakimbia wakaguzi basi waanze kutupiwa jicho jengine kubwa, wana matatizo na wakigundulika kuwa wana matatizo wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa namba 7 suala zima linalozungumzia agizo la 12 hatua zimechukuliwa kupatiwa Mamlaka ofisi ambayo kwamba kwa upande wa Pemba kufungua ofisi katika mikoa yote miwili. Hili lilikuwa ni agizo naomba nikinukuu:

"Kamati inasisitiza kuchukuliwa hatua za kupatiwa Ofisi Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi na wizara inahitaji kuwapatia ofisi ya kudumu kwa upande wa Pemba".

Niwapongeze hapo kwa sababu suala zima la kupata ofisi kwa ofisi hii ni muhimu na nimeiona katika Mkoa wa Kaskazini pale Mzambarauni na kama ilivyo kazi hii inahitaji mashirikiano, kwa sababu leo kama ofisi itakuwepo Chake Chake tu na mahitaji ni mengi, wala rushwa na watoa rushwa wametawanyika kila ikiwa maofisi yako karibu ni tayari kama mwananchi anaona kuna sehemu ya dalili ya rushwa anaweza kukimbia haraka. Hili jambo nalipongeza sana kuona kwamba ofisi zinaendelea kuenezwa sehemu baada ya sehemu kuona kwamba wale waovu wanapotokezea ni wepesi kwenda kuripoti Ofisi za Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi hawa na kuweza kuweka mtego. Lakini kama leo tatizo liko Wete ufate mpaka Chake Chake hata ukija iko wapi.

Lakini suala la kuweka ofisi karibu na makaazi katika wilaya na mkoa ni vizuri sana nalipongeza sana suala hili na waendelee kueneza ofisi hizi kila pahali hata isiwe Mkuu wa Mkoa tu hata katika Wilaya ziweko ofisi hizi.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 8 unasema usimamizi wa masuala ya kisheria. Kwa kweli, suala hili Mhe. Naibu Spika naunga mkono sana kuhusu usimamizi masuala ya sheria katika maofisi ya serikali. Ofisi za Serikali ninavyokumbuka iliangizwa kwamba kila Ofisi ya Serikali iwe na Mwanasheria. Lakini suala hili naona halijatekelezwa ipasavyo na ndipo pale inapokuja wakati mwengine serikali inakuwa na kesi zake leo mlalamikiwa anatia wakili halafu serikali unakuta inashindwa kwa nini na sisi tuna wanasheria wetu.

Lakini kama tunakuwa na mwanasheria atapata muda wa kusimamia ofisi yake inapotokezea tatizo la kisheria. Hili ni suala ambalo lilikuwa liendelee kutiliwa mkazo kwamba kila ofisi iwe na wanasheria wake baada ya kutumia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tu. Maana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ina mambo makubwa ya nchi ambayo kuwa inaweza kusimamia na wapi tupatiwe na mambo kama hayo. Hivyo, itakapokuwa inamfanywa mwanasheria ndani ya wizara itasaidia kuharakisha kesi na kutoka maamuzi haraka.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 9 kifungu namba 3 naomba ninukuu:

"Kamati inaagiza kufanyiwa kazi suala zima la udhalilishaji kwani imekuwa ni changamoto kubwa inayoikabili jamii na hata kukosekana imani kwa chombo cha Mahakama na jamii".

Kwa kweli, suala hili Mhe. Naibu Spika hili kila mmoja anaesimama anazungumza suala la udhalilishaji. Udhalilishaji imekuwa ni nyimbo ya kila siku ukisikia mawio huwezi kusikia mawio hujasikia suala la udhalilishaji, huwezi kusikiliza kesi za Mahakama usisikie suala la udhalilishaji.

Kutokana na hali hii naomba kushauri sana kwamba wizara iendelee kutoa elimu kwa jamii, kuona kwamba kila mmoja suala hili linamgusa kama ukimuoa mtoto wa mwenziwe na yeye ni wake kamkuta katika mazingira ambayo yanamashaka, basi na yeye aanze kutia mashaka na kuona kwamba anachukuwa hatua pale na ikibidi kuona kwamba anatakiwa kutoa ushahidi aweze kutoa ushahidi pale anapohitajika. Lakini leo unamkuta mtoto yuko katika mazingira mabaya kwa nini haunze wewe kumuhimiza wewe ondoa hapa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile mambo mengine yanachangia kwa mfano kama mashuleni kwetu tayari kwenye madrassa zetu walimu wetu nao wameanza kufanya mtindo huo wao wakati ni kioo cha jamii wanatakiwa waoneshe dalili nzuri. Lakini, leo wamekuwa mungunye wanaharibika ukubwani. Wao wanatakiwa wawe ni waangalifu sana na kuchunga watoto wale lakini sasa inakuwa yule unaempa kumchunga ndie anaeharibu hili jambo la kushikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, wananchi sote kwa pamoja tutoe ushirikiano kuhakikisha kwamba suala hili la udhalilishaji linapungua baada ya kuongezeka. Bado ni janga hili ambalo tunaendelea nalo, huwezi kukaa wiki moja ukawa husikii kesi hizi za udhalilishaji.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 11 wa agizo namba 8. Naomba ninukuu:

"Kamati inashauri wizara kufanya jitihada mategenezo jengo la Mahakama ya Mkoani kwa upande wa ndani ambao wa kukarabatiwa na mradi wa *ZUSP*".

Mhe. Naibu Spika, Mahakama ya Mkoani ni Mahakama ambayo kila mara inafanyiwa matengenezo.Kwa kweli, mimi nikiwa mmoja wapo nikiwa katika Ofisi ya Mahakama wakati niko huko tayari umeshafanywa. Mhe. Naibu Spika, kwa nini ofisi hii haihamii kwenye kiwanja chake ikafanya utaratibu wa kujenga ambacho kiko Mkoani pale itaweza kupata nafasi ya kutosha kiwanja kipo pazuri, nafasi ya kutosha.

Kwa hiyo, nashauru sana kwamba wizara ifanye mpango mzima ambao kuwa utaweza kujenga ofisi yake baada ya kukaa ofisi ile pale ukifika ofisi ina joto, ofisi nafasi ni ndogo, hivyo Mahakama wakati inaendesha inakuwa watu wanasumbuka sana. Pale wataweza kujenga jengo nafasi na kuweza wanaofika pale waweze kuondoka bila ya usumbufu wowote na kuona kwamba hawana madhila watakayoyapata.

Mhe. Naibu Spika, mwisho niende katika ukurasa namba 20 suala la maslahi ya wafanyakazi wa kima cha chini. Niipongeze serikali kwa kweli wananchi wafanyakazi ambao kuwa wameweza kuangaliwa kima cha chini cha mishahara yao lakini maslahi hayaji kwenye mshahara tu.

Kwa upande wa Pemba Mhe. Naibu Spika, niliwahi kutoa ushauri wangu suala zima la wizara hii Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuona kwamba wafanyakazi wa Pemba wanapata matatizo makubwa sana ya kwenda kazini na kurudi. Kweli, mishahara wameongezwa lakini mshahara huu ulioongezwa ni sawa unaendelea kubaki humo barabarani. Kwa mfano, mfanyakazi anayetoka Wete kuja Chake Chake na mfanyakazi anayetoka Mkoani kuja Chake Chake kwa kweli wanapata tabu sana.

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi hawa wanapata tabu sana kama siku zote wataweza nauli zao hicho kilichoongezwa kitabaki ni sawa sawa na hakuna. Hivyo, nilishauri na naendelea kushauri kwamba bado wazira ifanye utaratibu wa kuweza kupata mabasi mawili ambayo kuwa yataweza kuchukuwa wafanyakazi wa sehemu hizi kwa ajili ya kuwasaidia watumishi wetu, kama vile inavyofanya hapa kuchukuwa wafanyakazi kupeleka Mkokotoni Ofisi za Kaskazini huku inatoa fedha kwa ajili ya wafanyakazi wanaokwenda kule serikali inalipa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, na kule naomba sana ushauri huo nao ufanyiwe kazi kwamba yatafutwe mabasi mawili kwa utaratibu watakaona unafaa wafanyakazi nao waweze angalau kupumua waweze kufika kazini mapema na wa kuondoka waondoke kwa wakati. Leo hii mfanyakazi anaweza kufika saa 3 mfanyakazi hajafika kazini na ikifika saa 10 za usiku anajua nitafika vipi kazini. Lakini saa 8 tayari anaanza kutafuta nitaondoka vipi kwa maana hiyo hata kazi ofisini zipo anawacha. Kwa hivyo, utumishi hapo unazorota.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana waziri suala hili bado nalipigia kelele kwamba wafanyakazi wa Pemba waangaliwe mateso wanayoyapata kwenda na kurudi kazini.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchangio wangu huo naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Shehe Hamad Mattar, ahsante kwa mchango wako. Sasa mchangiaji anayefuata Mhe. Miraji Khamis Mussa na ajitayarishe Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi jioni hii kuchangia tu machache katika majibu ya utekelezaji ya Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Lakini naomba nitoe maelezo kabla kwenda katika vifungu ambavyo utekelezaji wake umeelezwa kwa umakini na Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri katika utaratibu ambao umeutumia humu maana wewe mwalimu na Naibu wako Mwanasheria. Kauli kubwa ya kitabu hichi katika utekelezaji wake maana yake itanatumika "ita" "ushauri umepokelewa" na asilimia 70 nimekihesabia mimi kila kitu

"ita, ita" . Sasa napata mashaka sana kama ni miezi sita sasa wizara "ita" inaendelea na kauli hiyo labda leo tukiondoka itakuwa kama ndio tumeachana na wewe katika utekelezaji wa majukumu na maazimio ya kamati.

Mhe. Naibu Spika, sasa niiombe sana kamati na ripoti yao waliokwenda kuisoma pale sijui walikipitia kwa umakini sana hichi kitabu na alau wakapunguza hizi kauli za "ita, ita". Sasa baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niende sasa kwa vipengele na maoni yangu kama utaratibu ambao unautumia.

Agizo la 2 linaloshusu utaratibu wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kunako eneo hili Mhe. Naibu Spika, nilisikia kutangazwa kwa ajira na walifanya *interview* na *selection* zilifanyika, lakini mpaka leo wizara haijatupa majibu mazuri nini kilichokwamisha hapa, na majibu ya hapa yamekuja yamefunga sana kama wao na taasisi wanategana. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri kwa sababu mambo yote yanamalizia kwake atuambie hasa suala hili baada ya *interview* hatua ipi imebakia, ili tuone sasa kweli anatekeleza majukumu vizuri na kama ambavyo tunamuamini katika kuutafutia ufumbuzi utekelezaji wa kamati.

Lakini Mhe. Naibu Spika, niende katika agizo la 12 ambalo kwa ujumla linaelezea kamati imeliona suala la nyumba za majaji litizamwe kwani lina umuhimu mkubwa. Jibu lake la utekelezaji ushauri umepokelewa na tuna ahidi maana kule tumeondoka kwenye "ita" tunakuja "tunaahidi" alau maana yake Mhe. Waziri alikuwa atwambie tu kwenye eneo hili serikali imeshaweza kujua gharama na gharama hizi tutazipeleka kwenye bajeti labda ya mwaka ujao au labda tutenga. Sasa majibu hayaoani kama kuna dhamira kubwa ya kutekeleza na kutatua tatizo hili yaani kama tunafungika hivi. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja na hapa atutosheleze vizuri kwa sababu yeye ni mwalimu na anatutega sana wanafunzi wako.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kwenye agizo la 17 la kamati. Pia nalo ukilipitia kuwa kuna suala la marekebisho ya Sheria Nam 4 ya mwaka 2005. Lakini nayo Sheria Nam. 4 ya mwaka 2005 itafanyiwa mapitio, lakini huku mbele yake kuna maelezo ambayo tatizo hili walisema kuna sheria namba 6 ambayo inaokoa tatizo hili.

Sasa tukamate wapi tumeshafikia pahala kwa sheria hii inatosheleza au kwamba kuna mapitio ni mapitio yepi yaliyobakia katika utekelezaji ambao Mhe. Waziri ameuelezea hapo atakwenda nao kwa mujibu wa maelezo yake. Hivyo, tunaomba ufafanuzi wa ziada zaidi ili leo tukiachana na yeye katika utekelezaji huu, tuone basi kamati ameifanyia haki katika kuisaidia kuyatekeleza yale maagizo.

Lakini niende Mhe. Naibu Spika, kwenye agizo la 22 ambalo kamati inaagiza Wizara ya Afya kufanya utaratibu wa kuongeza wafanyakazi kwa Ofisi na Wakala wa Mkemi Mkuu Pemba. Lakini katika majibu ya utekelezaji kuna kipengele ndio kinatutia mashaka, kinasema hivi hata hivyo wizara itakaa ndio hizi "ita" nilizozikataa, yaani ukija katika miezi sita sasa wizara haijakaa inatizama Mhe. Waziri na Waziri wanagharama gani ya kukutana kwao, maana hawa pia wanahitaji kulipwa. Sasa miezi sita hawajakaa leo wanakuja na kauli ndani ya Baraza hili kuwa watakaa. Kuna kauli ambazo nadhani

haziwezi kutumika kama kweli tuna nia njema ya kuyatekeleza maagizo ya kamati kama vile kamati zinashauri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika agizo la 2 ukurasa namba 20 ambalo linasema:

"Kamati inashauri kuangaliwa muongozo wa Utumishi wa Umma kwa watu wenye ulemavu"
Lakini hapa majibu ya Mhe. Waziri ameeleza vizuri na naomba nimshukuru. Lakini, kwa sababu ni miezi sita sasa hebu na ajira zimetoka na wamaetoa maelezo kwamba wanatoa kipaumbele hebu watwambie kipaumbele walichokitoa ndani ajira za hii miezi sita toka Machi mpaka sasa tunapokea majibu, kipaumbele gani walichokitoa na watu wangapi wenye ulemavu waliomba na wakasaidiwa kupata ajira. Hivyo, angalau wangeweka kwa takwimu kipindi hichi hichi tulichowashauri tunaweza tukapata uhalisia wa hapa kweli kama ilishauri lakini na utaratibu ulifuatwa. Kwa hivyo, naomba atakapokuja Mhe. Waziri kwa kitakwim labda atwambie tu hawakuomba na tukwenda kuhakiki hiyo kauli baada ya kuitoa kipi cha ukweli zaidi. *(Makofi)*

Naibu Spika, naomba niende na agizo jengine la 18. Hapa kamati ilishauri vifungu vya fedha vya Taasisi ya Nyaraka vilivyo serikalini viwe vinaingizwa katika Idara ya Nyaraka moja kwa moja. Lakini hapa pia kuna kauli katika utekelezaji aidha wizara tutawasiliana ndio hivi ambavyo ninasema mwenzetu waziri mwalimu na hata hapa walikuwepo na viti vya Baraza wako karibu. Kwa hivyo, pia mpaka leo hawajawasiliana maana yake wataendelea kuwasiliana.

Mhe. Naibu Spika, sasa tujue tu na hapa kwamba ah! Mhe. Waziri bado tuna kauli ya kuwa tutawasiliana, tatizo lao nini la kutokuwasiliana. Hapa tungepata jawabu labda tulikwisha wasiliana lakini kikwazo ni hiki, lakini baada ya miezi sita tunakuja na jawabu kuwa tutaendelea kuwasiliana. Haya maagizo tukiondoka leo watakuja kutuambia vipi tena na kikao kipi cha kuwa watakuwa wameshawasiliana. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atupe kwa ufupi kuna changamoto gani za kutokuwasilia kwao, ili tuweze kuwashauri kikao chengine waweze kuwasiliana vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, katika agizo la 23. Kamati inaagiza kupatiwa mafunzo ya watendaji wa Idara ya Nyaraka. Lakini hapa kwenye utekelezaji wa agizo umepokelewa na litafanyiwa kazi. Sasa tunapata mashaka, kwa sababu taasisi ile ilikumbwa na kadhia kubwa sana na mengi ambayo tuliyasema humu Barazani yalikuwa yanasaidia serikali, ili kutafuta muelekeo mwema na sio dhamira nyengine. Sasa leo kama kamati ilikwenda nayo ikaona kama kuna umuhimu wa watu wetu wale kupata mafunzo ndani ya miezi sita maana yake inarudi kauli ile ile.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye agizo hili atupe tu labda *highlight* kuwa ni gharama gani ambazo pengine zimeweza kukwamisha, hata katika hiyo bajeti tuliyonayo kusaidia kwa umuhimu wake tatizo hili mpaka leo linaendelea kupatiwa kauli kuwa limepokelewa na litafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kwenye agizo namba 27. Kamati inaagizo kuchukuliwa hatua zinazofaa kwa suala la kutuingizwa kwa fedha za matumizi moja kwa

moja katika baadhi ya taasisi Pemba. Hii kauli yake inalingana na ile ambayo niliitoa huko nyuma, kuwa wizara tutawasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango.

Kwa hivyo, naomba kama ambavyo Mhe. Waziri nilimuuliza kule, naomba na hapa nisirejee isipokuwa aje anipe jawabu linalolingana, kwa sababu yeye na Mhe. Wizara ya Fedha na Mipango nasema hata Barazani viti vyao vimekaribiana, sasa hamjawasiliana inaonekana kuna shida kidogo, ni shida ipi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwenye agizo Nam. 28. Kamati inaagiza kufanyiwa haraka uwepo wa taasisi zilizokosa ofisi huko Pemba.

Katika utekelezaji wizara itashirikiana na taasisi husika, maana taasisi imo ndani ya wizara, lakini mpaka leo itashirikiana na taasisi husika. Inaonekana Mhe. Waziri na waziri nilisema mwalimu "ita" hizi zinatupa mashaka. Sasa na hapa pia tuweke sawa tu maana pengine ni kauli tu iliyoandikwa humu na sisi wanafunzi wako ni wagumu wa kufahamu kuna kasoro kidogo. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi atufahamishe vizuri, "ita" nyingi kama hizi utekelezaji wake tunaelekea wapi, akeshatuweka sawa katika utaratibu huo basi, sisi tunashukuru.

Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi niunge mkono hoja kwa asilimia 70. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa. Sasa nitampa nafasi Mhe. Suleiman Sarahan Said na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii, ili kuichangia kamati yetu katika kuweza kuleta ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze sana kamati, lakini niipongeze sana wizara pamoja na waziri wake katika umoja wao ambao wanaendelea katika kuiweka vizuri wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, labda nikazie tu kidogo katika baadhi ya masuala kama tuseme litakuwa ni wazo langu. Mhe. Naibu Spika, hizi Mahakama ndogo ndogo ambazo ziko katika wilaya ama ziko katika maeneo, kwa kweli ziko katika hali ambayo hairidhishi. Hapa nimeona kwamba kuna fungu limetengwa kwa ajili ya Mahakama Kuu. Mahakama Kuu moja inaweza ikachukua zaidi ya Mahakama tano mpaka kumi pengine katika kujenga Mahakama zile ndogo ndogo. Kwa kweli, naona kwa muda huu Mahakama Kuu iliko Vuga, naona kama ilifanyiwa ukarabati pengine bado kutokana na hadhi ya jengo, pengine na kwamba haitoshelezi lakini naona bado inatizamika. Lakini hizi Mahakama nyengine naweza kusema ni baraza tu nyengine, kama Kengeja basi ni kama banda la kuuzia urojo.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, pale ni pahali panapohukumiwa haki. Wengine ndio wamemaliza maisha pale, wengine ndio wanafanya matatizo yao yatakuwa katika familia

imeharibika. Kwa hivyo, kimbilio letu Mhe. Naibu Spika, katika utawala bora ni Mahakama na mtu akitumia mkono wake inaonekana kwamba mtu huyu itakuwa amechukua hatua mkono mwake na atahadhibiwa. Lakini kama na mazingira nayo yatakuwa hayaridhishi basi baadhi ya watu wengine ndio hushindwa wakachukua sheria mkoni mwao.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri akajitahidi kuziangalia hizi Mahakama za chini zaidi kwanza katika kuboresha na watu kule chini wanakuwa hawana haki, kwa sababu uwezo wao wa kufuatilia kitu chao inakuwa ni kidogo, pamoja na mazingira yale ya umasikini na ufukara pia yanamsababishia kushindwa kuendelea na kesi. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri akalitizama hili la kuwaboreshea zaidi wananchi katika sehemu zile.

Lakini pili Mhe. Naibu Spika, najua sasa hivi Majaji wetu wanajitahidi sana, kwa kweli wanajitahidi katika kutenda haki na uwadilifu. Wapo, na wala siwezi kusema kwamba asilimia mia hawapo, waliokuwepo kidogo bado naweza kusema ni tamaa na mambo mengine yanayowapelekea huko, na pengine labda hajajifahamu maelezo yake ya kiapo chake cha utiifu, lakini sasa hivi wanajitahidi sana.

Mhe. Naibu Spika, katika kuwapongeza lakini pia na wao niwape pole, kwamba makazi na baadhi ya mambo yao na kwa kazi wanayoifanya inaonekana kidogo kuna *balance* iliyokuwa haiko sawa. Kutokana na hali hiyo, naomba wizara ikawatizama Majaji hawa, ili wakazidi kuwa roho zao zifunguke katika kutenda haki, maana yake wengine anaweza kughilibika kutokana na sababu zilizokuwa labda haziepukiki, lakini Mwenyezi Mungu atawasaidia, kwa sababu pale ukiachia masuala ya kisheria, lakini pale na masuala ya kidunia na Akhera pia yapo. Sasa mtu anapohukumu wengine wanaotizama Akhera basi wanaangalia na mbele, ili kuzidi kuitoa haki.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana katika mchango huu wa kuzungumzia habari ya Mahakama zisitengenezwe hizi ambazo zimeshakuwa na kiwango kidogo sana, tunapoteza pesa sana. Mhe. Naibu Spika, Mahakama zijengwe mpya hata kama ni moja baada ya moja. Kwa sababu Mahakama kama ya Mwanakwerekwe, yale yalikuwa ni mabanda ya maonesho hayakidhi. Kuna sehemu za kumuweka shahidi mbali asiweze kutoa ushahidi mwengine, lakini tunafikichana hapo hapo hata ule ushahidi wenyewe hautekelezeki. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri alitizame kwa kina ili liweze kuleta ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pia nizungumzie suala la matapeli. Kwa kweli, sijui nchi yetu mpaka sasa hivi iko vipi katika suala la nyaraka *fake.* Nyaraka *fake* ambazo naweza kusema za kila aina, kila siku zinapamba moto na mtu anajisifia nazo kuwa ana nyaraka *fake* wala hakuna sheria ambayo inaweza kumkamata. Hivyo, kwanza haogopi, tena anajisifia, maana yake mtu anakuja na *document* Mahakamani akijua nyaraka hii ni *fake*, lakini bado anakuja nayo mwenyewe na kujisifia hii ndio *document* yangu. Matokeo yake Jaji anamuambia hii haifai ni *fake*, anaondoka na *document* yake.

Mhe. Naibu Spika, yule anaisumbua serikali, anawasumbua wananchi, anambabaisha Jaji ili atoe hukumu iliyokuwa sio. Kwa hivyo, watu kama wale Mhe. Naibu Spika,

wanatakiwa wachukuliwe hatua za kisheria, lazima hapa tuusaidie umma, katika kuangalia mtu yeyote atakayepatikana na nyaraka *fake*, basi achukuliwe hatua za kinidhamu. Kwa maana hiyo, sio mpaka mtu aseme ukitaka mshitaki, ukitaka ufanye hivi, wengine hawana nguvu za kushtaki. Lakini kama mtu kenda na *document fake* mwenyewe Mahakamani, basi ikikamatwa na yeye awekwe ndani atajua ilipotoka na itakuwa ni funzo na somo kwa wengine.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka nizungumze na watendaji katika maofisi. Mhe. Naibu Spika, watendaji katika maofisi hawaogopi kuiba, hawaogopi jambo lolote. Maana yake sheria hata kama ukimkamata huna pa kumpeleka na hata ukimpeleka basi atatoka, kwa sababu sifikirii kama sheria zetu zina mkandamizo maalum kwa mtu. Nafikiri kubwa labda itafika siku aambiwe wewe wacha kazi umestaafishwa, lakini sifikirii kama kuna kitu chengine ambacho kinafanywa. Kwa hivyo, wengine wanafanya kama bahati mbaya, na wengine wanafanya kwa makusudi na ndio mtindo wao na kwa sababu sheria inaonekana haijawajibika vya kutosha.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumze kwamba suala hili la rushwa bado Mhe. Naibu Spika, kwa upande wetu wa Zanzibar limekamata hatamu sana. Wanajua kwamba mtu yeyote asiyetengeneza rushwa basi hafanikiwi katika shughuli yake yoyote ile, ikiwa mtu hujatengeneza mazingira ya rushwa basi wewe hufanikiwi. Sasa Mhe. Naibu Spika, rushwa ni adui wa haki, kwa kweli mnyonge anakuwa hana haki pale. Kwa hivyo, ninashauri sana Mhe. Waziri akalichukulia kwa jicho la huruma suala la rushwa likaweza kupungua kwa asilimia kubwa sana.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Naibu Spika, naomba kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa upande wa Pemba iweze kufunguliwa au iweze kuboreshwa zaidi, kwa sababu kesi ziko na matatizo yako, lakini bado tunaona matatizo ya kupata baadhi ya mambo Unguja inakuwa kidogo yanapunguza ile hamasa ya kutaka kutetea haki yake.

Kwa hivyo, Mhe. Mwanasheria Mkuu itakapofunguliwa ofisi Pemba au ikawa kuna maboresho zaidi, pia Mwanasheria Mkuu wa huku atapunguza matatizo, inawezekana yakapungua sana kila mmoja Mwanasheria Mkuu Zanzibar ikawa *files* zinarundikana sana.

Pia, Mahakama ya Kadhi Pemba. Mhe. Naibu Spika, nako kule kuna matatizo mengi ya Kadhi. Ingawa labda kuna jopo kule la Masheikh wanatatua baadhi ya kesi, lakini bado kama sheria basi Mahakama ya Kadhi kwa upande wa Pemba ikafanyakazi zaidi kwa sababu nako kuna matatizo yake.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kumtakia na kumueleza Mhe. Waziri kwamba sheria tunapanga kila siku na kila siku tunapiga kelele suala la udhalilishaji, lakini sijui tafiti gani zinaonesha kwamba ni kitu gani kilichopandisha mori mpaka udhalilishaji ukaongezeka pamoja na adhabu zinazotolewa, pamoja na mambo mengine. Lakini suala la udhalilishaji bado ni changamoto.

Kutokana na hali hiyo, naiomba wizara ikafanya utafiti wa kutosha, ili ikaangalia ni kitu gani kinachosababisha udhalilishaji ukaongezeka, hata kama kuna adhabu ambazo

zinatolewa lakini bado ni kiini au ni kitu gani ambacho kinasababisha kwamba suala hili liweze kuleta madhara zaidi na sio suala zuri. Kuna baadhi ya watoto tunawakatisha maisha, kwa kweli linakuwa ni jambo ambalo ni baya sana. Sasa naomba sana Mhe. Naibu Spika, ukiacha kesi, lakini tukafanya utafiti wa kutosha ni kitu gani hasa kinachowafanya watu wakimbilie huko.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe malizia. Nakupa dakika moja ya kumaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Dakika ngapi moja. Eeh!

Mhe. Naibu Spika, basi mimi nitasema mbio mbio kuhusu kupatiwa kwa vitendea kazi katika hizi Tume za Maadili, ambazo ndio tunazozitegemea katika kufanikisha. Kwa hivyo, ninaomba hawa watu wizara ijitahidi kuwapatia vitendea kazi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la utumishi wa umma nimeona kidogo tumechanganya mambo sana. Sisi bado tuna vijana wengi ambao wamesoma na wengine hawakusoma, lakini bado tunawachanganya. Unatangaza elimu ya kidato fulani, anaingia aliyesoma na asiyesoma, kwa vyovyote utamchukua aliyesoma, kwa hivyo anakosa haki yule mtu ambaye hakusoma. Lakini yule ile kazi uliyomtangazia kama ni ya kupiga deki au ya kufanya kitu gani haifanyi, ule unakuwa ni uchochoro wa kupita na pale inakuwa suala lile halitekelezeki tena, baada ya miezi mitatu anachukua kozi nyengine anaondoka yale masuala yanakuwa hayaendi. Sasa yule mtu aliyekuwa hakusoma ile nafasi yake imepotea na ule utendaji na ufanisi unakuwa haupatikani.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni suala la faini. Naomba sana Mahakama, katika kesi ambazo zinaonekana hazina madhara makubwa basi faini ikatumika zaidi, ili kupunguza msongamano wa kule Mahakamani na pia serikali kupata mapato, ili kupunguza matatizo pamoja na makesi na mambo chungu nzima. Kwa hivyo, naomba sana kama kesi hazina madhara basi faini ikatumika zaidi, ingawa wakati mwengine tunasema inakuwa na zote mbili yaani kifungo na faini. Lakini ningeomba sana faini ikatumika zaidi kwa zile kesi ambazo hazina madhara.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, muda wako umekwisha.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kusema machache katika wizara yetu hii. Awali ya yote nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana mahala hapa.

Lakini pia nichukuwe fursa hii kuipongeza sana kamati kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameitoa kuishauri wizara. Pia nichukuwe fursa ya pekee kumshukuru na kumpongeza Makamu Mwenyekiti kwa uwasilishaji wake mzuri na fasaha sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu katika agizo namba 3. Mhe. Naibu Spika, agizo namba 3 limeeleza suala zima la udhalilishaji na ukubwa wa changamoto zake ambazo zipo. Lakini katika utekelezaji tumeelezwa tokea Machi, 2013 kuna mkakati maalum wa kupambana na kesi za udhalilishaji. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri anieleze ni kesi ngapi zimeweza kupatiwa hukumu tangu mkakati huu umeanza.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika agizo namba 11, ambalo linaeleza upatikana wa fedha za mashahidi, ambapo kamati imesisitiza upatikanaji wa fedha, lakini utekelezaji serikali imekiri kama ni kweli fedha hizi zinapatikana kwa mashahidi. Lakini mimi ningeomba kuna suala la *assessors* katika Mahakama zetu. Kuna fedha, lakini kwanza niseme mimi nilikuwa mjumbe katika hawa *assessors* kwenye Mahakama ya Mfenesini, kwa hivyo naelewa vizuri. Wakati naondoka niliwacha nadai fedha nyingi nikawa sijalipwa, lakini kutokana na moyo wangu mwenyewe fedha hiyo nimesamehe kwamba nimeondoka mahala pale na Mwenyezi Mungu ameniweka mahala pengine, nimesamehe. Lakini kuna wenzangu ambao wapo *assessors* pale wanafanyakazi mpaka muda huu na wanadai fedha zao za nyuma nyingi hawajalipwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, je, ni lini serikali itaweza kuwapatia fedha zao hizi ili na wao waweze kufika Mahakamani, kwa sababu saa nyengine inakuwa fedha zinachelewa lakini wanaweza kutumia fedha zao wenyewe kwa kwenda kushughulikia kesi na wanapokosa fedha basi inawezekana pia ucheleweshaji wa kesi unatokea kwa sababu wanakuwa hawana nauli za kuendea.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala zima ambalo wenzangu wengi wameligusia, ni suala zima la nyumba za Majaji hasa kwa kule Pemba. Mhe. Naibu Spika, mimi niseme mwenyewe pia nilikuwa mjumbe miaka mitano iliyopita katika Kamati ya Katiba na Sheria, suala hili tulilizungumza sana kwamba nyumba ziko vibaya za Majaji na pia Mahakama zetu wanazofanyia kazi nazo ni mbovu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naiomba serikali majibu yanapokuwa hivi mepesi zaidi bila ya kuonekana angalau hatua moja imechukuliwa, basi naiomba sana serikali kuweza kushughulikia nyumba hizi za Majaji wetu, lakini pia na kuzishughulikia Mahakama zikawa katika hali nzuri. Kwa kweli, niseme katika Mahakama za Pemba tulipotembea wakati huo zilikuwa mbovu zaidi na kila siku zinavyozidi maana yake zinazidi kuharibika zaidi. Hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kwa kuliona hilo basi tuweze kujipanga vizuri, ili tuweze kutatua changamoto hii ya majengo haya ya Mahakama, lakini na majengo ya Makadhi. Kuliko kuanza kufikiria kujenga Mahakama nyengine mpya wakati hizi ambazo tunazifanyia kazi ni mbovu na ziko katika hali ngumu, naomba sana hili.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna agizo la 18 ambalo linaeleza katika Ofisi ya Walaka wa Mkemia Mkuu. Mhe. Naibu Spika, ofisi hii imetakiwa kuwa na uwadilifu mkubwa kutokana na suala zima la madawa ya kulevya. Lakini nimekuwa nikijiuliza kwa sababu tulikuwa tunapata taarifa mbali mbali, Mkemia hapa serikali imeeleza kama anaonekana ni mtu muadilifu, na kwa kuwa wao wanamuelewa vizuri na mimi nataka nikiri hilo. Sambamba na hilo, zile taarifa tunazozipata baada ya kukamatwa ule unga halafu sikuya pili au ya tatu ukaambiwa unga huu umebadilika umekuwa siyo unga wa madawa ya kulevya umekuwa sembe, umekuwa unga wa ngano. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hili linakuwa linatokea wapi. Kutokana na hali hiyo, naiomba sana serikali kwa sababu suala zima la madawa ya kulevya ni jambo ambalo linatuumiza vichwa kwani linapoteza nguvu kazi ya taifa. Suala hili pale unapobadilika unga ile taasisi inakabidhiwa unga ukabadilika, basi naomba serikali ichukue hatua za kinidhamu kabisa kwa wale watakaobainika kwamba wamekabidhiwa unga halafu wao wakaweza kubadilisha na wakasema kwamba sio unga ni kitu chengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme kwa hayo machache naunga mkono ripoti hii kwa asilimia 95 na zile tano nitaziengezwa pale ambapo nitajibiwa maswali yangu haya. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla, sasa hivi tutampa nafasi Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Khamis Juma Mwalim, ambaye atakuja kutujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia fursa hii kutoa baadhi ya ufafanuzi wa hoja juu ya baadhi ya maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, nianze moja kwa moja mchango wangu katika suala la Mahakama. Baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wamepaza sauti zao kuzungumzia kwamba baadhi ya Mahakama zipo katika hali siyo ya kuridhisha.

Mhe. Naibu Spika, naomba ifahamike kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Mahakama zetu zinafanyiwa marekebisho pale ambapo panastahiki kufanya hivyo. Sote ni mashahidi tukienda Pemba Mahakama ya Chake Chake *Alhamdulillahi* ilikuwa katika hali ambayo haikuwa inaridhisha, lakini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imejitahidi na imefanya marekebisho makubwa pale na sasa hivi ukienda utaona kwamba ile Mahakama ni mpya na ukweli wenyewe imefanyiwa marekebisho isipokuwa marekebisho yalikuwa ya yali ya juu kabisa.

Sambamba na hilo hata kwa upande wa Makunduchi kulikuwa na Mahakama yetu kule ambayo nayo ilikuwa katika hali ambayo hairidhishi, lakini tunashukuru kwamba tumepiga hatua na Mahakama ile ukienda utadhania ni mpya.

Mhe. Naibu Spika, tunayo Mahakama yetu Mwanakwerekwe nayo hii ilikuwa katika hali ambayo hairidhishi, lakini nimwambie Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe angalau siku mbili hizi katika pita pita yao wanapokuwa wanakuja Baraza la Wawakilishi, basi wapitie pale Mahakama ya Mwanakwerekwe. Mahakama ile ibadilika, sasa hivi inavutia na imeandaa mazingira mazuri ya wafanyakazi na wananchi ambao wanafika pale kupata haki zao. Kwa kweli, serika inajitahidi kuhakikisha kwamba zinafanyiwa marekebisho Mahakama zetu, ili ziwe na hadhi nzuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pia Waheshimiwa Wajumbe wengine walikuwa wanazungumzia suala zima la elimu katika suala la udhalilishaji. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikipiga hatua sana katika taasisi mbali mbali kutoa baadhi ya vipindi kutoa elimu inayohusiana na masuala ya udhalilishaji. Serikali haijakaa kimya, serikali ina njia mbali mbali kuhakikisha suala hili linafikia hatua nzuri zaidi ya kukomeshwa nchi kwetu. Nadhani jitihada zimeonekana, tunayo Mahakama ya Watoto Mahonda na hii ni miongoni mwa jitihada za serikali kuhakikisha kwamba suala la udhalilishaji linafikia kikomo.

Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa kwamba hivi karibuni kutaletwa Mswada wa Sheria ya Adhabu, kwa hivyo hiyo nayo itakuwa ni miongoni mwa suluhishi. Mswada utakaoletwa hapa kwa wale wanaojaribu kuwaficha wale wadhalilishaji hivyo na nao tuwahesabu kwa maana na wao kwamba wamefanya lile kosa, kwa hivyo sheria kali hii itawakumba. Serikali inajitahidi kwa hayo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuna mjumbe mwengine alizungumza suala zima kwamba walimu wa vyuo wachukuliwe hatua ambao wanadhalilishwa watoto. Hili liko wazi, tumesikia katika vyombo vya habari, tunasikia katika taasisi mbali mbali kwamba watoto ambao wanadhalilishwa na walimu basi walimu hatujalishi uwalimu wao kama wamefanya kosa bila ya kujali mwalimu basi sheria itafata mkondo wake. Serikali inajitahidi kufanya yote hayo.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa Waheshimiwa Wajumbe alizungumza kwamba suala la magereza kwamba yaweze kufanyiwa marekebisho. Ni sawa ingawa kwamba hili litakuwa zaidi lipo katika Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, ambao ndiyo wanaoshughulikia suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa upande wangu suala la wastaafu wanapostaafu kucheleweshewa zile stahiki zao. Hili nalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Mjumbe mmoja.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli taasisi husika kwa wale wastaafu wanapofikia umri wa kustaafu, maafisa utumishi pale huwa wanatakikana kupeleka taarifa ile kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mashirika (*CAG*) lakini sio kwamba akifika pale tu moja kwa moja lile *file* linapelekwa sehemu husika inabidi *CAG* pamoja na mengine alikaguwe lile *file*. Kwa hivyo, kama zitakuwa taarifa zimekamilika juu ya huyu anayestaafu, basi *CAG* anaandika taarifa ile kupeleka Wizara ya Fedha kwa ajili ya kupata malipo.

Mhe. Naibu Spika, si kweli kwa maana kwamba hawa wanachelewesha kupata stahiki zao, isipokuwa ucheleweshaji ule unategemea kwamba ni maandalizi mazuri, ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka sio kwamba baada ya kulekwa *file* kwa *CAG* kule na wao waweze kupata hiyo stahiki yao, inabidi ofisi ya *CAG* ikae ichunguze na iangalie, kama kuna makosa na wakati mwengine inawezekana ikawa kuna makosa ambayo yanatokea katika taasisi husika. Kwa hivyo, *CAG* moja kwa moja bila ya kuangalia vizuri inawezekana yule mstaafu mwenyewe atakosa haki yake ya msingi. Serikali inajitahidi

kuhakikisha kwamba mara tu hawa wastaafu wanapofikia umri wa kustaafu basi wawe wanapata fedha zao kwa wakati maalum.

Mhe. Naibu Spika, ni hayo tu na ninaunga mkono ripoti hii kwa 100%. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa tumpe nafasi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kufika hatua hii tulivyofika sasa hivi. Niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia nao ni kama hawa wafuatao:

1) Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
2) Mhe. Ali Suleiman Ali
3) Mhe. Omar Seif Abeid
4) Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
5) Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud
6) Mhe. Shehe Hamad Mattar
7) Mhe. Miraji Khamis Mussa
8) Mhe. Suleiman Sarahan Said
9) Mhe. Panya Ali Abdalla
10) Mhe. Khamis Juma Maalim
11) Mhe. Salma Mussa Bila, amechangia kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana kwa namna ulivyokiendesha kikao chetu hiki. Nimegundua kwamba Waheshimiwa Wajumbe wengi waliochangia waliosimama walikuwa wamekuja na hoja mpya. Sasa hivi tunahitajia kuzifanyia kazi kwenye kikao kinachokuja, kwa sababu yale mengine yaliyozungumzwa kwenye hoja 87 mengine hayakuwemo. Sisi tulichokuja nacho hapa, silaha zetu zilikwenda kwenye zile hoja 87, sasa haya mengine yamejitokeza hapa hapa. Tutayachukua kama ile lugha ambayo Mhe. Miraji Khamis Mussa haitaki, tuta, ita, ndiyo tunaendelea nayo itabidi kutokana na hivi.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika nikushukuru kwamba ulitoa muongozo mzuri kwamba haya mengine itabidi tuyafanyie kazi baadaye. Lakini kwa ujumla nimenukuu vifungu 15 ambavyo nitavitolea ufafanuzi kwa ujumla.

Waheshimiwa wengi kwa ujumla wameshangia masuala ya mafungu ya fedha haya kwenye taasisi mbali mbali ikiwemo Ofisi ya Mufti, Tume ya Maadili, Idara ya Nyaraka na kadhalika. Tumesema kwa vile mwaka huu hatukuwahi kwa hiyo bajeti inayokuja tutahakikisha hilo tutalifanyia kazi vizuri na tumeshawasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango, nashukuru tumewasiliana sana na Wizara ya Fedha na Mipango kwa masuala mengi sana kila wakati katika masuala haya, ili kuhakikisha Ofisi ya Mufti, Tume ya Maadili, Idara ya Nyaraka na wengineo kama ilivyokuwa zamani, basi wanapata mafungu yao kikawaida.

Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri amezungumza masuala ya Mahakama, hilo halina matatizo kalizungumza vizuri. Isipokuwa kuna Mhe. Mjumbe mmoja alizungumzia suala zima kwamba fungu la mashahidi lile halitoshi kwamba wanapewa nauli tu mengine hawapewi, lakini si angalau kidogo wanapewa, tushukuruni kile wanachopewa, sasa wakeshapewa nauli tukatafute na mambo mengine, sasa biashara hii itakuwa kubwa sana. Kwa hivyo, kwa sasa hivi kwanza tukubali tuwape nauli zao na gharama zile ambazo wanatumia njiani mpaka wakafika pale Mahakamani.

Mhe. Naibu Spika, jengine Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumza kuhusu ufinyu wa ofisi mbali mbali, vimetajwa ofisi nyingi hapa zinazohitajiwa kuwa na ofisi. Tumesema Pemba tunajengo letu jipya linajengwa pale kwa mashirikiano ya wizara tatu. Kwa zile ofisi zote ambazo hazina ofisi za kudumu kule Pemba tutahakikisha kwamba sisi katika jengo hili jipya tunawapatia ofisi zile.

Tume ya Maadili ni moja ambayo itapatiwa Ofisi kule Pemba lakini pia kwa hapa Unguja nimesema kwenye taarifa yangu ya utekelezaji kwamba tayari iliyokuwa Ofisi ya Ubalozi wa Misri au Egypt, jengo lile tumeshapewa na litatumika na Tume ya Maadili, watapewa kama ni jengo lao.

Jengine kuhusu Idara ya Nyaraka vifaa vile vilivyoletwa. Mhe. Mjumbe mmoja aliniuliza ni vifaa gani hivyo. Tutizameni ukurasa wa 27 repoti yetu hii ya Utekelezaji vifaa vyote vimeorodheshwa pale ambavyo tumewapatia nyaraka ikiwa kuna ma *AC*, *Scaner*, makaratasi, madawa, *gloves* na mambo mengineyo. Mhe. Naibu Spika, mambo yote yamo katika ukurasa wa 27 Waheshimiwa Wajumbe tusomeni tutaona.

Mhe. Naibu Spika, hapafu vile vile kumezungumza suala ya Sheria ya Ndoa. Mhe. Naibu Spika, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba Sheria ya Ndoa tutaileta hapa Barazani hivi karibuni tuje tuifanyie kazi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf amezungumzia sana suala la adhabu kali kwa walimu wa madrasa wanaodhalilisha watoto na wengineo. Hili tunavishukuru vyombo vyetu vya sheria hivi sasa vinaangalia vizuri suala hilo, Mahakama zetu na Mwendesha Mashtaka wanalifanyia kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mmoja alisema kwamba hawa wafanyakazi nadhani Mhe. Omar Seif Abeid bahati mbaya hayupo, ndiyo matatizo wakati mwengine tunajibu wenyewe hawapo na halafu tunakuja kuulizwa tena. Mhe. Omar Seif Abeid alisema kwamba, hawa wafanyakazi kwa nini hatujawahamisha mpaka leo moja moja. Taratibu za kiutumishi zipo huwezi tu kumuhamisha mfanyakazi kiholela lazima tufuate utaratibu wa Utumishi kwa Sheria ya Utumishi wa Umma kuna utaratibu wake. Kwenye taarifa yangu nimesema kwamba wafanyakazi hawa kutokana na mahitaji yaliyopo na umuhimu wao tutawapeleka moja kwa moja kwenye Tume ya Maadili. Lakini Tume ya Maadili huwezi kumpeleka mfanyakazi yeyote tu kuna mambo ni lazima tuyaangalie vizuri, nadhani hilo linatoshelezesha kwa sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, pia nilipata swali kwa baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe, kwamba Ofisi ya *CAG* ilikuwa imeshafanya usajili, imeshachagua wafanyakazi lakini kwa nini

hawajaajiriwa mpaka leo. Tatizo ni kwamba Ofisi ya *CAG* Bodi yake imemaliza muda wake na hawezi kuchukua maamuzi makubwa kama haya kama hawajapata ushauri wa Bodi. Kwa hivyo, hatuwezi kuchukua lakini sasa hivi taratibu za kuunda bodi mpya zinaendelea. Hivi karibuni katika mchanganyiko wa marekebisho ya sheria, na sheria hii vile vile imo na tutaileta Barazani na tutarekebisha na hatua hizo zitachukuliwa na wafanyakazi hawa wataajiriwa wote kama tulivyokusudia.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf nadhani alizungumzia suala zima la *ZAECA* wapewe fungu la pesa ili watakavyotaka ushahidi wampe mtu fungu la pesa. Sasa hili lina mambo ya kisheria kidogo, *ZAECA* na wao wanapewa pesa sasa ili wakawakamatishe watu kuna utaratibu wake, hatuwezi kutangaza hadharani mambo kama haya isipokuwa tu nimepata *point* yake tutaiangalia vizuri.

Halafu ameuliza swali *CAG* iko wapi? *CAG* ipo chini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma, Utawala Bora, ndipo walipo na mimi ndiyo ninawasilisha bajeti yake. Sasa suala hili kwamba haji kwenye kamati ni suala la kulirekebisha tu, lakini wajibu wa utaratibu ulivyo *CAG* ripoti zake anazitayarisha anampelekea Mhe. Rais, baadaye Mhe. Rais anamtafuta waziri anayehusika na masuala yale anawasilisha Barazani. Baadaye *PAC* wao wanafuatilia *concerns* zote yale maeneo yote kwa mashirikiano ya pamoja kati ya *PAC* na wizara yetu tunashirikiana kwa pamoja. Kwa hivyo, yupo kwetu sote lakini zaidi yupo Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, kuna Mhe. Mjumbe mmoja alizungumza suala la nyumba za wanafunzi. Kwa bahari nzuri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kesho watakuja na taarifa yao, kama hili lilikuwemo katika maoni au utekelezaji au maagizo basi atatoa ufafanuzi, lakini hili sio la wizara yangu la kutengeneza nyumba zile, tuliache kama lilivyo wahusika watalifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kuhusu Mkemia Mkuu, Mhe. Miraji Khamis Mussa alisema lakini hayupo, tutakaa mpaka lini na Wizara ya Afya, kwani jambo hili ni la zamani hatujalifanyia kazi. Ndiyo kama nilivyosema kuna suala la ajira, lazima watu wakae, wazungumze na ndiyo utaratibu ulivyo. Wenzetu wa Wizara ya Afya hili suala ni lao, wao walianzishe halafu sisi tutoe vibali vya kuwaajiri watu wale kwa wale wafanyakazi ambao wanaohusika katika sehemu ya kitengo kile.

Mhe. Naibu Spika, mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote walichangia na tutajitahidi kushirikiana nao tena, kwa zile hoja ambazo ni mpya tukijaalia tutazifanyia utaratibu mwengine. Lakini pia nimuombe sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwamba yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, ajitahidi sana bahati mbaya au nzuri alikwenda kidogo kutembea mahali kufanya kazi, kwa hivyo kaja na nguvu mpya. Nampongeza sana maoni yake tumeyachukua na *Inshaallah* tukijaaliwa tutayafanyia kazi.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwaulize kama mmepokea ripoti ya Mhe. Waziri mtanyoosho mikono. Ahsanteni sana.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue fursa hii kuwashukuru sana na kuwapongeza kwa utulivu wenu pamoja na michango mbali mbali ambayo mmeitoa tangu asubuhi mpaka kufikia muda huu. Sasa naakhirisha kikao hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1:27 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 03/10/2017 saa 3:00 asubuhi)